

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA NNE**

**Kikao cha Nane – Tarehe 9 Septemba, 2021**

*(Bunge Lilianza Saa Nane Mchana)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, ndc – KATIBU WA BUNGE:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

**NAIBU SPIKA:** Hati za kuwasilisha mezani, Waziri wa Viwanda na Biashara, kwa niaba yake Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara Mheshimiwa Exaud Kigahe.

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:**

Maelezo ya Waziri wa Viwanda na Biashara Kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa Eneo Huru la Biashara la Afrika (*Agreement Establishing African Continental Free Trade Area – AfCFTA*).

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira.

**MHE. DKT. ALFRED J. KIMEA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira Kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa Eneo Huru la Biashara la Afrika (*Agreement Establishing African Continental Free Trade Area – AfCFTA*).

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Dkt. Alfred,

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, ndc – KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI KWA WAZIRI MKUU**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge maswali kwa Waziri Mkuu, leo ni siku Alhamisi, ninayo majina hapa ya Wabunge ambao wamejiorodhesha kwa ajili ya kuuliza maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nimuite Mheshimiwa Waziri Mkuu asogee sehemu ya kujibia maswali. (*Makoff*)

Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mbunge wa Mlalo swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili niulize swali la kwanza kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera yetu ya Elimu hasa elimu ya msingi imeelekeza kwamba elimu ya msingi ni bure kuanzia ngazi ya msingi; na zoezi hili lilikuwa linafanyika vizuri sana, tunaipongeza sana Serikali kwa hatua hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu nilitaka kuufahamu, ni upi mkakati wa Serikali katika Sera ya Afya angalau sasa katika afya msingi kwa maana ya zahanati na vituo vya afya kuweka eneo hili tupate huduma za afya bure?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu kwa swali hilo.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shangazi, Mbunge wa Mlalo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Serikali yetu imeandaa sera upande wa elimu na kuifanya elimu sasa ipatikane bure kuanzia elimu ya awali mpaka kiwango cha sekondari, kidato cha nne na mkakati huu unasaidia sana kuwapunguzia wazazi gharama za kumpeleka mtoto shule na huku tukiwa pia tumeweka ulazima wa kila mtoto wa Kitanzania kupata elimu ya msingi ambayo kwa sasa inaenda mpaka kidato cha nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge anataka kujua nini mpango wa Serikali wa Sera aina ile ile ya elimu kuifanya pia kwenye sekta ya afya ili tuweze kutoa huduma za afya bure.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka tu kueleza kwamba tunaendelea kufanya mapitio ya sera zetu na hasa kwenye sekta ya huduma za jamii ili Serikali yetu iweze kutoa ikiwezekana unafuu mkubwa kwenye utoaji wa huduma za jamii kwa Watanzania ikiwemo na sekta ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pindi tutakapofanya mapitio haya na kukamilisha kuona uwezo wa kifedha wa kugharamia kwa upande mwingine, kwa maana ya kupata vifaa tiba, utafiti na maeneo mengine yote, Serikali itatoa tangazo wakati pale tutakapokuwa tumekamilisha utafiti huo ambao sasa hivi wataalam wetu wanaufanyia mapitio, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas, Mbunge wa Kinondoni, swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba na mimi nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa majibu mazuri ya swali lililopita lakini naomba nimuulize juu ya changamoto ambazo zipo katika matumizi ya Sheria ya *Road Traffic (Road Traffic Act)*, ile *Cap 168* pamoja na Kanuni zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo na matatizo ya matumizi ya barabara hasa kwa waendesha pikipiki/bodaboda ambao wanakiuka sheria zilizopo katika mahitaji ya jinsi gani ya kuendesha vyombo vyao. Na sasa imezidi pale Dar es salaam hasa watumiaji wa barabara za mwendokasi, madereva wa mwendokasi wanapita kwenye taa nyekundu; hadi jana usiku saa moja na nusu wameua vijana wawili.

Ni nini kauli ya Serikali katika kuhakikisha watumiaji wote wa vyombo vya moto barabarani wanafuata sheria na kwamba polisi/trafiki wanasimamia sheria zile ipasavyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu kwa swali hilo.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abbas Tarimba, Mbunge wa Kinondoni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria hizi ambazo tumeziweka sisi hapa Bungeni tunatarajia kwamba kila Mtanzania atakuwa anatekeleza wajibu wake bila ya kushurutishwa. Matumizi ya barabara yameainishwa kikamilifu kupitia sheria zetu na usimamizi unaendelea pia kwa vyombo ambavyo tumevipa jukumu la kusimamia kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini usimamizi wa sheria hautakiwi usimamiwe na Jeshi la Polisi peke yake tu, kila Mtanzania anatakiwa kufuata sheria pale ambapo sheria imeshatungwa na inataka itekelezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba watumiaji wa pikipiki walio wengi hawajali matumizi haya ya sheria zetu na kujali kwamba sheria hizi ni lazima zitekelezwe. Lakini pia Jeshi letu la Polisi linacho kitengo kinatoa elimu kila siku, na Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote mnajua kwenye televisheni zetu za *TBC, ITV, Star TV* lakini pia Azam tumetengewa muda na Jeshi la Polisi linafanya kazi hiyo vizuri sana, kuelimisha Watanzania kuhusu matumizi sahihi ya barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunasimamia sheria hizi nitoe wito kwa watumiaji wa barabara hasa watumiaji wa vyombo vya moto wote kwamba ni muhimu sana kuzingatia Sheria za Barabarani. Hii ni muhimu sana kwa sababu inalinda uhai wa Watanzania wote, kuanzia yeye mtumiaji wa chombo chenye cha moto, watumiaji wa njia hizo wanaotumia kwenda kwa miguu lakini pia pamoja na wale wanaotumia barabara hizi za mwendokasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu njia hii ya mwendokasi tumeshaeleza wazi, kwamba njia hii tumeitenga maalum kwa ajili ya magari ya mwendokasi, lakini pia tumetenga njia nyingine kwa ajili ya magari yetu ya kawaida. Tumejenga na njia ya pembezoni ya watembeaji wa miguu pamoja na vyombo vingine vya moto. Kwa hiyo, ni wajibu wetu Watanzania kutekeleza sheria, ikiwemo na kujali matumizi ya barabara zetu hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mkakati wa Serikali hapa ni kuendelea kutoa elimu na kusimamia sheria. Pale ambapo tunaona kuna mtu anavunja sheria, hatua za kisheria zinachukuliwa hapohapo; huo ndio mkakati ambao tunao kwa sasa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, Mbunge wa Nkasi Kaskazini uulize swali.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2017 Serikali ilikuja na utaratibu wa upigaji chapa kama eneo la kutambua mifugo nchini. Zoezi hilo lilikuwa na changamoto zake ikiwepo chapa hizo kupotea au kufutika pamoja na ngozi kukosa ubora. Kupitia Bunge lako Tukufu, Bunge liliitaka Serikali kuja na namna bora ya utambuzi wa mifugo. Mwaka huu Serikali imekuja na utaratibu mpya wa kualisha hereni mifugo; zoezi ambalo limeanza tarehe 17 mwezi wa Nane mwaka huu kwenye baadhi ya miko.

Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi hilo ni zuri kwa sababu lina *barcode* ya nchi, mkoa, wilaya na jina la mfugaji. Hata hivyo, changamoto kwenye zoezi hilo ni pamoja na gharama ya shilingi 1,750 kwa kila ng'ombe. Lakini ng'ombe huyo akipoteza hereni mfugaji analazimika tena kulipia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa nia ya Serikali ni njema na itakwenda kuondoa wizi wa mifugo uliopo sasa hivi. Serikali haioni kuwa ni vyema iende ikafanye tathimini upya ione namna bora kwanza kupunguza gharama lakini kuona namna bora wataweka hiyo hereni na isiweze kuondoka kwenye mifugo? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu majibu kwa swali hilo.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aida Khenani, Mbunge wa Nkasi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Serikali imetafuta njia nzuri sana ya kufanya maboresho ya utambuzi wa mifugo yetu, ng'ombe wakiwemo. Na mfumo huu ulitokana na tatizo kubwa sana la wizi wa mifugo hapa nchini pamoja na kukosa takwimu sahihi za mifugo yetu hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumetafuta njia kadhaa za kuweza kutambua na kupata takwimu za ng'ombe hawa. Awali tulikuwa tunatumia njia ya kupiga chapa, lakini tumegundua kwa kupiga chapa tunapoteza ubora wa ngozi

ambapo ngozi zetu sasa nchini Tanzania haziuziki nje; na hata tulipoanza kutumia Kiwanda chetu cha Kilimanjaro Leather kwa kutengeneza viatu, ngozi zote zilizopigwa chapa hazitumiki vizuri kwa sababu zenyewe zimepoteza ubora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tumetafuta njia nzuri ya kuweza kutambua hawa ng'ombe, tukaamua kutumia njia ya kuvalisha hereni. Kwanza mwanzo tulikuwa tunatoboa lakini sasa hatutoboi bali tunaibandika. Inawezekana pia ng'ombe mmoja mmoja kutokana na kupita kwenye majani na miti hereni zinadondoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia kikao cha juzi cha mifugo ambacho mimi mwenyewe nilikuwa mgeni rasmi na mjadala uliofanyika kwenye kikao kile juzi pale Jijini Dar es salaam, kwenye eneo hili Wizara ya Kilimo wameondoa hizo tozo; endapo ulinunua kwa mara ya kwanza na sasa ng'ombe amepoteza herein. Tunachofanya ni kurudi tena kwenye mtandao na kujaza zile data zote kwenye hereni mpya tunampa mfugaji ili ng'ombe aendelee kuwa na ile alama aendelee kutambulika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo hatua nzuri ya kumuondolea gharama mfugaji ni hiyo ya kumrudishia tena ile hereni ili aweze kuivaa. Pili, hereni hii tumekuwa makini sana, hatutoboi tena bali tunatafuta namna ya kuigandisha vizuri pamoja na ile *spring* inabana vizuri kiasi kwamba hata akiwa na pilikapilika haiwezi ikadondoka kwa urahisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaendelea kutafuta njia nzuri zaidi ya hiyo. Niseme sasa kwamba tumepokea mawazo yako, na uzoefu ambao tumeuona kupitia wafugaji wetu kwamba hizi zinadondoka na kunakuwa na shida tena kurudi ofisini kupata hereni nyingine, kwa hiyo tunatafuta njia nzuri zaidi ya kutambua ng'ombe hawa kwa kuweka alama ambayo haitaharibu ubora wa masikio ya ng'ombe lakini pia haitasababisha gharama tena kwa mfugaji ili gharama ile ile aliyoitumia kwa mara ya

kwanza iendelee kutumika kama alama ya kumtambulisha ng'ombe huyo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Aleksia Asia Kamguna, Mbunge wa Viti Maalum, swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**MHE. ALEKSIA A. KAMGUNA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengi yana maeneo makubwa ya kiutawala nchini kwetu; kwa mfano, Mikoa ya Tabora, Tanga na Morogoro. Mkoa wa Morogoro una hususan wa *square meter* 73,000 ambazo ni kubwa sana. Sasa zile zinafanya kwamba ule mkoa ushindwe kutimiza adhima yake ya kuhudumia watu wake kikamilifu. Kwa mfano, kuna baadhi ya maeneo hayafikiki kabisa huduma za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa maeneo haya hayafikiki na huduma zinakuwa ni hafifu.

Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kugawa haya maeneo hatimaye huduma za jamii ziweze kufika kila eneo kwa urahisi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu majibu kwa swali hilo.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kantona, Mbunge kama ifuatavyo, samahani kama nimekosea jina.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aleksia Kamguna.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Kamguna, vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, upo ukweli kwamba tulikuwa na nia ya kugawa maeneo mapya ya utawala, hasa baada ya kugundua kwamba kuna maeneo makubwa sana kuliko huduma ambazo zinatolewa.



Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Morogoro, Tanga na Tabora ni miongoni mwa mikoa mikubwa sana ambayo pia tumepata taarifa kwa maandishi lakini pia kupitia vikao mbalimbali wakiomba kuyatenga tena maeneo hayo na kuongeza maeneo ya utawala kwa lengo la kurahisisha utoaji huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali tulisitisha kidogo kutoa maeneo mapya ya utawala na kutaka kuimarisha maeneo yale ambayo tumeikabidhi mamlaka hiyo, kwa maana ya vijiji, kata, wilaya hata halmashauri na mikoa mipya ili iwe na miundombinu ya kutosha na kuwapeleka watumishi wa kutosha kuweza kuhudumia maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nini mpango wa Serikali kwa sasa, tunasubiri sensa hii inayokuja mwakani ya mwaka 2022 iweze kutupa takwimu halisi ya idadi za idadi ya wakazi ili pia tuone idadi ya watumishi ambao tumewapeleka kuwahudumia na miundombinu tuliyoipeleka kuhudumia wananchi hao halafu tutafanya maamuzi kulingana na ukubwa huo na vigezo hivyo ambavyo tutavitumia kuweza kutoa maeneo haya mamlaka mpya. Hii ndiyo sababu kwa sasa hatujaruhusu tena kutoa mamlaka mpya kwenye maeneo mengine mapya kwa sababu hiyo. Kwa hiyo, baada ya sensa Serikali itafanya maamuzi ya kuona umuhimu wa kugawa maeneo hayo kulingana na vigezo vile ambavyo tumeamua kuvitumia, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mbunge wa Viti Maalum, swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kumekuwepo na uhaba wa rasilimali watu kwenye taasisi za idara mbalimbali za Serikali, mathalani kada ya walimu, watumishi wa afya na kwenye majeshi yetu; Jeshi la Polisi, Magereza na JWTZ kitu ambacho kinapunguza ufanisi katika kutoa

huduma kwa wananchi. Hata jana Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani alikiri kabisa kwamba kuna upungufu ambao unapelekea hata kufunga vituo vya polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imechukua hatua kwa kutangaza ajira 3,000 kwenye Jeshi la Polisi lakini kuna masharti ambayo yameambatana, kwanza wamesema ni ambao wamemaliza JKT na JKU lakini sharti namba tano na sita linaeleza kwamba ni wale vijana waliomaliza *form four* na *form six* kati ya mwaka 2017 na 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunatambua kwamba ajira zilisitishwa tangu mwaka 2015 na kuna vijana ambao wamemaliza *form four* na *form six* kati yam waka 2015/2016 na wameenda JKT na JKU na zaidi wamejenga Taifa letu kwa mfano Oparesheni Magufuli, Operesheni Makao Makuu na Operasheni Mererani.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu ni kwa nini sasa Serikali isifanye rejea kwenye tangazo lao la ajira ambalo lina-*limit* vijana hawa wa 2015/2016 ili liweze kuwa-*accommodate* na wao? Kwa nini wasiseme kwamba ajira inatolewa kwa vijana wote wenye sifa kuanzia waliomaliza *form four* na *six* 2015 mpaka 2020? Mfano lringa na Mbeya wamewakataa walivyoenda kwenye usaili. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Matiko sehemu ya kwanza ya swali lako linahusu sera, sasa hili lingine anaweza akajibu hata Waziri maana umeuliza mahsusi kuhusu ajira 3,000 zilizotangazwa na Jeshi la Polisi. Hata hivyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu nikupe fursa kwa ujumla kabisa kuelezea kuhusu uhaba wa watumishi.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Matiko, Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Serikali inaendelea na zoezi la kuajiri watumishi wa sekta mbalimbali hapa nchini ikiwemo na hayo matangazo aliyoyasema ya

Jeshi la Polisi. Sina uhakika na vigezo hivyo na wito walioutoa kwamba wanataka waajiri vijana kuanzia mwaka gani lakini tuichukue hiyo kama ushauri kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ambayo sasa inasimamia ajira hiyo ili waanze kufanya mapitio ya ajira hiyo na vigezo ili pia hawa waliomaliza jeshi kuanzia mwaka 2015 nao waingie halafu wachujwe wote tupate vigezo na tuweze kuwapata wale ambao wana sifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua pia tulikuwa na hilo kundi la Operesheni Magufuli na Operesheni Mererani na wote waliahidiwa kuingia kwenye orodha ya ajira na kama miongoni mwa hao walianza mwaka 2015 na kumaliza 2016 na hao walioanza kuchukuliwa 2017 mpaka sasa basi Wizara naona itatimiza wajibu wake kuwaita wote halafu iwachuje waweze kupata ajira pia. Kwa hiyo, tunaupokea ushauri wako na Waziri wa Mambo ya Ndani yuko hapa atalichukua hilo kwa ajili ya kulifanyia kazi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, Mbunge wa Mbulu Vijijini sasa uliza swali lako kwa Waziri Mkuu.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kunipa nafasi ya kuuliza swali kwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa pamekuwa na wizi wa ng'ombe uliokithiri katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Mfugaji mara nyingi anapopata tatizo lolote anatomia ng'ombe wake kumsaidia na hao ng'ombe wamekuwa wakitolewa mkoa mmoja hadi mwingine pamoja na kuwa na chapa hizi alizozijibu katika swali la mwanzo.

Je, Serikali ina kauli gani kuhusiana na wizi huu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu kwa swali hilo.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Flatei Massay, Mbunge wa Mbulu, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge anataka kujua hatua zinazochukuliwa na Serikali katika kudhibiti wizi wa mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Watanzania wote kwamba vyombo vyetu vya ulinzi nchini vimeendelea kufanya kazi kubwa sana na nzuri ya kudhibiti matukio ya uhalifu kote nchini ikiwemo la wizi wa mifugo na matukio mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye eneo la mifugo tunaendelea na udhibiti huo na tumetafuta njia rahisi ya kuweza kupunguza matukio haya. Moja, ni ile njia ambayo nimejibu muda mfupi uliopita ya kuweka alama mifugo hii ili iweze kutambulika ni ya nani, ya eneo gani ili pale inapopotea tunaweza kuipata. Pia, tumeendelea kushirikisha wananchi kwenye ulinzi shirikishi kwa matukio yote ikiwemo wizi wa mifugo na wa namna nyingine yoyote ya uhalifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatujaishia hapo, tumeendelea pia kushirikiana na wafugaji hawa kuhakikisha kwamba tunaweza kuimarisha ujenzi wa maeneo wanayoishi mifugo hii kwa mfano maboma yao, tumekuta maeneo mengine maboma yao wanazungusha tu miiba peke yake lakini ni rahisi ng'ombe hata kuruka na kuondoka na baadaye tunasema wameibiwa lakini kumbe boma lile siyo imara sana. Kwa hiyo, tumeendelea kutoa elimu ya uimarishaji wa maeneo hayo wanayohifadhiwa ng'ombe ili kuzuia wizi na wakati mwingine ng'ombe wenyewe kutoroka.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, tumedhibiti sana vibali vya usafirishaji holela kutoka eneo moja mpaka eneo lingine. Kama mwizi anaiba ng'ombe eneo A anawapeleka eneo B bila ya ukaguzi inakuwa ni rahisi sana sasa tulichofanya ni kudhibiti usafirishaji wa ng'ombe kutoka eneo moja mpaka lingine. Sasa ng'ombe hawezi kuhama kutoka kijiji kimoja mpaka kingine bila ya kibali maalum kinachotambulisha mwenye mifugo na kule anakokwenda. Hii ndiyo ambayo inasimamiwa sana kwa sasa ili kuweza kupunguza wizi wa mifugo kwenye maeneo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tutaendelea kutoa elimu kwa wafugaji lakini tunaendelea pia kufanya mikutano ya wafugaji kama nilivyosema ili haya mengine yote yanayojitokeza katika udhibiti wa wizi wa mifugo yaweze kupungua kwa kiasi kikubwa huku vyombo vya ulinzi vikiendelea na kazi yake ya ulinzi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile, Mbunge wa Mufindi Kusini, swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**MHE. DAVID M. KIHENZILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa fursa ulionipatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunafahamu kwamba kilimo ndiyo uti wa mgongo wa nchi yetu na kwa sasa kuna changamoto kubwa ya kupanda kwa bei ya pembejeo nchini na hii ipo kwenye pembejeo zinazohusu mazao mbalimbali ikiwemo mahindi. Suala hili limekuwa tatizo kubwa kwa nchi nzima lakini pia kwenye mikoa yetu ya Nyanda za Juu Kusini ikiwemo na Mufindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa mfano mbolea ya *DAP* kwa maeneo ya kule kwetu ni zaidi ya shilingi 100,000 wakati huo bei ya mahindi ni karibu shilingi 5000 yaani inakuhitaji ubebe karibu debe 20 za mahindi ili urudi na mfuko mmoja wa mbolea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu, ni upi mkakati wa Serikali wa muda mrefu na muda mfupi katika kutatua changamoto hii ambayo ni kero kubwa sana kwa wananchi wetu? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu kwa swali hilo.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kihenzile, Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba sasa hivi tunapata tatizo kubwa la upatikanaji wa mbolea; tatizo hili sio la Tanzania tu ni duniani kote kwa sababu uzalishaji umepungua sana. Jitihada za Serikali katika kuhakikisha tunapata mbolea ya kutosha zinaendelea na mwezi mmoja uliopita nilikuwa na Waziri wa Kilimo nchini Morocco ambako pia kuna kiwanda kinazalisha mbolea nyingi inayosambazwa karibu duniani kote na tumegundua kwamba mahitaji ni makubwa mno na kwa hiyo hata bei zake nazo zimepanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, bei ya mbolea sasa duniani kote iko juu lakini mpango wa muda mfupi ambao tumeutumia ili kupata mbolea angalau iweze kushusha bei ni kutoa ruhusa kwa wafanyabiashara kuingiza mbolea hapa nchini. Tunaamini kwa kuleta mbolea kwa wingi na kwa ushindani inaweza ikasaidia kidogo kupunguza bei badala ya bei hii ambayo ameitaja Mheshimiwa Mbunge inaweza kuwa bei ya chini ya kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama njia ya muda mfupi sisi wenyewe hapa nchini tumeazimia kutoa wito kwa wawekezaji kuja kuwekeza viwanda vya kutengeneza mbolea hapa. Mpaka leo hii tuna kiwanda kimoja tu kile cha pale Minjingu lakini bado tunazalisha kwa kiwango kidogo sana. Tumefanya jitihada za kupata wawekezaji kutoka nchi jirani ya Burundi na nimepata fursa ya kwenda kukutana na mwekezaji kulekule nchini Burundi tumezungumza na amekubali kuja hapa na tayari tumempa eneo hapa jijini Dodoma na ameanza hatua nzuri ya kuanza kuchimba msingi na ujenzi wa kiwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaamini uzalishaji mkubwa unaofanywa pale Burundi akija kuzalisha hapa tatizo la upatikanaji wa mbolea litakuwa limepungua sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niwasihi sana wakulima kwamba Serikali inaendelea kufanya jitihada za kila namna kuhakikisha upatikanaji wa mbolea unakuwepo kwa kiwango kikubwa ili kupunguza bei ambazo mkulima anaweza kumudu kuipata na kuendelea na kilimo chake

huku tukiwasiliana na nchi ambazo zinazalisha mbolea ili tuweze kupata mbolea kutoka maeneo yote. Kwa hiyo, tumetoa fursa kwa wafanyabiashara na pia Serikali kupitia Wizara ya Kilimo wanaendelea kuhakikisha kwamba tunapata mbolea ya kutosha kutoka nchi rafiki. Hizi zote ni jitihada za kuhakikisha kwamba tunapata mbolea na ikiwezekana tupate mbolea itakayoanza msimu huu wa kilimo. Huo ndiyo mpango wa muda mfupi na muda mrefu ambao tunautumia kwa sasa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu tunakushukuru sana kwa kujibu maswali ya Waheshimiwa Wabunge muda wako wa maswali umekwisha. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana, Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMB, ndc - KATIBU WA BUNGE:**

#### **MASWALI NA MAJIBU**

**NAIBU SPIKA:** Maswali ya kawaida, tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, Mbunge wa Singida Mashariki sasa aulize swali lake.

Na. 95

#### **Serikali Kujenga Shule ya Sekondari Mungaa**

**MHE. MIRAJI J. MTATURU** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga Shule ya Sekondari ya Kidato cha Tano na Sita Mungaa ambayo ni ahadi ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan aliyotoa kipindi cha Kampeni mwaka 2020 alipopita Jimbo la Singida Mashariki?

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina mpango wa ujenzi wa shule 26 za wasichana, moja katika kila Mkoa na ujenzi wa shule 1,000 za sekondari kwenye kata zisizo na shule za sekondari ili kupunguza msongamano wa wanafunzi madarasani na vikwazo hususani kwa watoto wa kike kutembea umbali mrefu. Vilevile, Serikali itafanya upanuzi wa shule za sekondari 100 kuweza kupokea wanafunzi zaidi wa kidato cha tano na sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa shule zote mpya za sekondari na upanuzi wa sekondari za kidato cha tano utafanyika kwa awamu. Awamu ya kwanza ya ujenzi itaanza mwaka wa fedha 2021/2022 ambapo Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 220. Kabla ya kuanza ujenzi, Serikali itafanya tathmini ya maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya za sekondari na mahitaji ya upanuzi wa sekondari za kidato cha tano na sita ikiwa ni pamoja na Shule ya Sekondari Mungaa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Miraji Mtaturu, swali la nyongeza.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwanza, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tarafa ya Mungaa ina shule zaidi ya nane za *O-level* na kwa sababu shule hii ya Mungaa ni kongwe ndiyo maana niliomba shule hii iweze kujengwa ili kuwapatia fursa wanafunzi wanaokosa nafasi ya kwenda kidato cha tano na sita kama ambavyo imekuwa ni tatizo kwenye maeneo mengine.

Kwa hiyo, naiomba Serikali katika tathmini hiyo iweze kuchukua umuhimu wa pekee kuhakikisha shule hiyo inajengwa.



Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, katika vikwazo ambavyo Mheshimiwa Naibu Waziri ameeleza ni pamoja na vikwazo vya watoto wa kike katika shule zetu za sekondari zikiwemo shule za kata. Ni nini mkakati wa Serikali kujenga hosteli za kuweza ku-*accommodate* wanafunzi wote wa kike katika shule zetu ambazo ziko katika Jimbo la Singida Mashariki? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa David Ernest Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali madogo ya nyongeza ya Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, Mbunge wa Singida Mashariki, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza alikuwa ameeleza tu kwamba Tarafa ya Mungaa ina shule nane za *O-level* na hivyo alikuwa anasisitiza tu kwamba tuiweke kwenye tathmini. Katika jibu la msingi tumekubali kwamba kwenye tathmini ya zile shule 100 ambazo tunakwenda kuzifanyia upanuzi nchi nzima kwa ajili ya kupokea watoto wa kidato cha tano miongoni mwa shule tutakayoifanyia tathmini ni Shule ya Mungaa. Kwa hiyo, hilo tumelikubali litafanyika katika mwaka huu wa fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili kuhusu vikwazo kwa watoto wa shule ambao wanatembea umbali mrefu kuelekea shuleni, moja ya mkakati wa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Rais mama yetu Samia Suluhu Hassan ni pamoja na kujenga hosteli. Ndiyo maana katika mwaka huu wa fedha tumetenga fedha nyingi tu kuhakikisha kwamba tunajenga hosteli katika maeneo mbalimbali na ninyi mmepitisha bajeti hiyo. Kwa hiyo, tunachosubiri tu ni fedha zitakapotoka tutaainisha maeneo mbalimbali na tutazingatia Jimbo la Singida Mashariki. Ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Grace Tendega, swali la nyongeza.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini ukiangalia majibu yake yanasema kwamba bado wanafanya tathmini ina maana hawajaanza na robo tayari ya mwaka tumeshapita.

Sasa swali langu ni lini watakwenda kujenga shule hizo ili watoto wa kike wasiweze kupata adha hizo kwa sababu tumeona adha wanazozipata watoto wa kike hasa Mkoa wa Iringa wanapata changamotoo kubwa sana. Kwa hiyo, tunaomba majibu ni lini wanaanza, tumeshapitisha robo sasa? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa David Ernest Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Grace Tendega, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge anasema kwamba robo ya kwanza ya mwaka imepita na bado inaonesha kama hatujafanya tathmini, kwa hiyo anachotaka kujua *exactly* ni lini? Ni kwamba Serikali ina mipango na mikakati yake na mimi nimwambie tu kwamba kabisa Serikali ya Awamu ya Sita hatutashindwa kukamilisha haya majengo kwa wakati. Moja ambacho hafahamu tunapojenga kwa mfano darasa ni muda wa miezi mitatu darasa linakuwa limekamiliika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunachokisubiri sasa hivi tu baada ya robo ya kwanza na mifumo ya fedha kufunguka kinachofuatia baada ya hapo ni fedha kuanza kuzitenga na kuzipeleka katika maeneo husika yaliyopangwa katika bajeti. Kwa hiyo, ninyi ondoeni wasiwasi Serikali ya Mama Samia Suluhu Hassan hii kazi tunaiweza na tutaimaliza kwa wakati. Ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri kwenye hilo zoezi mtusaidie maana shule moja inapokuwa inachukua eneo kubwa wale watoto wa kike wanapata changamoto kubwa sana kwenda shule na kurudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, swali la nyongeza.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na mimi nilitaka niulize swali. Serikali ilikuwa na programu ya kukarabati shule kongwe nchi nzima ikiwepo Shule ya Sekondari *Iringa Girls* na *Lugalo Secondary* zilizopo Iringa ambazo ni za bweni kwa watoto wa kike na hasa watoto wenye ulemavu wa ngozi, viungo na wasioona. Pale hapakufanyika ukarabati wa mabweni mawili; moja katika shule ya *Iringa Girls* na nyingine *Lugalo Secondary*.

Je, ni lini sasa Serikali itatukamilishia mabweni yale ili watoto wale wenye ulemavu wasiendelee kupata shida ya mahali pa kulala? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa David Ernest Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, Mbunge wa Iringa Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri anazungumza kitu ambacho anakifahamu kwamba hizi shule alizozitaja ziko katika mipango yetu. Kwa hiyo, aondoe wasiwasi tu kwamba tutatekeleza ahadi ya kuwasaidia wanafunzi wote sio *Iringa Girls* na Lugalo ni shule zote kongwe tulizozikusudia zitafikiwa. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kiruswa, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali ilishaahidi kujenga shule bora ya mfano ya wasichana katika kila mkoa nchini; na kwa kuwa shule hiyo ya mfano katika Mkoa wa Arusha tulikubaliana kwamba itajengwa katika Jimbo la Longido; na kwa kuwa tulishatenga eneo la kujengwa shule hiyo katika Kata ya Angekahang, ni lini ujenzi wa shule hiyo ya mfano kwa ajili ya wasichana wetu itaanza kujengwa?

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Mheshimiwa David Ernest Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Kiruswa, Mbunge wa Longido, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli mpaka sasa hivi tumeshaainisha maeneo yote 26 ambayo shule hizi zitajengwa baada ya kupata mapendekezo kutoka katika kila mkoa. Kwa hiyo, kinachosubiriwa sasa hivi tu ni fedha itoke na baada ya hapo tutapeleka fedha kwa awamu ya kwanza katika mikoa 10 ambayo tumeainisha mwaka huu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge atupe muda eneo lake halitabadilishwa na kazi hiyo itafanyika kama ambavyo imekusudiwa. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo, Mbunge wa Arumeru Mashariki, sasa aulizwe swali lake.

Na. 96

**Kujenga Barabara Zinazopanda Milimani  
Arumeru Mashariki**

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami barabara zinazopanda milimani Arumeru Mashariki ili kuwafikishia Wananchi huduma pamoja na kupunguza gharama za matengenezo ya mara kwa mara kwa barabara hizo ambapo gharama zake ni kubwa kutokana na ugomu wa kijiografia?

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Mheshimiwa David Ernest Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo, Mbunge wa Jimbo la Arumeru Mashariki, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Serikali imeidhinisha jumla ya shilingi bilioni 1.93 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa barabara za milimani zenye jumla ya urefu wa kilomita 82.1 pamoja na barabara za ukanda wa chini zenye jumla ya urefu wa kilomita 22.3 kwa kiwango cha changarawe, kujenga daraja moja, makalavati 63 pamoja na kuchimba mifereji ya kuondoa maji barabarani yenye urefu wa kilomita nane.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, barabara zenye urefu wa kilomita sita za ukanda wa milimani zitafanyiwa usanifu kwa ajili ya ujenzi wa kiwango cha lami. Barabara hizo ni Leganga – Mulala kilomita mbili; *Police* – Magarisho kilomita mbili; Sangisi – Ndoombo kilomita mbili kwa gharama ya shilingi milioni tano kwa ajili ya usanifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Serikali ilifanya matengenezo ya barabara za Maji ya Chai – Sakila kilomita tatu; *Police* – Ngurdoto kilomita 3.5; Mji Mwema – *Dispensary* kilomita 0.5; Leganga – Ngarasero kilomita 0.8; Kisimiri Sekondari kilomita nne; Ngarenanyuki – Ngabobo kilomita 2.5; Ubungo – Irrikolanumbe kilomita 2.6;

Sangisi – Ndoombo kilomita tano; Tengeru – Nambala kilomita mbili; Poli – Seela kilomita mbili pamoja na ujenzi wa barabara ya Sangis – Nambala kilomita 1.9 kwa kiwango cha lami kwa jumla ya gharama ya shilingi bilioni 1.38.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kwa barabara zinazopanda milimani Arumeru Mashariki kadri ya fedha zinavyopatikana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Pallangyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali lakini sija ridhika nayo. Hata hivyo, naomba kwanza kibali chako nitoe shukrani na pongezi zangu kwa Serikali ya Awamu ya Sita ambayo inafanya kazi vizuri sana, hususan kwenye barabara. Tunashuhudia barabara za lami zinajengwa kila mahali, lakini hiyo neema ya barabara za lami bado haijafika Arumeru Mashariki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata jibu la Serikali halijasema bayana kwamba tutapata lini hizo barabara za lami, badala yake Mheshimiwa Waziri ametoa *statistics* za ukarabati na ujenzi wa barabara za kule jimboni kwa kiwango cha udongo na changarawe.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali, narudia tena; je, ni lini Serikali itakuja kujenga barabara za lami zinazokwenda milimani ili kuweza kupambana na hali ngumu ya *terrain* ambayo siyo rafiki kwa maana ya kwamba kila msimu wa mvua zile barabara zinachimbika zinakuwa mito?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Pallangyo, hilo si ndiyo lilikuwa swali lako la msingi?

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, hakunijibu.

**NAIBU SPIKA:** Sasa kama halijajibiwa Kanuni zetu zina utaratibu wake, wewe eleza kwamba swali halijajibiwa, lakini usirejee tena swali lako la msingi kwa sababu majibu ameshayatoa, kwa hiyo maana yake ukimuuliza atajibu hivyo hivyo ambavyo ameshajibu.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu hajajibu.

**NAIBU SPIKA:** Sawa. Kama swali lako halijajibiwa basi wewe kaa, ufuatae utaratibu wa Kikanuni ili swali lako lipate kujibiwa.

Swali la Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mbunge wa Babati Vijijini, litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray.

Na. 97

### **Mgogoro Kati ya Kiwanda cha Minjigu na Vijiji**

**MHE. REGINA N. QWARAY K.n.y. MHE. DANIEL B. SILLO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itamaliza mgogoro wa mpaka kati ya Kiwanda cha Mbolea cha Minjingu na Vijiji vya Olacity na Minjingu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu kwa swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mbunge wa Jimbo la Babati Vijijini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, mgogoro kati ya Kiwanda cha Mbolea cha Minjingu na Vijiji vya Olacity na Minjingu ulitokana na vijiji kutokutambua mipaka halisi kati ya vijiji hivyo na kiwanda, hivyo kusababisha wananchi kutoka katika vijiji hivyo kuingia na kufanya maendeleo katika eneo la kiwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwezi Januari, 2021 Serikali ilifanya uhakiki wa mpaka wa Kiwanda cha Minjingu na vijiji vinavyozunguka kiwanda hicho na kubaini kuwa kuna jumla ya kaya 83 ndani ya eneo la kiwanda ambapo kaya kutoka Vijiji vya Olacity na Minjingu ni miongoni mwa vijiji hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, miongoni mwa kaya hizo, kaya 40 za wahanga wa mafuriko ambazo ziliombewa na Kijiji cha Minjingu makazi ya muda ndani ya eneo la kiwanda, lakini baada ya muda wa makubaliano kuisha, kaya hizo zimegoma kuondoka katika eneo la kiwanda, hivyo kusababisha kuwepo kwa mgogoro huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaelekeza Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Manyara kukutana na pande zote mbili zinazohusika ili kuutafutia ufumbuzi mgogoro huo ifikapo Desemba, 2021.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray, swali la nyongeza.

**MHE. REGINA N. QWARAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Je, Serikali imejipangaje kutatua mgogoro unaofanana na huo katika Vijiji vya Magara na mashamba ya wawekezaji kule Kiru?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Serikali itakuja lini kutatua mgogoro katika vijiji vya Kata ya Kaiti ambavyo ni Vijiji vya Minjingu, Vilima Vitatu na Kakoi kati ya wafugaji na Jihubi? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.



**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu swali lake la kwanza na la pili ameanisha baadhi ya maeneo akisema Vijiji vya Magara na mashamba ya wawekezaji na hilo eneo lingine katika Mkoa wa Manyara. Katika maagizo ambayo sisi Serikali tumeyatoa ni kwamba tutaagiza Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na haya maeneo aliyoyataja, basi waende kutafutia ufumbuzi na watatuletea taarifa Ofisi ya Rais, TAMISEMI ili tujue hatua zaidi za kuchukua. Hata hivyo, tunaamini kwamba yapo ndani ya ofisi ya mkoa na wanaweza kuyamaliza na hii migogoro isiendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Lukuvi.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Silinde, Naibu Waziri TAMISEMI, na kwa niaba ya Waziri, nataka niongeze kidogo majibu kwa Mheshimiwa Mbunge kwa kumpa taarifa kwamba viongozi wa Chama Cha Mapinduzi wa Mkoa wa Manyara wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM wa Mkoa na Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Mkoa walikuja kuniona juzi kueleza hayo matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimewaahidi kwamba mwezi Oktoba tutakwenda kuitisha mkutano wa Viongozi wote wa Mkoa watuambie kwa pamoja matatizo yote yanayowasibu juu ya migogoro yao yote, halafu tupange ratiba ya kutekeleza kwa pamoja, pamoja na haya aliyoyasema. Hii ni nyongeza ya haya. Maagizo ya kwa Mkuu wa Mkoa tutayapeleka, lakini na mimi mwenyewe nitakwenda mwezi Oktoba. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Lukuvi, ni miezi sita sasa unasubiriwa Mbeya, sasa hizi ahadi zako za kwamba unakwenda mahali halafu kwenda huendi, naamini huko kwa Mheshimiwa Regina Qwaray utatimiza hiyo ahadi yako ya kwenda mwezi Oktoba. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango; Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, Mbunge wa Manyoni Mashariki, sasa aulize swali lake.

Na. 98

**Serikali Kuhuisha Vigezo vya Mfumo wa  
Miradi ya Kimkakati Nchini**

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhuisha vigezo vya mfumo wa miradi ya kimkakati kupitia maandiko ya miradi ili iweze kusaidia Halmashauri kubuni miradi ya kiuchumi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Mhandisi Masauni, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, Mbunge wa Manyoni Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imejikita katika kutoa huduma bora na zenye uhakika kwa wananchi wake ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kwamba Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaendelea kujiongezea mapato kwa kutumia fursa zilizopo katika maeneo yao ili kutoa huduma bora kwa lengo la kupunguza utegemezi wa ruzuku kutoka Serikali Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufikia lengo hili, Serikali iliandaa mkakati maalum wa kuwezesha halmashauri

kujitegemea kimapato. Katika kutekeleza mkakati huo, Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatakiwa kuhakikisha zinatumia kwa ukamilifu fursa za kimapato zilizopo katika maeneo yao na kuongeza uwezo wa kujitegemea kimapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za kugharamia miradi ya kimkakati hutolewa kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa na Wizara ya Fedha Mipango. Hivyo, hoja ya Mheshimiwa Mbunge kuhusu uboreshaji wa vigezo vilivyowekwa kwenye uchambuzi wa miradi ya kimkakati imechukuliwa na kwa sasa Serikali inaangalia njia bora itakayosaidia kuboresha utaratibu wa maombi na vigezo vya uandaaji wa miradi ya kimkakati kabla ya utoaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, ninayo maswali mawili ya nyongeza. Swali langu la kwanza; ni lini sasa Serikali itatoa huo mwongozo mpya ili tuweze kusaidia zile halmashauri ambazo zina uhitaji mkubwa wa kuwekeza kwenye miradi ya kimkakati?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; katika Jimbo la Manyoni Mashariki hatuna stendi ya mabasi. Sasa nini *commitment* ya Serikali kuhakikisha kwamba kwa kupitia huu mfumo itakuwa tayari kusaidia Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni kujenga stendi ya mabasi ili itumike kama kitega uchumi kwa halmashauri?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Mhandisi Masauni, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, Mbunge wa Manyoni Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na mwongozo mpya ilitokana na mapendeezo ambayo Mheshimiwa Mbunge amewasilisha. Kwa hiyo pale ambapo utakuwa umekamilika kwa kuzingatia haya mapendeezo ambayo ametupatia tutampatia. Hata hivyo, kwa huu mwongozo ambao tunaendelea nao na tunadhani mpaka sasa hivi haujaleta changamoto kubwa, ninao hapa na nitampatia baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la pili; niwapongeze kwanza yeye Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wake wa jimboni kwake kwa jitihada ambazo wameanzisha, lakini nimhakikishie kwamba kama ambavyo tumekuwa tukifanya siku zote kuhakikisha tunasaidia ujenzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo katika halmashauri zetu mbalimbali ikiwemo miradi ya stendi za mabasi, basi na jimbo lake na lenyewe tumelichukua tutaangalia tuingize katika mpango wetu wa utekelezaji pale tutakapofanya upembuzi wa kina kubaini kwamba ni utaratibu gani muafaka wa kuweza kuendelea na mradi huo na bajeti itakapokuwa imeruhusu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, pamoja na hayo, nadhani ni vizuri kuangalia uwiano. Kuna mikoa kadhaa haina stendi ya kisasa, haina soko la kisasa. Yaani wao hawana kabisa eneo la kuweka hii miradi ya kimkakati, inaleta kidogo changamoto tukifikiri kwamba wale wa eneo waliopelekwa kule wanaoandika hii miradi ni watu wa Serikali.

Sasa inakuwaje maeneo mengine wanapelekwa wenye kujua sana kuandika, kwa hiyo mikoa hiyohiyo kila siku halafu mikoa mingine haina stendi wala soko la kisasa. Nadhani Serikali iangalie namna ya kuoanisha haya mambo ili wengine wasijikute wako katika hali ngumu, wengine hali zao ni nzuri kila wakati kwa sababu huko wako watu wazuri wa kuandika hiyo miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda, swali la nyongeza.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kuniona. Kwa kuwa suala la kujenga uwezo wa halmashauri na hasa katika miradi hii ya kimkakati linakwenda sambamba na suala la kuinua hali za wananchi kiuchumi ili waweze kushiriki vizuri katika miradi hii, nini hatua ya Serikali mpaka sasa katika kilio kikubwa cha wananchi cha kupunguza riba za mabenki?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Mhandisi Masauni, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza ya Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka hapa wakati wa mjadala wa bajeti, Mheshimiwa Kilumbe alikuwa miongoni mwa Waheshimiwa Wabunge ambao walilizungumzia sana tatizo hili la ukubwa wa riba katika mabenki yetu ya biashara. Muda mfupi Mheshimiwa Rais wetu Samia Suluhu Hassan alitoa maelekezo kwa Serikali kuangalia jinsi gani ambavyo tutapunguza riba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi, kama ambavyo nilikuwa nimeeleza jana wakati najibu swali, naomba nirudie kuwahakikishia kwamba yale maeneo matano ambayo Benki Kuu ya Tanzania iliyaainisha kuwa kama ni njia ya kuweza kufikia malengo hayo tayari yameshaanza kufanyiwa kazi. Kwa hiyo, nimthibitishie Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda kwamba, wakati wowote kuanzia sasa mabenki kadhaa tayari yameshaanza kupeleka maombi yao kwenye Benki ya Tanzania kwa ajili ya kutumia fursa hizo zilizotolewa zenye dhamira ya kufikia malengo haya ya kuhakikisha kwamba riba inakuwa nafuu kwa kiwango kisichoziidi asilimia kumi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nyamoga, swali la nyongeza.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa moja kati ya vigezo vilivyopo katika mwongozo ni

halmashauri iwe na hati safi kwa miaka mitatu mfululizo; na kwa kuwa kigezo hiki ni kandamizi kwa wananchi kwa sababu wanaosababisha hati kuwa chafu au safi siyo wananchi bali ni watumishi wa halmashauri.

Je, Serikali haioni kwamba hata kama kuna marekebisho yanafanywa kigezo hiki kiondolewe mara moja ili halmashauri zote zipate haki ya kuomba miradi hii ya kimkakati? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Mhandisi Masauni, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza ya Mheshimiwa Justin Nyamoga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inapoandaa miradi hii ya kimkakati moja katika dhamira zake kubwa ni kuhakikisha kwamba miradi hii inakuwa na tija kwa ujumla wake. Ndiyo maana miongoni mwa vigezo, ukiachilia mbali hicho ambacho Mheshimiwa Mbunge amekizungumza, ni kuangalia mtiririko mzima wa fedha katika mradi ili kuona kwamba mradi ule utaweza kujiendesha kwa faida na baadaye uweze kuwa na tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hati chafu inapokuja inatoa kiashiria hasi juu ya ufanisi wa mradi husika. Hata hivyo kwa kuwa jambo hili ni la kitaalam, naomba nilichukue halafu tukaiwasilishe hoja yake kwa wataalam, tuone jinsi gani inaweza ikafanyika bila kuathiri lengo halisi la kuona tija inapatikana katika mradi ule, lakini wakati huohuo isiathiri dhamira njema ya wananchi kwa makosa ambayo hayawahusu.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Antipas Zeno Mgungusi, Mbunge wa Malinyi, sasa aulize swali lake.

Na. 99

**Barabara ya Lupiro – Malinyi – Kilosa Kwa Mpepo – Namtumbo Lumecha Km 296**

**MHE. ANTIPAS Z. MGUNGUSI** aliuliza:-

Je, Serikali haioni haja ya kutenga fedha za kuvunja Mlima Londo ili kuunganisha Wilaya ya Malinyi na Namtumbo hata kwa kiwango cha changarawe ili njia hii iweze kupitika huku Serikali ikiendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa kiwango cha lami wa Barabara ya Lupiro – Malinyi – Kilosa – Kwa Mpepo – Namtumbo Lumecha ya kilomita 296?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa *Engineer* Godfrey Kasekenya Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Antipas Zeno Mgungusi, Mbunge wa Malinyi, kama ifuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) ilikamilisha kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Barabara ya Ifakara – Lupiro – Malinyi – Kilosa Kwa Mpepo – Londo – Lumecha mwaka 2018. Katika usanifu huo, barabara itakayojengwa imeukwepa Mlima Londo kutokana na gharama kubwa ya kuuvunja mlima itakapopita barabara hiyo. Hivyo, Serikali itajenga barabara kwa kiwango cha lami kupita katika maeneo yaliyoainishwa katika upembuzi yakinifu na usanifu wa kina.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, namsihi Mheshimiwa Mbunge awe na subira wakati Serikali ikiendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami. Aidha, Serikali

itaendelea kuifanyia matengenezo barabara hii na kuendelea kuifungua kulingana na upatikanaji wa fedha. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Antipas Zeno Mgungusi, swali la nyongeza.

**MHE. ANTIPAS Z. MGUNGUSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Nilijitahidi kuwa *specific* kidogo; watu wa Malinyi na Namtumbo na Ruvuma yote tunahitaji kuona Mkoa wa Morogoro na Ruvuma unaunganishwa kwa maana ya kufunguliwa. Suala la lami tutavumilia kusubiria, tunajua gharama ni kubwa, kilometa ni nyingi, lakini kuunganisha tu hata kwa kiwango cha vumbi; je, Serikali iko tayari?

Mheshimiwa Naibu Spika, kama inaridhia, iko tayari kuweka fedha kidogo kwa ajili ya barabara hiyo katika bajeti inayofuata? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mhandisi Godfrey Kasekenya Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Antipas Mgungusi Mbunge wa Malinyi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyosema, eneo analoliongelea lina milima mingi na linapita kwenye safu ya Mbuga ya Selous, ina urefu wa takribani kilometa zisizopungua kama kilometa 100. Ndiyo maana katika jibu letu la msingi tumesema tumeona tumefanya tathmini, kuvunja ule mlima ni gharama sana.

Kwa hiyo, kuna haja ya kutafuta fedha kubwa ili katika huo mradi tuweze kupindisha barabara kuzunguka hiyo milima ili tuweze kuwa na uhakika wa kuipitisha hiyo barabara.



Mheshimiwa Naibu Spika, ombi lake limechukuliwa, lakini ni wazi kwamba fedha inayohitajika ni eneo la zaidi ya kilometa 100. Kwa hiyo, ni bora tukaamua kabisa kuujenga huo mradi. Hata hivyo, bado tumeendelea kutoa fedha kidogo ili kufungua kulingana na fedha inavyopatikana kuunganisha Mkoa wa Ruvuma na Morogoro kati ya Wilaya hizo mbili za Malinyi na Namtumbo. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Kutokea Msekwa Mheshimiwa Vita Kawawa, swali la nyongeza.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali iligharamia barabara hii fedha nyingi sana; imejenga madaraja ya Mto Kilombero kwa gharama kubwa, imejenga Mto Furuu, Mto Mwatisi, Mto Londo na Mto Luhila kwa upande wa Mkoa wa Ruvuma Jimbo la Namtumbo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haioni sasa ipo haja kukifungua hiki kipande ili tuweze kupita angalau barabara iwe inapitika na gharama zilizoingia kwa Serikali kujenga haya madaraja, basi zionekane zina faida?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mhandisi Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Vita Kawawa, Mbunge wa Namtumbo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana nimpongeze Mheshimiwa Vita Kawawa kwa kutambua juhudi kubwa ambazo zinaendelea na Serikali hii ya Awamu ya Tano na ya Sita ambapo tumeshajenga madaraja haya aliyoyataja, dhamira njema ya Serikali ikiwa ni kuiunganisha iwe mkoa. Katika kitu kigumu kwenye barabara ni madaraja. Kwa hiyo,

anaeleza pia kwamba Serikali ina dhamira kabisa na ndiyo maana tumeendelea kujenga hizo barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tayari mwaka huu tumetenga shilingi bilioni mbili na nusu kwa ajili ya kuendelea kujenga hiyo barabara. Kwa hiyo, kadri fedha zitakazopatikana naomba nimhakikishie Mheshimiwa Kawawa na Mheshimiwa wa Malinyi kwamba Serikali ina nia ya dhati. Kwa hiyo, tutaikamilisha hiyo barabara; na kama walivyosema, inawezekana tukaanzia eneo hilo ambalo sasa limekuwa ni kikwazo zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Felista Njau, swali la nyongeza.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ni lini Serikali itajenga barabara inayoanzia Bunju A kupitia Mabwepande ikiunganisha na Jimbo la Kibamba ambayo barabara hiyo imekaa muda mrefu na ikitolewa ahadi bila utekelezaji? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mhandisi Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Felista Njau, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba yalikuwa pia ni ahadi ya Mheshimiwa Hayati Rais na pia yalikuwa ni maagizo. Kwa hiyo, nimhakikishie kwamba hizo barabara, *TANROADS* kwa maana ya Mkoa wa Dar es Salaam kusaidiana na Ofisi ya Rais, *TAMISEMI (TARURA)* tutahakikisha kwamba hizi barabara zinatekelezwa kuanzia kipindi hiki cha mwaka wakati wa utekelezaji wa bajeti ya kuanzia mwaka huu 2021. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Michael Kembaki, swali la nyongeza.

**MHE. MICHAEL M. KEMBAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nachukua nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kutupa zaidi ya kilometa 80 ya barabara ya lami kutoka Tarime Mjini, kuelekea Serengeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu ni kwamba kwa sababu tayari wananchi wakazi wale wa Tarime waliopo pembezoni mwa barabara wameshabomoa nyumba zao kwa ajili ya kulima barabara ile, lakini kuna kipande ambacho kulikuwepo na Mkandarasi ambaye alikuwa anajenga kipande pale *Lebu Center* kwenda Mugabiri na tayari yule Mkandarasi anaendelea...

**NAIBU SPIKA:** Uliza swali Mheshimiwa Kembaki.

**MHE. MICHAEL M. KEMBAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo najenga hoja ya swali langu.

**NAIBU SPIKA:** Huna haja ya kujenga hoja, wewe taja barabara unayotaka kuulizia swali.

**MHE. MICHAEL M. KEMBAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mkandarasi yule anaendelea na ujenzi wa kile kipande na tayari wananchi wamebomoa kwamba ile barabara inajengwa upya kutoka hapo mjini kuelekea...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kembaki uliza swali.

**MHE. MICHAEL M. KEMBAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu ni hivi ni kwa nini Mkandarasi yule asingepewa sehemu nyingine ajenge badala ya kujenga sehemu ambayo tayari *TANROADS* watakuja kujenga?

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mhandisi Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Michael Kembaki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mkandarasi yupo *site* na anajenga, namwomba Mheshimiwa Mbunge baada ya hapa nikutane naye kupata maelezo sahihi kwa ajili ya kutatua hiyo changamoto anayosema ili kwa pamoja na Meneja wa *TANROADS* Mkoa tuone namna ya kuondoa hiyo changamoto. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Kutokea Msekwa Mheshimiwa Boniphace Butondo, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo na ahadi za viongozi wetu Wakuu wa Serikali na ahadi hizi zimekuwa zikitolewa tangu Awamu ya Nne, Awamu ya Tano na sasa Awamu ya Sita na ahadi hizo zimekuwa hazipo katika mkakati mzuri wa kuziratibu na pengine kuweka bajeti kwa ajili ya kuzitekeleza: Nini mpango mkakati wa Serikali wa kuhakikisha kwamba sasa ahadi zile zote zinaratibiwa nchi nzima na kuwekewa mkakati wa kibajeti ili mradi ahadi hizi ziwe ni ahadi zinazotekelezeka? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mhandisi Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Boniphace Butondo, Mbunge wa Kishapu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Boniphace Butondo kwamba ahadi zote zinazotolewa na viongozi wa kitaifa zimeratibiwa na kwa kweli

tunazifahamu na ndiyo maana tunakuwa tunazitambua kwamba zinatakiwa zitekelezwe. Zikishatolewa ahadi zinakuwa ni kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mbunge kwamba kinachogomba hapa wakati fulani huwa ni bajeti kwamba unapanga, lakini hutegemea na bajeti ya Serikali. Kwa hiyo, ahadi zote ambazo zimetolewa zikiwepo na ahadi ambazo zimetolewa katika Jimbo lake, tunazifahamu na tumeziratibu na nyingine tumezipangia bajeti.

Kwa hiyo, ndiyo maana tunasema kulingana na upatikanaji wa fedha zikipatikana, miradi yote ambayo Waheshimiwa Viongozi wetu wa Kitaifa wamezitoa tutaitekeleza. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 100

### **Usalama wa Askari Wawapo Kazini**

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS** aliuliza:-

Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusu usalama wa Askari ambao wakati mwingine huvamiwa na kujeruhiwa pamoja na kuporwa silaha wakati wakiwa kazini?

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, Mbunge Viti Maalum kutoka Zanzibar, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Askari wa Jeshi la Polisi wapo imara katika kutimiza majukumu ya kazi zao za kila siku na wamepata mafunzo mbalimbali yakiwemo mafunzo ya mbinu za medani, matumizi ya silaha na mafunzo ya kujihami. Pia katika utendaji wa kazi wao hufuata utaratibu wa kujilinda na kulinda wengine, ila mazingira na maeneo ya utendaji kazi husababisha changamoto mbalimbali kutokea kama hizo za kuvamiwa na kujeruhiwa. Mara zote Jeshi la Polisi hudhibiti hali hiyo na kushughulikia kwa haraka matukio ya namna hiyo na kuimarisha amani na utulivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, swali la nyongeza.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza sina budi kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri na yanaleta faida kwa Watanzania. Hata hivyo nina maswali mawili madogo ya nyongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa uvamizi katika vituo vya Polisi siyo jambo jema, lakini nashukuru Jeshi la Polisi wameweza kudhibiti, lakini suala kama hilo huenda likajirudia. Swali langu linasema hivi: Je, ikitokea wamevamiwa katika vituo vyao na kwa bahati mbaya askari kajeruhiwa au askari kauliwa; familia ile inayomtegemea yule askari ambapo ndio tegemeo lao kimaisha, Serikali inawaambia nini au itawasaidia nini ili waweze kuishi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa wanapovamia vituo, lengo kuu ni kupata zile silaha na kuwaathiri Polisi wenyewe walioko kituoni. Je, wakati wanapozungumza au wakati taarifa tunapozipata, baadhi yao wanazipata silaha; wanapokuwa wamezipata zinakuwa katika hali gani? Katika hali ya ubora ule ule wa awali au tayari zimebadilishwa ili wasiweze kuzitambua? Ni hayo tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Bi. Fakharia, Mbunge wa Viti Maalum, kutoka Mkoa Mjini Zanzibar, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi imeweka utaratibu maalumu wa askari wake watakapopata mitihani katika harakati za kulinda amani na utulivu wa nchi hii, lakini ni ikiwa imethibitika kwamba mitihani huo umemkuta ama ameupata akiwa katika harakati za kazi zake za kawaida za kiaskari. Kwa hiyo, kuna kanuni ya fidia ya pamoja ya Jeshi la Polisi na Magereza, hiyo hutumika. Katika kanuni hiyo imeelezwa viwango ambavyo huwa mtu anafidiwa kutokana na tatizo lililomkuta; kuna viwango akipata ulemavu, kuna viwango akikatika, na kuna viwango akifa. Kwa hiyo, Serikali kupitia Jeshi, imeweka utaratibu maalumu kupitia hii kanuni ambayo inawapa watu nafasi ya kuweza kupata fidia zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lingine kwamba je, Silaha hizi tunakuwa tumezipata zikiwa zimeharibika au vipi? Silaha hizi zitakavyokuwa, zikiwa zimeharibika, zikiwa nzima, wajibu wetu tukizipata katika matukio ya kihalifu, maana yake ni kuzichukua. Kama itakuwa zimeharibika, maana yake tuna utaratibu wa kuzitengeneza. Ikiwa hazijaharibika, tunaingalia; kama silaha ile ina kesi, tunaiacha kesi ile iendelee, ikimalizika, silaha ile inarudi Serikalini, inarudi jeshini, tunaendelea kuitumia kwa ajili ya Ulinzi na Usalama wa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Emmanuel Adamson Mwakasaka, Mbunge wa Tabora Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 101

**Tatizo la wizi wa kimitandao**

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya ziada ya kudhibiti tatizo la utapeli na wizi wa kimitandao kupitia simu za mkononi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Kundo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel Adamson Mwakasaka, Mbunge wa Tabora Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali tayari imechukua hatua za kuweka mazingira salama kwa wananchi hususan kwenye mitandao kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2015 Serikali ilitunga Sheria ya Makosa ya Mitandao kwa lengo la kutambua kisheria makosa yanayofanyika kwenye mitandao ili kuweza kuchukua hatua stahiki yanapobainika makosa hayo; na vile vile, Sheria ya Miamala ya Kielektroniki kwa lengo la kutambua miamala inayofanyika kimitandao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilianzisha Kitengo cha Uhalifu wa Mitandao chini ya Jeshi la Polisi kwa ajili ya kufanya uchunguzi wa makosa ya kimitandao ikiwemo wizi wa aina yoyote kwenye mtandao na kuandaa majalada ya kufungulia mashtaka kwa kusaidiana na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka. Watuhumiwa wanaokamatwa kutokana na matumizi mabaya ya mitandao huchukuliwa hatua stahiki.



Mheshimiwa Naibu Spika, Februari, 2021 Serikali imeunda Kamati ya Taifa ya Kusimamia Utatuzi wa Matumizi Mabaya ya Huduma na Bidhaa za Mawasiliano ambayo inahusisha Wizara na taasisi zote zinazohusika katika kushughulikia makosa ya mtandao. Kamati hiyo ni Kamati ya kudumu na inaishauri Serikali namna ya kutatua changamoto za mitandao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kushirikiana na Watoa Huduma wa Simu za Mkononi imeanzisha mfumo kupitia namba 15040 wa kupokea na kuzifungia namba ambazo zimeripotiwa na kuthibitika kutuma ujumbe au kupiga simu za utapeli. Baada ya kuthibitisha namba hizo kufanya vitendo hivyo, namba husika hufungwa na kitambulisho cha *NIDA* kilichotumika kusajili namba hiyo kufungwa pia, lakini vile vile hata kifaa ambacho kimetumika pia(simu) kinafungwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali itaendelea kuongeza jitihada za kuelimisha Umma matumizi mazuri na sahihi ya *TEHAMA* kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka, swali la nyongeza.

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Wizi wa kimtandao unaongezeka kila kukicha; kwa kuwa *TCRA* kwa maana ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania wana uwezo wa kujua namba fulani inayofanya wizi ipo mahali fulani: Je, kwa nini Serikali sasa haioni kwamba uwepo utaratibu maalumu wa Jeshi la Polisi pamoja na *TCRA* kuzuia watu kabla hawajaibiwa kwa sababu wana uwezo wa ku-*trace* hiyo namba? Hilo la kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, pale namba inapotumika ambapo namba ile siyo ya kawaida kwa mfano hizi namba zinazoanzia 15000 na kuendelea ndiyo namba ambazo ni za mitandao yenyewe, unakuta zinatuma ujumbe

kwa mfano umeshinda labda shilingi milioni 600, umeshinda shilingi milioni sita, umeshinda kiasi kadhaa; anatuma mtu anaendelea kukatwa fedha zake. Sasa nauliza je, pale mwananchi ambapo anakuwa hana kosa na kosa ni la hawa wenye mitandao wenyewe kwa mfano *TiGO* au *Vodacom*, kuna mkakati gani wa Serikali ili wananchi ambao hawakufanya makosa yoyote waweze kubanwa hizi kampuni za simu kulipa fedha zao? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba nimpongeze Mheshimiwa Emmanuel Adamson Mwakasaka, Mbunge wa Tabora Mjini, kwa kazi kubwa anayoifanya kwa maslahi ya wananchi wa Jimbo lake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, naomba niwashukuru na kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa kazi kubwa ambayo wamekuwa wakiifanya kwa kushiriki katika michakato mbalimbali ya kuishauri Serikali ili tuweze kuboresha huduma kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo ambalo Mheshimiwa Mwakasaka ameliongelea ni kwamba Serikali inamakati gani wa kujaribu kuzuia wizi kabla hata haujatokea? Sheria ya makosa ya Kimatandao ya Mwaka 2015 ambayo ilianzishwa mahususi kwanza kutambua makosa yenyewe ya kimatandao ni yapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kikubwa ni kwamba kupitia Kamati ambayo imeshaundwa, kwa nafasi hiyo, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuisimamia vizuri Kamati hiyo, kazi yake kubwa ni kwenda kutoa elimu kwa Umma. Inapotoa elimu kwa Umma ni pale ambapo sasa Mtanzania anajua kabisa kwamba ni kosa lipi ambalo linahusika na sheria hii na kulihalalisha kwamba nikilifanya basi hatua za kisheria zitachukuliwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine ni kujenga uwezo kama ambavyo nimesema kwamba kuna kitengo maalum cha makosa ya kimtandao, ambayo ni *Cybercrime Unit* ambayo inashughulika na makosa haya. Lakini kuwajengea uwezo na kuleta vitendea kazi ambavyo...

**NAIBU SPIKA:** Elekea kwenye jibu la pili hilo ameshaelewa Mheshimiwa Mwakasaka. Jibu swali lake la pili. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Swali la pili anaongelea kuhusu *message* ambazo wanakuwa wanatumia. Nalo hili linaangukia katika makosa yale yale ya kimtandao tunasema *unsolicited messages*. Hili tayari tumeshakaa na watoa huduma tumeshaanza kuweka mkakati wa kuhakikisha kwamba, tunawasaidia na kuelewa kwamba namna gani *message* hizi hazitakiwi kutumwa kwa watanania ambao hawajaziomba. Matokeo yake wanakuwa na makosa ambayo hawajahusika moja kwa moja. Ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Wizara ya Maji, Mheshimiwa Minza Simon Mjika, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 102

### **Hitaji la Maji Kijiji cha Milambi - Wilaya ya Busega**

**MHE. MINZA S. MJIKA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itachimba visima vya maji katika Kata ya Mwamanyili Kijiji cha Milambi Wilayani Busega ili kuwapunguzia adha ya maji akina mama wa Kijiji hicho?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Minza Simon Mjika, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la Serikali ni kuhakikisha wananchi wanapata maji safi na salama. Serikali itafanya upanuzi wa mradi wa maji wa Mwamanyili ambao chanzo chake ni Ziwa Victoria kwenda katika Vijiji vya Mwamanyili, Mwanangi, Milambi na maeneo ya Nassa *Ginery*. Upanuzi huo utahusisha ukarabati wa chanzo cha maji, ulazaji wa bomba la urefu wa kilometa 13.6 na ujenzi wa vituo vya kuchotea maji 15. Kukamilika kwa utekelezaji wa mpango huo kutaboresha huduma ya maji hadi kufikia asilimia 54. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mpango wa muda mrefu, Serikali imepanga kutekeleza mradi mkubwa wa maji kutoka Ziwa Victoria kwenda Miji ya Busega, Bariadi na Itilima Mkoani Simiyu. Mradi huo utanufaisha zaidi ya vijiji 200 vya Miji hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Minza Simon Mjika, swali la nyongeza.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nina penda kushukuru sana kwa majibu mazuri ya Waziri. Lakini nina maswali mawili tu ya nyongeza. Katika Mkoa wa Simiyu kuna Wilaya tano lakini Wilaya ya Meatu ndio ina ukame sana kuliko Wilaya zote hizo tano. Nilipenda kujua ni lini sasa Serikali itachimba visima virefu vya maji na kusambaza katika vijiji hivyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, je, Naibu Waziri yuko tayari kuambatana pamoja nami twende naye katika Wilaya ya Meatu aone wakina mama wanavyopata adha ya maji katika Wilaya ya Meatu? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Minza Mjika kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nipende kupokea pongezi kutoka kwa Mheshimiwa Mbunge. Lakini vile vile nipende kumpongeza na yeye, kwa kazi nzuri anayoifanya kwa ushirikiano mkubwa ndani ya Wizara ya Maji. Amekuwa mfuatiliaji mzuri sana akisaidiana na Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo kaka yangu Simon wanafanya kazi nzuri kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa Serikali katika mwaka huu wa fedha 2021/2022 ni kuchimba visima virefu katika Wilaya ya Meatu. Tunatambua namna gani wakinamama wanapata shida ya maji katika Mji ule. Hivyo, tumshukuru Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan, ameliona hili na ameshatupatia fedha tutaenda sasa kifua mbele kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuambatana kwangu ni kawaida. Hivyo, niseme Mheshimiwa Minza usiwe na wasiwasi baada ya Bunge hili, baada ya kumaliza ratiba ya Mikoa niliyoipanga nitakuja kwako Simiyu hususani Meatu. Lengo ni kuona hali halisi na kuongeza chachu na ufanisi wa miradi yetu ya maji. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri Mbunge wa Meatu ni Mheshimiwa Leah Komanya, Mheshimiwa Simon Lusengekile ni Mbunge wa Busega. Kwa hiyo, naamini utawapitia hawa wote utakapoenda huko Simiyu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Jumanne Sagini, swali la nyongeza.

**MHE. JUMANNE A. SAGINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri kuhusu maji Busega. Lakini tatizo la maji Busega linakaribia kufanana na tatizo la maji Butiama. Huu ni mwezi wa tano kwenye Kijiji cha Butiama cha Baba wa Taifa hawajapata maji na

wataalam wanasema ni tatizo la mashine. Sasa Naibu Waziri atuambie lini wananchi wa Butiama wataweza kupata maji kutoka Ziwa Victoria? Na ambapo tayari kuna bomba lililochakaa lakini tatizo ni mtambo unashindwa kusukuma. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu kwa swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sagini, Mbunge wa Butiama kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara tunatambua eneo lile miradi ni mchakavu lakini tayari tumeshaelekeza wataalamu wetu kuweza kuipitia na ukarabati kufanyika, pamoja na mradi wa muda mrefu mradi wa Ziwa Victoria nao upo katika mipango mkakati ya Wizara.

**NAIBU SPIKA:** Kutokea Msekwa, Mheshimiwa Almas Maige, swali la nyongeza.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, Jimbo la Tabora Kaskazini vijiji 58 vitapata maji ya Ziwa Victoria. Swali, Je, Serikali ina mpango gani kuchimba visima virefu katika maeneo ambayo bomba la Ziwa Victoria halipiti?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Maige Mbunge wa Tabora kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu fika mradi mkubwa wa maji kutoka Ziwa Victoria umeweza kufika katika Mkoa wa Tabora. Lakini kwa maeneo ambayo mradi huu hauwezi kufika kwa sababu, bomba kuu linapopita ni kilomita 12 kulia na kushoto wanaweza kunufaika moja kwa moja.

Maeneo ambayo yako ndani zaidi mpango wa Serikali ni kuchimba hivi visima virefu na tayari Serikali imeviandaa visima zaidi ya 500 kwa ajili ya nchi nzima. Hivyo niweze kumtoa hofu Mheshimiwa Maige na yeye ataweza kuingia katika mgao wa visima hivi. Lengo ni kuona kwamba wananchi wenye imani kubwa kwa Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan wanaweza kuhudumiwa na kutuliwa ndoo kichwani. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, Mbunge wa Mbulu Vijijini sasa aulize swali lake. *(Makofi)*

Na. 103

**Mradi wa Ujazilizi kwa Mkoa wa Manyara na  
Jimbo la Mbulu Vijijini**

**MHE. FLATEI G. MASSAY** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka Mradi wa Ujazilizi katika Mkoa wa Manyara na Jimbo la Mbulu Vijijini ili kuwafikia wananchi wengi ambao hawakupitiwa na Mradi wa REA I, II na III?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Lujwahuka, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Flatei Gregory Massay Mbunge wa Mbulu Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (*REA*) inaendelea na utekelezaji wa miradi ya ujazilizi kupitia mpango wa kupeleka umeme vijijini, ili kufikisha umeme katika vitongoji vya Tanzania Bara vikiwemo vitongoji

vya Jimbo la Mbulu Vijijini. Miradi hii inatekelezwa awamu kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Mwaka 2021/2022, jumla ya vitongoji 246 katika Mkoa wa Manyara vikiwemo vitongoji vyote visivyo na umeme katika Jimbo la Mbulu Vijijini vinatarajiwa kufikishiwa umeme. Gharama ya Mradi ni shilingi bilioni 45. Zoezi la kupeleka umeme katika vitongoji ni endelevu linalotekelezwa kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (*REA*) pamoja na *TANESCO*.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Fletei Massay, swali la nyongeza.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, nimpongeze Naibu Waziri kwa kazi anayofanya na Waziri mwenyewe kwenye Wizara hii. Lakini tatizo lililoko sasa *REA* inapokwenda kwenye kupeleka umeme vijijini zinapelekwa nguzo 20 tu na kwa sababu ni vijijini, nyumba ziko mbalimbali inatokea nyumba 10 tu zinapata umeme vijijini. Je, *REA* mnaonaje kwa nini msiongeze nguzo ili nyumba nyingi zikapata nguzo kuliko kupata nguzo hizo 20? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Waziri amekuwa akitoa taarifa ya wateja wanaotumia *unit* chini ya 70 kuuziwa *unit* kwa shilingi 100. Lakini sasa wateja hawa wanauziwa *unit* kwa shilingi 300. Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa taarifa humu ili wananchi hawa wakajua nini hasa, umeme unatakiwa kulipiwa kwa hawa wateja wanaofikisha *unit* chini ya 70? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya ngongeza ya Mheshimiwa Fletei kama ifuatavyo: -



Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kumshukuru kwa pongezi alizozitoa kwa Wizara na kweli tunaendelea kujitahidi kwa maelekezo ya Serikali kuhakikisha tunatimiza maelekezo tunayopewa. Lakini nimpongeze kwa kufuatilia maeneo kwenye Jimbo lake na mimi nilienda kuzindua umeme na mambo yanakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na nimuhakikishie kwamba nguzo 20 ni kwa wateja wa awali. Naomba uniruhusu nichukue nafasi hii kuwaeleza Waheshimiwa Wabunge wote kwamba, tunapoendelea na mradi wa *REA* awamu ya tatu mzunguko wa pili karibia kila eneo tumetoa kwa kuanzia nguzo 20. Lakini ni wateja tunawaita wateja wa awali sio kwamba ndio tumemaliza zoezi, kadri muda unavyozidi kuendelea *TANESCO* wataendelea kupeleka umeme katika maeneo hayo. Lakini pia *REA* wenyewe wataendelea kuongeza wigo wa kazi wanayoifanya kuhakikisha kwamba sasa watu wengi zaidi wanapata umeme katika maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo la pili kuhusiana na gharama za umeme. Kabla sijajibu kwanza nipende kutoa shukurani zetu kubwa sana kwa Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Sita, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa kuamua kuwapenda wataanzania na kuwafikishia huduma ya umeme kwa gharama nafuu. Kwanza nguzo haziuzwi, mita haziuzwi, nyaya haziuzwi na *connection* ya umeme ni shilingi 27,000/= tu na hayo ndio maelekezo ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwenye eneo la umeme mwaka 2016 zilitengenezwa Kanuni kulingana na mazingira tuliyokuwa nayo, ambazo zilikuwa zinasema waunganishiwaji wote wa umeme na watumiaji wa umeme wa maeneo ya vijijini watauziwa *unit* 1 kwa shilingi 100 endapo matumizi hayazidi *unit* 75 kwa mwezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini maeneo ya Mijini hayakuwa yanahusika na utaratibu huu. Lakini baada ya kufikisha miundombinu mingi zaidi kwenye maeneo hata ya mjini tangu Disemba mwaka jana, Serikali imeelekeza popote

pale ulipo ili mradi unatumia *unit* zisizozidi 75 gharama ya *unit* 1 itakuwa ni shilingi 100/=. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba unipe nafasi ya kuwaelekeza Mameneja wote wa *TANESCO* nchi nzima, kukamilisha utaratibu ambao Serikali imeelekeza kupitia Wizara ya Nishati. Kuhakikisha watu wote wanaotumia umeme chini ya *unit* 75 kwa mwezi, kupata gharama kwa shilingi 9,150 ambayo ni *unit* moja ni shilingi 100. Na zoezi hili lilianza tangu mwezi wa saba. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Sasa Mheshimiwa Naibu Waziri swali lake ni kwamba, Serikali haioni namna ambavyo wale wanatakiwa kuendelea kuuziwa? Maana yake umeme umepanda bei kwa swali la Mheshimiwa Mbunge ni kwamba umeme sasa hauuzwi *unit* shilingi 100 umepanda. Sasa unampa maelekezo nani wewe ndio tunakusikiliza hapa, kwa nini umepanda yaani ndio swali lake. Kwa nini wasiendeleo kuuziwa vile vile ile bei iliyokuwepo? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa ufafanuzi. Umeme haujapanda bei, kwa siku za hivi karibuni kumekuwa kuna utaratibu mpya wa kukusanya kodi ya majengo kupitia kwenye LUKU. Tunaendelea kutoa elimu kwa wananchi kuwaelimisha kwamba hizo sio gharama za umeme bali ni *conduit* tu ya kupitisha hizi gharama za upande wa pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwenye eneo la umeme, kilichotokea ni kwamba, utaratibu wa kuwaweka watu kwenye gharama ndogo ulikuwa haujafanyika. Kwa hiyo, watu waliwekwa kwenye gharama kubwa kwa maana ya kwamba waliwekwa kwenye viwango sahihi kwa mujibu wa Kanuni zilizokuwepo mwaka 2016. Sasa kuanzia Disemba mwaka jana Kanuni zilirekebisha na utekelezaji unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelekezo ya Serikali ni kwamba, wale wote ambao walikuwa wamepelekwa kwenye tunazoiita *Tariff 1*, *Tariff 2* na *Tariff 3*, lakini gharama

zao hazizidi *unit* 75 kwa mwezi warudishwe kwenye tunayoita D1 ambayo ni *domestic one* ambayo *unit* ni shilingi 100.

**NAIBU SPIKA:** Sasa ngoja, sasa hapo umeshajibu. Wewe kaa. Maana yake ni kwamba bei inatakiwa kuwa ni ile ile sasa wewe wasiliana na watu wako wa *TANESCO* huko, wasiwauzie bei zaidi ya ile iliyokuwepo mwanzo ndio jibu lako hapo. (*Makofi*)

Kwa hiyo, Mheshimiwa kama utaendelea kupata changamoto huko Mbulu Vijijini bila shaka utampigia simu Mheshimiwa Naibu Waziri, ili awaeleze hao wa huko Mbulu Vijijini waliopandisha hiyo bei. (*Makofi*)

Wizara ya Maliasili na Utalii, Waheshimiwa Wabunge tumalizie swali la mwisho. Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris, Mbunge wa Morogoro Kusini sasa aulize swali lake.

Na. 104

### **Kuvuna Mamba Mto Ruvu Halmashauri ya Morogoro Vijijini**

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuvuna mamba katika Mto Ruvu hasa katika Vijiji vya Kigamila, Bwila juu, Magogoni, Bwila chini, Kongwa, Tulo, Lukuhinge, Kata za Mvuha na Serembala katika Halmashauri ya Morogoro Vijijini, ili kupunguza vifo vinavyosababishwa na mamba hao.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mary Masanja, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris, Mbunge wa Morogoro Kusini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kufanya tathmini ya mamba katika mito iliyopo katika Mikoa ya Katavi, Rukwa na Morogoro. Baada ya tathmini hiyo kukamilika na kubainika kuwa idadi ya mamba waliopo ni kubwa, mamba hao watafunwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, endapo itabainika kuwa idadi ya mamba katika maeneo husika ni ndogo, Serikali itabaini mamba wanaosababisha adha kwa wananchi na kuwavuna ili wasiendeleo kuleta madhara makubwa kwa wananchi. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Innocent Kalogeris, swali la nyongeza.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na idadi kubwa ya vifo ya karibu watu 60 ndani ya mwaka mmoja na watu 30 kupata vilema vya kudumu, Serikali inakuja na majibu ya kusema kwamba inafanya tathmini. Ni tathmini gani ambayo inataka kuifanya ili kujiridhisha ili waende wakavune na ni lini watakamilisha hiyo tathmini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, ni lini Serikali itatoa kifuta machozi kwa watu ambao ndugu zao wamefiwa au wameliwa na mamba na wengine wamepata majeruhi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mary Masanja, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris, Mbunge wa Morogoro Kusini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe ufafanuzi katika eneo la kufanya tathmini. Maeneo ambayo anayaongelea Mheshimiwa Mbunge ni maeneo ambayo kiuhalisia, ni maeneo ya Mito na maeneo mengi ya Mito

mamba wengi wanapenda kuishi maeneo hayo. Sekta ya Maliasili na Utalii tunahifadhi maeneo mbalimbali ambayo yanakuwa yamehifadhiwa. Lakini maeneo ya Mito ni maeneo ya mtiririko ambapo ukiangalia Mto kutoka eneo moja kwenda lingine ni eneo refu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunafanya tathmini kuangalia namna ya hawa mamba wanavyoishi majini kwa sababu, wanasafiri wanatoka njia moja kwenda njia nyingine. Unaweza ukamuona mamba yuko Morogoro lakini baada ya muda fulani ukamkuta yuko Pwani au yuko Mkoa wa Dar es Salaam. Kwa hiyo, tunafanya tathmini kuangalia hii namba ya hawa mamba ni kubwa kiasi gani. Kwa sababu, nao wana umuhimu fulani ambao katika maeneo hayo wanapaswa kuwepo sio kuwaondoa kabisa, kwa sababu vile vile, hiyo tunatambua kwamba ni moja ya maliasili ambayo inapaswa kuhifadhiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa hiyo, tukishakamilisha tathmini tutaangalia kama idadi ni kubwa basi tutawavuna. Swali la kwamba ni lini ni pale ambapo tutakamilisha tathmini ambayo sasa hivi mchakato wake tumeshaanza na kama ambavyo nimesema ni Mkoa wa Morogoro, Mkoa wa Katavi na Rukwa ambako ndio inasemekana kuna mamba ambao wanasumbua sana. Ikishakamilika tu ndani ya mwaka huu wa fedha tutawavuna ama kuwapunguza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lingine ameongelea kuhusu kifuta machozi nimtoe wasiwasi tu Mbunge kwamba, suala la kulipa kifuta machozi tumelianza toka mwaka wa fedha ulioisha na sasa hivi kuna maeneo yanaendelea kulipwa. Kwa hiyo, hata kwenye eneo lake kama wananchi hawajapata kifuta machozi basi ninawaelekeza Idara ya Wanyama Pori, wataenda katika eneo hili na wataenda kulipa wale wananchi ambao wameathirika na tatizo hili. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Wabunge tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge, lakini majibu kutoka upande wa Serikali.

Nilete tangazo la wageni nililionalo hapa mbele, tunao wageni wa Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, ambaye ni Waziri wa Viwanda na Biashara na hawa ni Viongozi na Watendaji Wakuu wa Wizara hiyo.

Kwanza tunaye Ndugu Doto James ambaye ni Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda na Biashara. Sijui amekaa upande gani? Haya, nadhani hajafika huyu.

Lakini yupo pia Dkt. Hashil Abdallah ambaye ni Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda na Biashara. Karibu sana (Makofi)

Sasa namuona mtu pembeni yako hapo sijaletewa jina lake. Kwa hiyo, na yeye anakaribishwa sana. Karibu sana. (Makofi)

Waheshimiwa tunaendelea Katibu!

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Hoja ya Kuahirisha Bunge kwa Dharura.

**NAIBU SPIKA:** Kanuni!

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo wa Spika.

Ninamuona mtu pembeni yako hapo, sijaletewa jina lake naye anakaribishwa, karibu sana. Tunaendelea Katibu!

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya kuahirisha Bunge kwa dharura!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Justine Nyamoga Kanuni.

#### HOJA YA DHARURA

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nasimama kwa Ibara ya 54 ya Kanuni ambayo inasema baada ya muda wa maswali kuisha Mbunge yeyote

anaweza kutoa hoja kuwa shughuli za Bunge zilizoorodheshwa kwenye orodha ya shughuli ziahirishwe ili Bunge lijadili jambo halisi la dharula na muhimu kwa umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa tunavyoongea Mikoa ya Iringa, Mbeya, Ruvuma, Rukwa, Songwe na baadhi ya Wilaya kama Kiteto na Kongwa zinataharuki kubwa kutokana na zao la mahindi hasa soko lake. *NFRA* wamepewa fedha kidogo na mahindi mwaka huu Mwenyezi Mungu alitujalia yalivunwa kwa kiwango kikubwa. Madhara yake ni makubwa kwa sababu tunaelekea kwenye msimu wa kilimo maana yake ni kwamba wananchi wale hawana fedha ya pembejeo wala fedha ya kulimia. Ikiwa tutamaliza Bunge hili tukanyamaza tukaondoka, hatutaweza kusikia kauli ya Serikali kuhusu kutoa fedha za kutosha ili wananchi wote ambao wamelima mahindi na wameyaweke majumbani yaweze kununuliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kutokana na udharula wa jambo hili na kwa sababu tunatarajia kumaliza Bunge hivi karibuni, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae nimeshawaona kwamba mmesimama wengi kuunga mkono hoja hii.

Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mheshimiwa Justin Nyamoga kwa mujibu wa Kanuni ya 54 akieleza kwamba lipo jambo halisi la dharura ambalo pia lina maslahi makubwa kwa umma lakini pia ni muhimu na ametaja Mikoa mbalimbali na baadhi ya Wilaya ambazo zimepata athari hizo alizokuwa anazisema.

Waheshimiwa Wabunge, kwa matakwa ya Kanuni hii huwa inabidi aeleze kwanza kama vile alivyoeleza, halafu nikiridhika kwamba ni hoja ya dharura ndiyo nampa fursa ili aeleze sasa hoja yake, tuelewe halafu ngazi hiyo ndiyo Wabunge mtaruhusiwa kama mnamuunga mkono au hamuungi mkono. Siyo kwa ngazi hii, ngazi hii alikuwa anataka kuniridhisha mimi nione kama ni ya dharura au siyo ya dharula.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nataka nimpe fursa aeleze kwa dakika tano hiyo hoja yake, halafu ndiyo atatoa hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Justin Nyamoga una dakika tano.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii ambayo umenipa ili niweze kuelezea hoja mahsusi kwa manufaa ya Taifa letu hasa wakulima wakiwemo wakulima wa Nyanda za Juu Kusini, Mikoa ya Mbeya, Rukwa, Ruvuma, Iringa pamoja na mkoa wa Songwe. Pia baadhi ya Wilaya kama Wilaya ya Kongwa, Kiteto na Wilaya nyingine za Mbulu na nyingine zinazolima mahindi. *(Mkofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka huu kulikuwa na mavuno mazuri ni Neema ya Mungu. Zao la mahindi ni zao la chakula lakini kwa Mikoa yetu ni zao la biashara pia. Wakulima wanapolima mahindi hutegemea mahindi hayo kuuza ili kupata pembejeo za mazao siyo mahindi tu kwa mwaka unaofuata lakini hata mazao mengine. Kutokana na Serikali kutoa fedha kidogo kwa *NFRA* kumekuwa na taharuki ambapo wananchi wengi wanapopeleka mahindi, mahindi hayo hayanunuliwi. Kiwango cha fedha kilichotolewa ambacho ni bilioni 14 ni kidogo sana, kutokana na hali hiyo, kuna hali ya taharuki ambapo kama hatutajadili tatizo hili, moja; mwakani wakulima hawatalima mahindi, kwa hiyo tutakosa chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili; kwa sababu sasa hivi hawauzi kwa hiyo hawapati fedha za kulima mazao mengine ikiwemo viazi, njegele na mazao mengine, kwa hiyo, ipo shida ya usalama wa chakula inayoweza kujitokeza ikiwa jambo hili litakaliwa kimya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu hiyo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa lamuliwe)*



**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, sasa tukae. Wasimame Wabunge wanaotaka kuchangia na nitawapa fursa Wabunge wachache kwa muda wetu nitawapa nafasi Wabunge Nane (8) nao watachangia kwa dakika tano tano tu.

Mheshimiwa Neema Mgaya, Mheshimiwa Judith Kapinga, Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, Mheshimiwa Mbunge wa Simanjiro, Mheshimiwa Japhet Hasunga, Mheshimiwa Condester Sichalwe, Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Msekwa.

**NAIBU SPIKA:** Haya Msekwa Mheshimiwa Vita Kawawa na Mheshimiwa Mheshimiwa Aida Khenani. Waheshimiwa Wabunge tutapata hawa wachangiaji na Katibu kila mchangiaji anachangia dakika tano, tutaanza na Mheshimiwa Neema Mgaya.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama kuunga mkono hoja iliyotolewa na Mbunge wa Jimbo la Kilolo kuhusiana na suala la mahindi. Nyanda za Juu Kusini na baadhi ya Mikoa mingine zao la mahindi ndiyo zao tegemezi kwa wananchi wetu kwa ajili ya biashara vilevile na chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kukosekana kununuliwa kwa mahindi haya kwa wananchi wetu, wakulima wetu, tunakwenda kuwapa umaskini. Kwa nini sasema hivyo, kwa sababu wananchi wale wametumia mbolea ambayo ni bei kubwa, kuzailisha mahindi hayo, lakini hii inavyoelekea kwa Serikali kushindwa kununua mahindi mengi kwa ajili ya wananchi hawa ina maana bei ya mahindi itakwenda kushuka na wananchi wale watakwenda kuuza mahindi kwa hasara kubwa na watashindwa kulima tena mwakani na kulima mazao mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali itambue kwamba wananchi hawa ambao wanalima mahindi, mahindi ndiyo uti wa mgongo wao kusomesha watoto wao na kuweza kuhudumia nyumba zao. Serikali imetoa bilioni 14 tu kwa *NFRA* kununua mahindi. Bilioni 14 inaenda kununua tani Eflu Kumi na Nne tu, wakati wazalishaji wa mahindi wanazalisha zaidi ya tani laki moja, sasa hebu fikiria zaidi ya tani laki moja lakini Serikali imetoa bilioni 14 tu ambazo zitaenda kununua tani elfu 14. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaiomba Serikali ifanye juu chini iangalie namna ya kuwasaidia wananchi wetu hawa maskini ambao wanajikwamua kwa njia ya kilimo, kulima mahindi na kama mtaona kwamba hamuwezi, hamna uwezo wa kununua mahindi mengi kuweze kukidhi mahitaji ya wale wananchi fungueni mipaka basi wananchi wetu waweze kuuza mahindi nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumza kwa uchungu mkubwa sana, kwa sababu wengine tumekua, tumelelewa na tumesomeshwa kwa biashara ya mahindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Judith Kapinga atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka ajiandae.

**MHE. JUDITH S. KAPINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa nafasi, nami napenda niunge mkono hoja hii ambayo imewekwa mezani kuhusiana na suala la mahindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ikiwemo Ruvuma, suala la mahindi kwetu ni suala la msingi sana. Kwa muda mrefu sisi wakazi wa Mkoa wa Ruvuma tumekuwa tukifanya kazi kwenye suala la mahindi kwa u-*serious* kiasi kwamba kila mwaka tumekuwa tukiongeza uzalishaji kwa sababu hamasa ambayo Serikali inatupatia. Ukichukua mfano mwaka 2019/2020 tani ambazo zilizalishwa

ilikuwa ni 787,311 ziada ilikuwa ni tani 314,928, lakini *NFRA* ilipanga kununua tani 25,000 lakini cha kushangaza walinunua tani 14,299 tu sawasawa na asilimia 4.5. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama haitoshi, mwaka huu Mkoa wa Ruvuma tumeongeza uzalishaji tena, uzalishaji umepanda kutoka tani 700,000 mpaka tani 816,242, ziada ya tani 326,497. Ununuzi uliopangwa ni tani 32,000 tu ambayo ni sawa sawa na asilimia 1.8 kwa mkoa mzima wa Ruvuma. Hili ni suala ambalo linasikitisha kwa kiasi kikubwa sana, wakulima hawa wamelima kwa nguvu kubwa sana lakini leo tunawaambia mahindi yao katika Mkoa wa Ruvuma tutanunua kwa asilimia 1.8. Kinachosikitisha zaidi hata hizo tani za awamu ya kwanza ambazo zimepangwa tani 3,000 zinanunulika kwa kusuasua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pale kituo cha Mbinga Vijijini katika Kata zote 29 kimetengwa kituo kimoja tu, yaani kama mtu anatokea kijijini kwangu lazima asafiri zaidi ya kilometa 60 kupeleka gunia zake Tano au 10 za mahindi. Lakini kama haitoshi, wamepeleka mahindi yao, lakini wanaambiwa badala ya bei iliyowekwa na Serikali 50,000/= gunia, wanaambiwa wauze kwa Shilingi 12,000! Mkulima huyu, anataweza kuinuka vipi? Kama haitoshi kwa bei hiyo ya 12,000/= sasa hivi wanaambiwa mahindi yao hayawezi kununuliwa kwa hiyo abebe gunia zake arudi nazo nyumbani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili ni kizungumkuti kikubwa sana, tulikuwa tunaelewa sawa kituo kikuu kipo kimoja, wananchi wanajikusanya hivyo hivyo kwa kujikongoja wanapeleka mahindi yao, lakini wakifika pale bei elekezi siyo ambayo inanunua mahindi yao, vilevile wanaambiwa warudi na magunia yao nyumbani. Suala hili *NFRA* walihitaji Bilioni 100 tu ili waweze kununua mahindi haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunaweza kupeleka karibia bilioni 600 kwenye korosho, mahindi hayawezi kutushinda! Tuna imani na Serikali yetu, mahindi hayawezi kutushinda, kwa mustakabari wa Mikoa hii ya Nyanda za Juu

Kusini tunaomba Serikali yetu sikivu ichukulie suala hili kwa uzito sana ili wananchi wetu wa Ruvuma, Songwe na Mikoa mingine waweze kunufaika. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, atafuatiwa na Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, Mheshimiwa Sophia Mwakagenda ajiandae.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa niseme kuwa naunga mkono kwa sababu usipopata soko huwezi kuendelea kulima, la sivyo mwaka kesho tunaweza tukaingia kwenye janga la njaa kwa sababu wakulima wengi wanaweza wakaacha kulima kwa sababu mazao yao yamejaa ndani ya nyumba zao, kama mazao yamejaa hayajauzwa utafanyaje, huwezi kulima tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, siyo mahindi tu hata na mpunga. Ukija Mkoa wa Morogoro upande wa Kilombero, Ulanga na Malinyi tuna shida ya mpunga, kwa hiyo vinakwenda kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu ya Kilimo husika imeshaongea na imekwisha kutana na Serikali, Mheshimiwa Waziiri, tumeshaliongelea hilo na naamini wamesema kuwa watalingalia jinsi ya kwenda nalo kwa sababu kweli ni tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho, namalizia kwa kusema kuwa, naomba sana wananchi, ndiyo hili suala ni tatizo kubwa lakini nawaomba wafanya biashara nao waweze kuunga mkono kwenye kununua haya mahindi kwa sababu mipaka iko wazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono ni tatizo kubwa sana na pia na mbolea na yenyewe ipo juu kidogo lakini Serikali ilishughulikia iweze kutupatia majibu. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, atafuatiwa na Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, Mheshimiwa Japheti Hasunga ajiandae.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliwahi kupata nafasi ya kufanya kazi Nyanda za Juu Kusini. Kilimo katika Mkoa ya Nyanda za Juu Kusini, huwezi kuotesha chochote bila kuwa na mbolea ya kupandia na mbolea ya kukuzia. Kama mbolea imeshafika shilingi 100,000 kwa mfuko, leo nilikuwa nauliza Wilaya ya Hai ni shilingi 110,000 kwa mfuko, lakini gunia la mahindi Songea ni shilingi 12,000 na Makete shilingi 18,000. Maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba wananchi hawa hawataweza kulima, na wasipolima maana yake wanakwenda kwenye umaskini uliotopea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu ni kuomba Serikali sikivu ya CCM kama ilivyofanya katika matukio mengine huko nyuma, wakati wa fedha tulizotoa za *stabilization*, wakati wa hali ya korosho ilivyokuwa bei yake ni mbaya, Serikali itazame bajeti yake sasa na itenge fedha za kunusuru wakulima ambao wanategemea kilimo hiki peke yake. Nikisema hivi nina maana ya nchi nzima, kwa sababu hata Babati mpaka sasa tunapozungumza pamoja na kazi nzuri ya ujengaji wa maghala hawajapewa hata shilingi moja ya kununulia hata gunia moja la mahindi kupitia *NFRA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kwamba Serikali inapaswa ijipange vizuri na kabla ya Bunge hili kumaliza Kikao chake ama leo au kesho tupate kauli sahihi ya Serikali ya kutengwa kwa fedha ili kunusuru maisha ya makulima hawa. Mahindi kwa watu wengine siyo mazao ya chakula tu ni mazao ya biashara katika Nyanda za Juu Kusini, katika Kanda ya Kaskazini, chini ya Mlima Meru, Mlima Kilimanjaro, kule Mbulu, Babati, Simanjiro, Kiteto na maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu ni hilo kwa Serikali sikivu ya Chama cha Mapinduzi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Sophia Mwakagenda atafuatiwa na Mheshimiwa Japhet Hasunga, Mheshimiwa Condester Sichelwe ajiandae.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na mimi ninapenda kuunga hoja iliyo mbele ya meza yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ndiyo Baba wa Taifa, kama inatokea *crisis* yoyote lazima Serikali ichukue wajibu wa kuhakikisha inatetea wananchi wake. Kipindi hiki cha kilimo kilichopita, wakulima wamelalamika bei za mbolea kuongezeka kiholela, kuna mbolea ya *NPK* ilikuwa inauzwa 52,000/= sasa ni shilingi 95,000 mpaka shilingi 100,000 sehemu nyingine 110,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkulima huyu kajikwamua amenunua mbolea kwa shida, amezalisha mazao yapo tayari, leo hii anashindwa kuuza tu kwa sababu bei ipo chini pia Serikali imetoa pesa kidogo kwa ajili ya kununua mazao hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukienda Nyanda za Juu Kusini kama alivyosema mtoa hoja, ni Mikoa ambayo inalima sana mahindi na ndiyo ambayo inalisha nchi hii kwa eneo kubwa sana kwa kutegemea mahindi kutoka Nyanda za Juu Kusini. Leo hii tunafahamu kabisa petroli na dizeli zote zimepanda, kwa hiyo usafirishaji vilevile pia umekuwa upo juu, tunaomba sana *NFRA* kwa kuwa wao ndiyo wana wajibu wa kununua mahindi ya wananchi wapewe fedha kutoka hizo bilioni walizopewa 14 ziweze kuongezeka kama walivyotaka wao bilioni mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wanategemea mahindi kulipa ada za watoto; Alime auze aweze kulipa ada; alime auze aweze kununua umeme; alime auze aweze

kufanya mahitaji yake madogo madogo; leo hii unapomkatisha kwa kuwa na mahindi yaliyokaa nyumbani bila ya kununuliwa huko ni kuwakatisha tamaa. Wengine wamesema hapa, tusipofanya hivyo mwaka huu ina maana mwakani utakuwa ni mwaka wa njaa kwa kuwa watu wamekwisha kukata tamaa ya kuweza kufanya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, imefanyika hivyo Nyanda za Juu Kusini kwenye viazi, wamelima viazi kwa gharama kubwa leo kiasi kinauzwa gunia kwa shilingi 12,000 hadi shilingi 17,000. Lazima Serikali isimamie hilo itafute fedha ili iweze kuongezea waweze kununua mahindi kwa wananchi kama wanavyotaka. Ninaomba Serikali itoe jibu leo hata wakisema kesho watu wetu huko nyumbani wanazimia kwa kuwa hawana pes ana mahindi yameshaanza kuharibika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga hoja mkono ili tuweze kuongezewa fedha za kununua mahindi. Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Japhet Hasunga atafuatiwa na Mheshimiwa Condester Sichalwe, Mheshimiwa Vita Kawawa ajiandae.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata hii nafasi. Kwa kweli hili tuchukulie kwamba ni janga kubwa, kwa sababu nakumbuka kabisa mwaka jana Serikali ilifanya kazi kubwa sana ya kuhamasisha wakulima kuongeza kilimo, na kazi ilipofanyika wananchi waliitikia wito, wamezalisha kwa kiwango kikubwa sana. Mkoa ya Nyanda za Juu Kusini ina mahindi mengi sana, ikiwemo Mkoa wangu wa Songwe. Mkoa wangu wa Songwe kwa upande wa chakula unashika nafasi ya tatu kitaifa, na tunajua asilimia takriban 60 Tanzania ni wakulima. Wakulima hawa baada ya kufanya kazi hii na kuzalisha sasa wamekosa kabisa soko kwenda la kuuza mahindi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sisi tunafikiri kwamba ni muhimu sasa mahali ambapo tumefika maadamu wananchi wamehamasika, wamezalisha vya

kutosha na mahindi yako mengi; sasa Serikali ichukue jukumu la kutafuta soko, kununua yale mahindina kuyahifadhi, kwenda kutafuta masoko nchini Kenya na nchi nyingine zote za Jirani ili waende wakauze maana mahindi ni biashara. Mahindi si tu chakula bali ni zao la biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasahivi ukiangalia pembejeo zimepanda sana bei, wakulima sasahivi wanasema hawataweza kulima mwakani, mbolea ya kupandia 115,000, *urea* 100,000,...

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** ...mahindi yenyewe ukichukua kwa mfano...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hasunga kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Kanyasu.

#### T A A R I F A

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanini ni muhimu sana sasahivi Serikali kuchukua jukumu la kununua mahindi, ni kwa sababu wale wateja *potential* wa mahindi ambao wangeweza kununua leo baada ya kufungua mipaka walishakuwa *scared* kutokana na tabia yetu ya kubadilika badilika. Kwa hiyo, mtu ambaye anataka mahindi alishaagiza mbali na ana *stock*. Kwa hiyo mteja pekee aliyebaki leo ambaye ni *reliable* wa mahindi hata ukifungua mipaka Tanzania, ni Serikali. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hasunga, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea kwa mikono miwili, nashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, kwamba kwa kweli sasahivi pembejeo zimepanda sana bei, gunia la



mahindi Mkoa wa Songwe sasahivi ni 18,000 mpaka 24,000. Atauza magunia mangapi ili aweze kupata mbolea na ili aweze kuendelea na kilimo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ilivyo hapa tulikofikia tunaiomba Serikali itoe fedha ikanunue mahindi yote ya wakulima ili wakulima hawa waendeleo kuzalisha nchini; na ikishatoa hizo fedha itasaidia sana. Wakulima hawa wanahitaji kusomesha watoto, wanahitaji kila kitu kutokana na kilimo hicho. Sasa hivi *NFRA* walitoa bilioni 14, ukichukua Bodi ya Nafaka ilipewa sijui bilioni ngapi, yaani hawajanunua hata asilimia tano ya mazao ya wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nafikiri Serikali illipe uzito hili suala. Ni suala la kitaifa na ni suala la *emergency*; itafutwe fedha mahali popote tukanunue hayo mazao tukawasaidie hao wakulima ili waendeleo kuzalisha kwa niaba yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Mbunge. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Condester Sichalwe, atafuatiwa na Mheshimiwa Vita Kawawa, Mheshimiwa Aida Khenani ajiandae.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niseme naunga mkono hoja iliyoko mezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, miongoni mwa kitu ambacho kinaendelea kuzua taharuki sana kwa wakuima hawa, pamoja na kwamba Serikali imetoa hela kidogo na kuweka vituo vichache vya kununulia mahindi lakini kinachowaumiza wananchi hawa *especially* mwananchi wa chini ambaye ana gunia mbili, tano mpaka 10, 20 ni pale ambapo wanaona hata hicho kidogo chao hakinunuliwi; na zaidi utakuta wakati mwingine mahindi yanatoka sehemu nyingine yanunuliwa. Hii yote imetokea kwa sababu Serikali imetoa tani kidogo na imeweka vituo vichache.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kwa Serikali; kwa nini hicho kiwango kidogo cha pesa ambacho kimetolewa kwanza kisimuangalie mkulima huyu mwenye kipato cha chini kabisa ambaye ana tani moja ama mbili, ambaye hata kulima wakati mwingine pembejeo na mbolea ni changamoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia Serikali ifungue mipaka. Tunazo nchi za karibu Zambia, Congo pamoja na nchi zingine ambazo wanahitaji mahindi hayo ili angalu wale wafanyabiashara ambao wana tani nyingi na wanatamani kutoa mazao yao nje nje, wawape hicho kibali na nafasi ya kupeleka mahindi hayo ili kile kidogo kama bado Serikali haijapata hela ya kutosha kununua mahindi kwa wingi waweze kuwahudumia wananchi hawa ambao wana gunia chache.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hata hawa ambao wana gunia mbili, tatu hawana pa kuuza, wameendelea kulalamika, wamejaza gunia zao tatu hapo, akina mama wamejazana, wanashindwa kupika. Ni kweli, Serikali hata akina mama hao wenye gunia kumi wameshindwa kuwaangalia, kuwapa nafasi, kuwasaidia?

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninaamini kwamba Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi ni Serikali sikivu sana. Tunaomba imuangalie mwananchi huyu wa kipato cha chini na kidogo ambaye amelima kwa jembe la mkono na hana hata uwezo wa kusafirisha kupeleka hapo Zambia. Hicho kidogo ambacho Serikali imepata imuangalie kwanza huyu mkulima wa chini ambaye ana gunia chache. kwa kuwa vituo ni vichache hawa wananchi wa kawaida ndio wapewe nafasi; lakini Serikali ifungue masoko hawa wafanyabiashara wakubwa, kwa sababu wana uwezo wa kupeleka mazao yao huko nje waupeleke huko. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Vita Kawawa kutokea Msekwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Aida Khenani, Mheshimiwa Kenneth Nolo ajiandae.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza niunge mkono hoja hii ya Mbunge wa Kilolo ambayo ameileta kwa waakati muafaka; na nakushukuru wewe Naibu Spika kwa kukubali hoja hii tuijadili kwa mujibu wa Kanuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa wenzangu wameelezea vizuri sana. Wa Mkoa wa Ruvuma tani tulizozialisha mwaka huu ni zaidi ya laki nane. Sisi kabla Serikali haijatoa kauli yake ya kununua wakulima walikuwa wanauza kilo moja shilingi 155. Walikuwa wanunuliwa kilo zao zile za mahindi kwenye *dumla* au kwenye kisado kile, kikombe kimoja cha lita nne ambacho wao wanunuzi, walanguzi walikuwa wanatia mchanga wa moto ambao umekaangwa halafu kile kindoo kile kinanenepa kinakuwa kama chura hivi. Kwa hiyo, zinakuwa kilo nyingi wanunua kwa shilingi 700, sawasawa na kilo moja shilingi 150.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilipotangaza kwamba watakuja kununua shilingi 500 tukawaambia wakulima waache kuuza kiholela na wakaamini Serikali yao itanunua mahindi yao. Sisi tulipangiwa tani 32,000 ndizo zitanunuliwa na Serikali, lakini mpaka sasahivi tumeanza kununua na tani 3,000. Tani 3,000 ni sawasawa na milioni 15 kwa shilingi 500; na ununuzi wake kwa Namtumbo wamenunua tani 300, tu lakini mahindi yamejaa tele pale, kwa hiyo ni *chaostupu* pale Namtumbo. Kila siku kelele na lawama.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima wameleta mahindi yao kutoka mbali, wameyasafirisha yapo pale lakini mahindi hayanunuliwi kwa sababu fedha hakuna za kuongeza kununua mahindi. Mpaka sasahivi zimenunuliwa tani 300.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu, naomba Serikali iziongeze fedha za kutosha kwenye *NFRA* ili waweze kununua na kwa wakati ili na wakulima waweze kupata fedha zao wajiandae na kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni mwezi wa tisa sisi ndiyo tunaanza kuandaa mahindi kule kwetu, na huwezi kuandaa

mashamba bila fedha, huwezi kununua mbolea bila fedha na fedha yao ndiyo mahindi yao. Sisi hatuna zao la biashara kubwa pale, ni mahindi na hayo ndiyo mahindi ya chakula tunaipa Serikali. Sasa tusije tukawakatisha tamaa wakulima mwakani wakashindwa kulima nchi yetu ikapata mazao machache na tukaingia na njaa.

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda anaopewa mchangiaji ni mfupi. Ni nani anayetaka kutoa taarifa? Taarifa hii itakuwa ya mwisho.

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE:** Huku Msekwa...

**NAIBU SPIKA:** Msekwa, ni nani anayetoa taarifa?

**MHE. ALLY. A. M. JUMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mlaghila Jumbe.

**NAIBU SPIKA:** Mekwa, karibu, Mheshimiwa Ally Kinanasi, taarifa.

## T A A R I F A

**MHE. ALLY. A. J. M. JUMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimpe taarifa mchangiaji kwamba, kama Serikali inaona pesa ni kidogo na kwamba imeamua kutoa pesa kidogo kidogo; na janga hili ni janga ambalo lipo kitaifa na limetokana na UVIKO 19.

Sasa kama tunapata msaada wa pesa za *relief* ya majanga ya UVIKO, mimi ningeomba pesa hizo za UVIKO pia zipelekwe kwenye kununua mahindi. Naomba nimpe taarifa hiyo. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Vita Kawawa unaipokea taarifa hiyo? Mheshimiwa Vita Kawawa hatukusikii kutoka Msekwa.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo, *microphone* yangu ilikuwa inasumbua kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakubaliana naye kwamba fedha za msaada tutakazozipata basi zije kujazilizia katika haya. Lakini kwa sasahivi fedha tulizonazo, maana hizi hatujui zinakuja lini, ziko kwa watu. Mpaka zitakapokuja hatujui ni lini, lakini wananchi wanataka wanunuliwe mahindi yao sasahivi. Kama kuna fungu linaweza likaazimwa liazimwe ili wananchi wakulima wa Tanzania waaminifu wanunuliwe mahindi yao sasahivi hizo fedha zitakuwa ku-cover.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi ushauri wangu kwa Serikali, *disbursement* ya hela hizi zisiende kama kwenye miradi mingine. Hili ni suala la dharura, na tulishawaahidi wananchi tunanunua haya mahindi. Tupeleke fedha hizi sasa hivi, za kutosha, washindwe wao *NFRA* kununua. Tupeleke wanunue mahindi kama Serikali ilivyokusudia kununua tani hizo 120,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakuomba sana na naunga mkono hoja. Ahsante sana (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Aida Khenani, atafuatiwa na Mheshimiwa Kenneth Nolo, Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda ajiandae.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nami naunga mkono hoja hii kwa umuhimu wake na madhara ambayo wameyapata Watanzania kwa muda wa miaka mitano sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya dakika tano; ningependa kulieleza Bunge na Wabunge wenzangu wajue, ni wajibu wa Serikali aidha yenyewe inunue kwa mkulima au itafute masoko kwa sababu ya wananchi wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka juzi tumezungumza hapa, pamoja na kuwa na mpango, pamoja na Ilani, pamoja na kupitisha bajeti bado jambo hili limekuwa ni sugu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mazingira yoyote yale, mimi natambua kwamba kila mwaka Serikali inafanya tathmini ya uzalishaji kwa Watanzania; na kama wanajua wamezalisha kiasi gani lazima wajue kiasi gani ni akiba kwa taifa ana kiasi gani kinatakiwa kipelekwe kiuzwe nje ya nchi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua kwamba kuna ugonjwa huu ambao uko ambao sio wa Tanzania, ni dunia nzima, lakini lazima Serikali iwe na Mpango. Pamoja na kwamba hili janga liko dunia nzima lakini lazima Serikali ifikiri ziada. Kama ugonjwa huu uko duniani kote kwa hiyo tunataka Watanzania wafe?

Mheshimiwa Naibu Spika, mahindi kwetu ni siasa, ni maisha. Hatuwezi kukubali Watanzania; mimi nimekwenda moja kwa moja, lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu, nilikwenda mimi mwezi Januari nikamwambia Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa sababu watu wana mahindi ya tangu mwaka juzi, mwaka jana na mwaka huu, wamezalisha tena, tunaomba kibali ili tuweze kutumia bandari zetu ambazo Serikali imewekeza fedha za kutosha kutumia hizo nchi za jirani kuweza kuuza mahindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua jitihada za Mheshimiwa Waziri Mkuu ambazo alizifanya, lakini mpaka sasa tuko kwenye ushindani, na kama ni ushindani lazima twende na muda. Tayari wenzetu wameshateka soko la Congo na Burundi. Kwanini sisi siku zote tunakuwa wa mwisho? Leo hata kama mkichukua maamuzi, tunawaambia hawa watu kwamba hiyo bilioni 14 tuliyopeleka hawa Watanzania hawana hata sehemu ya kuhifadhi mahindi, Serikali ina wajibu wa kuchukua mazao hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sSasa kama mpaka sasa hakuna utaratibu wa Serikali uliotolewa ni namna gani watahifadhi hayo mahindi kutoka kwa Watanzania ambao wamezalisha kwa miaka mitatu; ushauri kwa Serikali, mnaweza kusitisha miradi mingine ambayo haina ulazima kwa sasa tuweze kuwaokoa Watanzania ambao

tunategemea mahindi ndiyo korosho yetu, ndiyo dhahabu yetu Nyanda za Juu Kusini. Tunaiomba Serikali, kama ambavyo imeweza kuchukua hatua kwa mazao mengine Tanzania iangalie na zao la mahindi kwa jicho jingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kenneth Nollo, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Adold Mkenda, mtoa hoha ajandae.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi hii. Nami naiunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka tu tujikumbushe kwamba *NFRA* na Bodi ya Mazao Mchanganyiko zimeanzishwa kwa sheria mbili tofauti. *NFRA* imeanzishwa kwa kununua chakula iwapo yatatokea majanga na ukosefu wa chakula hapa nchini. Lakini, vile vile Bodi ya Mazao Mchanganyiko ile inafanya biashara ya mazao kwa kununua mahindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi nataka kutofautiana kidogo kwamba *NFRA* tunasema inunue mahindi, lakini yenyewe inanunua mahindi kwa kuangalia majanga yanayokuja mbeleni na tathmini ya majanga. Sasa hii *stocking* ambayo tunataka *NFRA* inunue, inanunua ili ije kufanyia nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, hii nayo itoe somo kwa wenzetu wa Serikali. Kwamba huwezi ukaelekeza kwamba tutanunua kwa 500 halafu *NFRA* uwezo huo haina. *NFRA* yenyewe hadi leo inaidai Serikali kama bilioni 160 ambayo imefanya kazi miaka sita iliyopita. Kwa hiyo kwenye upande huu naona ni vigumu kusema *NFRA* inunue leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa sasa mahindi ya Zambia yananunuliwa zaidi kwenye ukanda wetu huu. Shida inayotusumbua ni kwamba sisi hatutoi mahindi yaliyo bora. Kwa hiyo ninachotaka kushauri na sisi tuelewe, hatuwezi

kuilazimisha sasa kama *NFRA* inunue mahindi kwa *crisis*. Mahindi haya ni biashara...

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** ...tusiweke *control* kwenye habari ya mahindi. Tuache mahindi soko litaji-*regulate* watu watanunua mahindi. Tumekuwa tunauza mahindi...

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jesca, kwa sababu zilikuwa zinatolewa dakika tano nilisema Taarifa iliyotolewa na Mheshimiwa Ally Mlaghila Jumbe ilikuwa ya mwisho. Mheshimiwa Kenneth Nollo malizia mchango wako.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mahindi haya tumelima na tumelima kibiashara. Ukianza kusema kuna *crisis* kama ya moto umewaka uzime leo tsubiri, bei zitapanda mahindi yatauzwa. Hii ndiyo mara ya kwanza kuuza mahindi kwenye nchi yetu? Kwa hiyo, mimi ndiyo maana nilisema tukianza kuiambia Serikali ichukue fedha zingine inunue mahindi hapana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mahindi haya tumelima kwa ajili ya biashara...

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa, anapotosha huyu.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** ... ni msimamo wangu na nataka hili nieleweke namna hiyo...

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tusikilizane; namlinda mchangiaji. Maliza hoja yako.



**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kusema mahindi haya tumelima kwa ajili ya biashara na bado tuna muda mahindi haya tutauza na ukitaka kusema kuna *crisis* uingize Serikali kwa namna hii tunatengeneza *trend* ambayo baadaye itatusumbua...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa!

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** ... hii ni biashara...

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU SPIKA:** Haya, ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa, tunazungumzia mahindi si zabibu.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane. Ameshamaliza mchango wake. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda, Mtoa Hoja ajiandae.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe maelezo ya Serikali yafuatayo...

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumsikilize mchangiaji. Karibu Mheshimiwa Profesa Mkenda.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naomba nitoe maelezo ya Serikali yafuatayo...

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hebu tumsikilize mchangiaji. Karibu Mheshimiwa Profesa Mkenda.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba nitoe maelezo ya Serikali yafuatayo kuhusiana na hii changamoto ya kweli ya bei ndogo sana ya mahindi hasa katika Mikoa ya Ruvuma, Rukwa, Katavi pamoja na Nyanda za Juu Kusini kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli kwamba mwaka huu tumezalisha ziada mahindi mara mbili kuliko ziada iliyozalishwa mwaka jana. Na ni ukweli hapa katikati tulipata changamoto kidogo ya soko la nchi jirani ambayo wote tuliisikia na ambayo hatimaye ilikuja kutatuliwa. Ni kweli mpaka sasa hivi bei ya mahindi katika baadhi ya maeneo kwa kweli ni ndogo sana, inaleta changamoto na tunaogopa isije ikavunja moyo wakulima kwa msimu mpya wa kilimo unaokuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali. Kwanza, hatujatoa katazo la aina yoyote la kusafirisha mahindi nje ya nchi, nchi yoyote iwe ni Zambia, DRC, Kenya, *South Sudan* na kadhalika. Vilevile tumeharakisha sana kasi ya kutoa vibali vya kusafirisha mazao nje ya nchi kwa wale ambao wanataka kuuza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, tukumbuke wakati tulivyopata changamoto hii ya kuuza mahindi nje, Mheshimiwa Rais alifanya ziara ya Kitaifa Kenya na baadhi ya mambo aliyofanya ni kuhakikisha kwamba soko la Kenya linafunguka. Sasa hivi kwa taarifa tu ni kwamba kwa kweli mahindi yanakwenda kwa kasi sana lakini bado bei haijanyanyuka vya kutosha, hasa Mkoa wa Ruvuma, Rukwa, Katavi na upande huu, hasa upande wa Nyanda za Juu Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kwa upande wetu Serikali Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko imeingia mkataba sasa hivi na kampuni Mombasa ya kuuza zaidi ya tani laki moja kwa mwaka ya mahindi na imeanza kuyasafirisha

kuyapeleka Mombasa. Imefungua kituo cha kuuzia mahindi Nairobi na hivi tunavyozungumza timu inarudi kutoka Jubbah, Sudani ya Kusini, wamefunga mkataba, tunakuwa na kituo cha kuuza nafaka ya Tanzania nchini Sudani ya Kusini. Pamoja na hivyo bado tuna mkakati wa kuingia DRC na nchi nyingine kwa ajili ya kuuza si mahindi tu, lakini pamoja na mchele wetu. Timu nyingine iko Morocco, Comoro, tunaenda Zimbabwe na kadhalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tunakamilisha mazungumzo na *WFP* kwa ajili ya kununua mahindi, lakini itakuwa takribani tani 20,000, pengine siyo kiasi cha kutosha sana kubadilisha bei. *NFRA* na Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko wote wako sokoni na tuliwaagiza wawekeze nguvu zao Nyanda za Juu Kusini, hasa kule ambapo wafanyabiashara sasa hivi hawaendi kuchukua mahindi, kwa sababu sasa hivi soko lililofunguka sana ni soko la Kenya. Tumeona wengine kwenye *clip* kwamba fedha walizopata *NFRA* hazikutosha na ugomvi unatokea wakati wa kuuza, ni kwa sababu shilingi bilioni 14 ni wazi kabisa hazikuweza kutosha kununua mahindi hayo na haijakidhi kabisa mahitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napenda kutoa tu taarifa kwamba maelekezo ya chama wote tumeyasikia na maelekezo ni Wizara ya Kilimo ikae na Hazina izungumze, *specific* maelekezo tuliyasikia wote. Napenda kutoa taarifa kwamba mazungumzo yanaenda vizuri sana kwa yale maagizo ambayo tumepewa na Katibu Mkuu wa Chama na tunatumaini kuyamaliza pengine kabla Bunge halijaisha ili tuje kutoa taarifa kwamba tunaingia tena kazini kwenda kununua mahindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Justin Nyamoga, hitimisha hoja yako.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikushukuru sana wewe mwenyewe kwa kutoa nafasi ili hoja hii mahsus iweze kujadiliwa. Pia niwashukuru Wabunge

wote waliosimama kuunga mkono hoja na wale waliochangia hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zao la mahindi ni zao la biashara na hii dharura ya kutokea kwamba mazao hayajanunuliwa na Serikali ikachukua hatua, mahindi siyo zao la kwanza. Yako mazao mengine ambayo dharura kama hizi zilitokea na Serikali iliongeza fedha na mazao hayo yakanunuliwa. Ili kujenga usawa wa Watanzania wakulima wa mahindi wana haki pia kama yale mazao mengine ilivyokuwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi naiomba Serikali kwamba fedha kwa ajili ya kununulia mahindi ziongezwe kutoka shilingi bilioni 14 zilizotolewa mpaka shilingi angalau bilioni 100 ili kiwango kikubwa zaidi cha mahindi kiweze kununuliwa. Tumesikia maagizo na maelekezo ya chama, lakini kauli ya Serikali hapa ni muhimu sana ili sisi tunapotoka hapa Bungeni tukawaambie wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo la pili, naomba vituo vya kununulia mahindi viongezwe na kusogezwa karibu na wananchi. Haiwezekani Wilaya ya Kilolo isiwe na kituo hata kimoja watu wapeleke mahindi Iringa Mjini au Makambako ambapo ni kilometa nyingi tu. Huu nimetoa mfamo mmoja, lakini iko mifano mingi sana ambapo vituo hivi ni vichache na vinamtaka mkulima kusafirisha mazao, mkulima huyu ana magunia mawili, kumi, 20, kwa namna hii ni kuendelea kuwakandamiza wakulima na huenda tukashindwa kusonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu, Serikali pamoja na kwamba haijafungua mipaka, mipaka iko wazi lakini hawa wakulima tunaozungumza si wakulima wasafirishaji, Serikali isaidie katika kuhakikisha kwamba masoko yanapatikana, wanunuzi wanakuja na wananunua mahindi kutoka kwa wakulima hawa wadogo wadogo. Wakulima wanaoweza kusafirisha mahindi kupeleka nje ya nchi ni wachache, wakulima wengi ni wadogowadogo na wanahitaji mapato, kwa hiyo, Serikali ifanye hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo la nne, naiomba sasa Serikali kwa kujua kwamba hali ya ununuzi wa mahindi ni duni, kwa kujua kwamba tuko kwenye maandalizi ya kilimo mwakani, ifanye haraka kuhakikisha kwamba bei za pembejeo zinashuka. Kwa sababu, kama mahindi tunaanza kwa kilo shilingi 250 hadi 300 na mwezi Oktoba tunaanza kulima mahindi na tunahitaji mbolea wakulima hawa watawezaje sasa kununua mbolea kwa ajili ya mwakani? Kwa hiyo, suala la mbolea pia Serikali ihakikishe kwamba hizo bei zinashuka mapema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi napendekeza kwamba haya ambayo nimeyapendekeza yawe ni Maazimio ya Bunge hili ili Serikali iweze kuyafanyia kazi na ili wananchi wetu waliotutuma hapa Bungeni waweze kunufaika na Serikali yao. Mimi nina uhakika kwamba kama *NRFA* italundika mahindi mengi na yenyewe itafute masoko, iuze ipunguze inunue mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kutoa hoja hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nyamoga kwa sababu tunaendelea kujifunza Kanuni, unatoa tena hoja.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, sasa tukae.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijawahoji juu ya Maazimio ambayo ameyataja hapo Mheshimiwa Justin Nyamoga, Mheshimiwa Waziri Mkuu tukonaye hapa Bungeni, pengine ana jambo la kusema kabla sijalihoji Bunge. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, Serikali imesikia kilio hiki na Serikali ilianza zoezi la kununua mahindi kupitia Bodi ya Mazao Mchanganyiko kwa takribani mwezi mmoja sasa. Tulichojifunza kama Mheshimiwa Waziri wa Kilimo alivyoeleza kwamba mwaka huu uzalishaji umekuwa mkubwa na kwa hiyo Serikali tumeendeelea kuweka utaratibu wa kununua mazao haya. Moja, ni kwa Serikali yenyewe kwenda kununua kama ambavyo tunafanya kila mwaka kupitia Bodi ya Mazao Mchanganyiko pamoja na *NFRA* ambayo huwa inaweka akiba ya chakula ya Taifa kwa ajili ya matukio yetu ya ndani au inapotokea majirani wanapata matukio *NFRA* ndio inashughulikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kupitia uzalishaji huu tumezungumza na mataifa ya jirani, Mheshimiwa Waziri ameeleza tumezungumza na Sudani Kusini, Kenya na Mheshimiwa Rais alikuwa pale na tumezungumza na nchi jirani kama Burundi. Ni kweli kwamba nchi hizi nazo pia zimelima mazao haya na wamezalisha pia, kwa hiyo, kiwango cha kuagiza na kununua nchini kwetu sio kikubwa sana kama miaka mingine ambapo wanapata madhara ya hali ya hewa na kununua chakula kingi zaidi nchini kwetu. Hata hivyo, haya yote hayatufanyi sisi tushindwe kununua mahindi haya. Kama ambavyo tuliwapa taarifa wiki mbili zilizopita Serikali ilitoa shilingi bilioni 14 tumeipa *NFRA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wiki iliyopita nilijibu swali hapa la upungufu wa vituo na Serikali ina msimamo gani juu ya kuongeza vituo. Tulishaagiza *NFRA* pamoja na Bodi ya Mazao Mchanganyiko kufungua matawi kila Wilaya ili irahisishwe kuwafikia wakulima kwa ukaribu zaidi. Sasa hivi bado mahindi ni mengi, mkakati wetu ambao tumeufanya tumeshaomba fedha Hazina tuweze kuwaongezea fedha za kutosha kwa lengo lilelile la kuweza kununua mahindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ombi ambalo tena tumeliomba na tumekuwa tukiwasiliana hapa na Mheshimiwa Waziri yuko safarini ambaye tulikuwa

tunawasiliana kwa ukaribu, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote hasa wakulima wa zao hili la mahindi wa mikoa hii ya Nyanda za Juu Kusini kwamba kesho tutakapokuwa hapa kabla hatujahitimisha Bunge Serikali itatoa taarifa kamili juu ya utaratibu utakaotumika kununua mahindi hayo kutoka mikononi mwa wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya Serikali ni mazuri, tunatamani wakulima waingie kwenye msimu huu wa kilimo kwa ajili ya mwakani na wakulima waendeleo kutegemea zao hili kwa matumizi yote mawili, chakula, lakini pia hata biashara ambapo pia zao hili linatumika kama zao la biashara. Kwa hiyo, tuwape faraja Watanzania kwamba Serikali ipo, Serikali yenu sikivu na hili ambalo Waheshimiwa Wabunge hapa mmelizungumza tumesikia na kesho tutatoa Taarifa ya Serikali. Sina mashaka taarifa ambayo tutaitoa kesho ni ya kuwapa matumaini wakulima ili waendeleo na mikakati yao ya kulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni lile ambalo nimelieleza hapa wakati wa Maswali ya Papo kwa Papo kuhusiana na upatikanaji wa pembejeo, hasa kwenye eneo la mbolea. Tumeleza, naomba nirudie tena kwamba mahitaji ya mbolea mwaka huu duniani kote ni makubwa na yamezidi uwezo wa uzalishaji wa viwanda vyetu vilivyopo. Serikali ilijua hili na tukachukua hatua mbalimbali za muda mfupi na za muda mrefu. Hatua ya muda mfupi ambayo tumeichukua ni ile ambayo tumetoa fursa kwa Watanzania, wafanyabiashara kuagiza mbolea kutoka popote duniani ili kuileta hapa nchini tukiamini kwamba kwa ushindani huo ambao tutaufanya tunaweza kupunguza angalau wimbi la upandaji wa bei ya mbolea duniani ambako pia na hapa kwetu nchini tunapata athari hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mbili, mpango wa muda mrefu ni ule ambao tumeusema wa kuwasihi, kuwaomba, kuwapa fursa wawekezaji kutoka nje kuja kuwekeza viwanda vya mbolea hapa nchini. Nimeleza hapa kwamba mwezi mmoja uliopita nilikuwa nchini Burundi

kwa lengo la kukutana na mwekezaji wa uzalishaji wa mbolea na tayari amekubali na tumempa eneo hapa Dodoma anaanza kujenga eneo la Nala, tutakuwa na kiwanda kikubwa sana cha uzalishaji wa mbolea, pamoja na wengine ambao tumeendelea kuzungumza nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo wiki tatu/mwezi mmoja uliopita alikuwa nchini Morocco, amepata nafasi ya kuzungumza na wawekezaji wa mbolea lakini pia na wao wanasambaza mbolea duniani ili tupate mgawo wa kutosha. Yote haya ni tunamlenga mkulima aweze kulima mazao yake kwa kutumia pembejeo ambayo sasa tunafanyia jitihada kuipata. Kwa hiyo, mbinu zote hizi zinalenga kuboresha kilimo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba niwasihi, kesho Serikali itakuja na Kauli yake hapa kwa ajili ya jambo hili. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa ufafanuzi huo. Japokuwa tutakuwa tukisubiri hiyo taarifa, sisi kama wawakilishi wa wananchi, lakini sasa hoja yetu inabidi ifungwe kwa mimi kuwahoji Waheshimiwa Wabunge na sasa nitawahoji katika Maazimio yale ambayo ameyaleta Mtoa Hoja, Mheshimiwa Justin Nyamoga kwamba mosi; pesa ziongezwe; pili, vituo vya kununulia mahindi viongezwe; tatu, mipaka ya nchi ifunguliwe ili wafanyabiashara waweze kupeleka mahindi yao nje na nne, bei za pembejeo zishuke kabla ya msimu unaokuja.

*(Hoja lilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Bunge Liliridhia Hoja ya Mhe. Justin L. Nyamoga kuhusu Ununuzi wa Mahindi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, alisimama Mheshimiwa Justin Nyamoga kwa mujibu wa Kanuni ya 54, akatoa hoja ambayo niliridhika kwamba ni hoja ya dharura kuhusu ununuzi wa zao la mahindi. Waheshimiwa Wabunge,



mmepata nafasi ya kuchangia na yeye amepata fursa ya kuhitimisha hoja yake, sitarejea hayo kwa ajili ya muda na sasa Bunge limeshaazimia hayo mambo manne ambayo nimetoka kuwahoji hapa. Bila shaka katika taarifa atakayokuwa anaitoa Mheshimiwa Waziri Mkuu siku ya kesho Maazimio haya ya Bunge yatapata ufafanuzi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, kwa ujumla tuseme Bunge limeazimia siku ya leo kuhusu zao la mahindi kwamba, kwanza, Serikali iongeze pesa ili wakulima waweze kuuza mahindi yao. Pili, vituo vya kununulia mahindi viongezeke ili wakulima wasiende mwendo mrefu kwenda kuuza mahindi yao. Tatu, ni mipaka ya nchi ifunguliwe ili wafanyabiashara waweze kwenda kuuza, lakini pia wale wanaotaka kuja kununua waweze kuja. Nne, pembejeo zipungue bei kabla msimu wa kilimo haujaanza. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, hayo ndiyo yaliyokuwa Maazimio ya Bunge kwenye hoja hii ya ununuzi wa mahindi. *(Makofi)*

Tutaendelea na hoja iliyo mbele yetu, Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

### **HOJA ZA SERIKALI**

#### **MAAZIMIO**

**Azimio la Bunge la kuridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa Eneo Huru la Biashara la Afrika *(Agreement Establishing African Continental Free Trade Area – AfCFTA)***

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa nimuite Waziri wa Viwanda na Biashara ili aje atoe hoja yake kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa Eneo Huru la Biashara la Afrika. Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijasoma Azimio la Bunge, naomba uniruhusu nitoe maelezo mafupi kuhusu mkataba huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2013 nchi za Afrika ziliadhimisha miaka 50 tangu kuanzishwa kwa Umoja wa Afrika. Katika kikao hicho wakuu wa nchi na wakuu wa Serikali walifanya tathmini ya miaka 50 ya Umoja huu, wakaangalia changamoto na mafanikio na wakaazimia kwamba itengenezwe dira ya miaka mingine 50 ya Afrika na mwaka 2015 dira hii ikapitishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya misingi ya dira hii ni kuanzishwa kwa eneo huru la biashara la Afrika. Dira hii ina miradi ya kielelezo 17 na mradi namba tatu ni kuanzishwa kwa eneo huru la Afrika. Kwa hiyo, majadiliano yamefanyika na hatimaye tarehe 21 Machi, 2018 katika mkutano wa dharura wa 10 uliofanyika Mjini Kigali wakuu wa nchi na Serikali walikubaliana kusaini mkataba huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu wakati huo mpaka mwaka 2019 nchi 54 kati ya nchi 55 wanachama wa Umoja wa Afrika walishasaini mkataba huu, ikiwemo nchi yetu. Baada ya kusainiwa kwa mkataba huu hatua iliyofuata ni kuridhiwa kwa mkataba na kwa mujibu wa Ibara ya 23(1) ya mkataba huu nchi 22 zikisharidhia mkataba huu unaanza kufanya kazi. Mei, 2019 tayari nchi 22 zilipatikana kwa hivyo, mkataba huu ukawa hai.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa mkataba huu umesharidhiwa na nchi 41 na umeanza kufanya kazi rasmi kwa maana ya kufanya biashara tangu tarehe 01 Julai, mwaka jana. Mkataba huu una maeneo ya msingi saba.

Kwanza, tuna eneo la biashara ya bidhaa, biashara ya huduma, usuluhishi wa migogoro, eneo la uwekezaji, hakimiliki ya ubunifu, sera ya ushindani na hatimaye tuna biashara ya mtandao (*e-commerce*).

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo mafupi, naomba sasa nisome Azimio la Bunge, kama ifuatavyo:-

Azimio la Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania la Kurudhia Mkataba wa Uanzishwaji wa Eneo Huru la Biashara Afrika (*Agreement Establishing the African Continent Free Trade Area – AFCFTA*).

KWA KUWA Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Mwanachama wa Umoja wa Afrika kupitia hati iliyosainiwa na Serikali na kuwasilishwa Sekretarieti ya Umoja huo mnamo tarehe 25 Mei, 1963;

NA KWA KUWA Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika katika Mkataba wa Abuja mwaka 1991, Ibara ya 4(2)(d) ya mkataba huo inaelekeza kuanzishwa kwa soko huru baina ya nchi za Afrika;

NA KWA KUWA Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika waliandaa Mkataba wa Uanzishwaji wa Eneo Huru la Biashara la Afrika;

NA KWA KUWA mkataba huo unalenga kuchochea uchumi na biashara miongoni mwa Nchi Wanachama kwa kufunguliana masoko ya biashara ya bidhaa na huduma kwa kuondoleana ushuru wa forodha na kulegezeana masharti na taratibu nyingine zisizokuwa za kiushuru;

NA KWA KUWA hadi tarehe 31 Julai, 2021 Nchi Wanachama 41 kati ya Wanachama 55 wa Umoja wa Afrika zilikuwa zimesharidhia mkataba huo ambapo ni Nchi Wanachama 18 pekee bado hazijaridhia mkataba huo ikiwemo Tanzania na Sudani Kusini kwa upande wa Jumuiya ya Afrika Mashariki;

NA KWA KUWA Tanzania kama Mwanachama wa Umoja wa Afrika na moja ya nchi zilizosaini mkataba huo inapaswa kuridhia mkataba huo ili kukidhi matakwa ya

mkataba husika na pia kuwezesha utekelezaji wa mkataba wa uanzishaji wa eneo huru la biashara la Afrika nchini;

NA KWA KUWA Nchi Wanachama zinatambua kuwa kuridhiwa kwa mkataba huu ni moja ya nyenzo muhimu katika kufanya Bara la Afrika kuwa soko moja na nchi hizo kutekeleza juhudi za mtangamano wa kibiashara na uchumi ambazo Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika zimekwishaanzisha;

NA KWA KUWA madhumuni na misingi ya mkataba wa uanzishwaji wa eneo huru la biashara Afrika kama ilivyoainishwa kwenye kifungu cha 3 na cha 4 cha Mkataba huo ni pamoja na:-

(i) Kuwa na soko moja la bidhaa na huduma;

(ii) Kuwa na ushuru wa kusafiri kwa wafanyabiashara uhamishaji wa mitaji;

(iii) Kukuza biashara baina ya Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika kwa kuoanisha taratibu za kufanya biashara pamoja na kufunguliana masoko ya biashara;

(iv) Kuimarisha ushirikiano wa biashara na uwekezaji miongoni mwa nchi za Afrika;

(v) Kukuza na kujenga uwezo wa uchumi wa viwanda na uzalishaji Barani Afrika;

(vi) Kuchangia kufikia agenda 2063 (*The Africa we want*);

(vii) Kuongeza mchango wa Afrika kwenye soko la Dunia kwa asilimia 2.8 huku sekta za kilimo chakula na huduma zikiwa na nafasi kubwa zaidi ya ukuaji huo;

(viii) Kuongeza ufanisi kwa wafanyabiashara na viwanda na kusaidia mabadiliko ya kiuchumi kupitia upatikanaji wa soko na matumizi mazuri ya rasilimali za Afrika;

(ix) Kuondoa changamoto za nchi kuwa na wanachama katika zaidi ya eneo moja la kiuchumi na kuharakisha mtangamano;

(x) Kushirikiana kwenye uwekezaji miliki ubunifu na sera ya ushindani;

(xi) Kuharakisha mchakato wa kuwa na umoja wa forodha wa Afrika;

(xii) Kushirikiana kwenye maeneo yote ya biashara; na

(xiii) Kuanzisha mfumo wa kitaasisi kutekeleza na kusimamia Mkataba huu.

NA KWA KUWA kuridhiwa kwa Mkataba wa Eneo Huru la Biashara la Afrika kutatoa fursa kwa Tanzania kunufaika na mkataba huo kwa kusaidia:-

(i) Kupatikana kwa masoko mapya ya mazao ya kilimo na hivyo kuchochea uzalishaji wake nchini;

(ii) Kuimarika kwa mnyororo wa thamani wa mazao ya kilimo ambayo mengi yanahusisha wakulima wadogo wa mazao kama vile alizeti, pamba, karafuu, viungo, matunda na mbogamboga, kutokana na kuongezeka kwa soko la bidhaa ambazo zitazalishwa nchini;

(iii) Kuongezeka kwa uzalishaji kwa wakulima ajira na thamani ya mazao ya kilimo;

(iv) Kupatikana kwa soko kubwa la bidhaa na huduma lenye idadi ya watu takribani bilioni 1.2 ukilinganisha na idadi ya watu takribani milioni 522 katika nchi za *EAC* na *SADC*;

(v) Kuongezeka kwa tija na ubora kwa bidhaa na huduma za Tanzania kutokana na kuongezeka kwa ushindani na hivyo kupelekea kupungua kwa bei za bidhaa;

(vi) Kuimarisha ushirikiano wa kibiashara sambamba na kuviendeleza viwanda na wajasiriamali wadogo sana, wadogo na wakati;

(vii) Upatikanaji wa bidhaa za aina mbalimbali nchini; na

(viii) Uhalalishaji wa teknolojia kutoka nje ya nchi kutokana na uwekezaji utakaofanyika nchini.

KWA HIYO BASI kwa kuzingatia manufaa ambayo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itapata kutokana na mkataba huu, Bunge la Jamhuri ya Muungano katika Mkutano wake wa Nne na kwa mujibu wa masharti ya Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 1977, Bunge hili Tukufu linaazimia kuridhia Mkataba wa Uanzishaji wa Eneo Huru la Biashara (*Agreement Establishing the African Continent Free Trade Area – AFCFTA*).

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoka hoja.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara.

Sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira Mheshimiwa David Kihenzile, aje atoe maoni ya Kamati, karibu.

**MHE. DAVID M. KIHENZILE - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni taarifa ya maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu Azimio la Bunge Kuridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa Eneo Huru la Biashara (*Africa Agreement Establishing the African Continent Free Trade Area – AFCFTA*). (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru Mungu kwa kutujalia uhai, kuweza kufika siku ya leo kutokana na ufinyu wa muda, naomba taarifa hii yote kama inavyosomeka katika kitabu cha Kamati, iingie katika Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni 108(1) ikisomwa pamoja na kifungu cha 7(1)(b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2021, hoja ya Serikali kuhusu Azimio la Bunge Kuridhia Mkataba wa Eneo Huru la Biashara la Afrika (*Agreement Establishing the African Continent Free Trade Area – AFCFTA*), ililetwa mbele ya Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa ajili ya kupitia, kuchambua na hatimaye kulishauri Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 60(6)(b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu Mkataba wa Uanzishwaji wa Eneo Huru la Biashara la Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Nchi Mwanachama wa Umoja wa Afrika (*African Union - AU*) tangu tarehe 25 Mei, mwaka 1963. Umoja huu kupitia Mkutano wa Abuja ulizaliwa Mkataba wa Abuja yaani *Abuja Treaty*. Mkataba huu unaelekeza Kuanzisha kwa Eneo Huru la Biashara la Afrika (*African Continental Free Trade Area – AFCFTA*). Lengo la Mkataba huu ni kuweka ushirikiano wa kiuchumi baina ya Nchi za Afrika. Malengo mengine mahsusi ni pamoja na kuondoa au kulegeza masharti na vikwazo vya kikodi na visivyo vya kikodi katika biashara na huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo ya msingi yaliyozingatiwa na Kamati; ili kuiwezesha Bunge kutekeleza madaraka yake ipasavyo kwa mujibu wa Ibara 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Toleo la mwaka 1977 pamoja na marekebisho yake, Kamati ilizingatia mambo mbalimbali yaliyo muhimu katika kufanyia kazi hoja ya Serikali iliyo mezani leo. Mambo yaliyozingatiwa na Kamati ni pamoja na chimbuko la Mkataba, dhumuni na maudhui

ya Mkataba, faida na hasara za kuridhia Mkataba, pamoja na changamoto katika utekelezaji wa Mkataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, chimbuko la Mkataba huu ni katika kutekeleza ajenda ya 2063 ya Afrika Tunayoitaka (*Agenda 2063 The Africa We Want*), mpango ambapo miongoni mwa mikakati ya ajenda hiyo ni kuanzisha eneo huru la biashara kwa lengo la kuongeza mauzo ya bidhaa na huduma baina ya Nchi Wanachama hadi kufikia asilimia 52 ambapo kwa sasa mauzo hayo yapo chini ya asilimia 20.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhumuni la kuanzishwa Mkataba huu ni kuweka utaratibu wa pamoja wa Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika (*African Union*) unaolenga kuchochea uchumi wa biashara miongoni mwa Nchi Wanachama kwa kufunguliana masoko ya biashara ya bidhaa na huduma, kuondoleana ushuru wa forodha (*tariffs*) na kulegezeana masharti na taratibu nyingine zisizokuwa za kiushuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilijiridhisha kuwa, utekelezaji wa Mkataba huu haukinzani na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na sheria za nchi zinazohusiana na usimamizi wa biashara. Aidha, Kamati ilibaini faida na hasara zitokanazo na kuridhia Mkataba huu, kama vile:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilibainisha changamoto katika utekelezaji wa Mkataba. Vyote hivi vimeainishwa kwenye taarifa ya Kamati, naomba nisivisome kwa nia ya kuokoa muda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilijiridhisha pia kuhusu maudhui ya Mkataba wa *AFCFTA* kwa kupitia vifungu vya Mkataba huu. Baadhi ya vifungu muhimu katika Mkataba huu ni pamoja na: Ibara 3 kipengele cha 1-10 na Ibara ya 4 kipengele cha 1-7 ambavyo vinaeleza malengo ya jumla pamoja na malengo mahsusi ya Mkataba ambapo kimsingi yanalenga kuwa na soko moja la bidhaa na huduma kwa kuoanisha taratibu za kufanya biashara; kufunguliana masoko



ya biashara; pamoja na kuondoa vikwazo vya kikodi na visivyo vya kikodi miongoni mwa nchi wanachama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna fursa ya kujitoa katika Mkataba endapo Nchi Mwanachama itakutana na changamoto baada ya kuridhia na kuanza utekelezaji wa Mkataba. Ibara ya 27 ya Mkataba inatoa fursa hiyo isipokuwa jambo hilo linaweza kufanyika miaka mitano baada ya utekelezaji wa Mkataba kuanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Mkataba huu umekwisha anza na nchi zitakazojiunga zitalazimika kuingia na kuendelea pale walipofikia wengine. Kamati imejiridhisha kuwa bado tuna fursa ya kwenda sambamba na wenzetu kwa kuwa Ibara ya 28 - 29 ya Mkataba inatoa fursa ya kurejea Mkataba na kufanya maboresho pamoja na fursa kwa Nchi Wanachama kuwasilisha mapendekezo ya marekebisho ya Mkataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa Kamati:-

KWA KUWA Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi mwanachama wa Umoja wa Afrika *African Union AU* tangu 25 Mei, 1963, pamoja na baadhi ya itifaki zake

NA KWA KUWA eneo huru la biashara la Afrika ni fursa muhimu sana kwa Afrika kukuza ushirikiano wa pamoja kwa Waafrika kufanya biashara miongoni mwao na kuimarisha mikakati ya kuinua uchumi

NA KWA KUWA Tanzania kwa sasa inajielekeza katika kuhamasisha ujenzi wa viwanda hivyo eneo huru la biashara la Afrika ni fursa ya masoko ya bidhaa zetu.

HIVYO BASI Kamati inalishauri Bunge lako Tukufu kuliridha Mkataba wa Uanzishaji wa Eneo Huru la Biashara la Afrika (*Agreement Establishing African Continent Free Trade Area – AFCFTA*) kwa lengo la kujiweka katika nafasi ya kunufaika na Mkataba huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuridhia Mkataba huu, naomba nitoe maoni na mapendekezo ambayo Kamati imeona ni muhimu Serikali ikayazingatia kwa lengo la kuboresha utekelezaji wa Mkataba kama ifuatavyo:-

(i) Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa Mkataba kuna uwezekano mkubwa wa kupoteza ajira ya watu wetu hususani katika sekta ya uzalishaji viwandani, pia kuna uwezekano wa viwanda vilivyokua kupotea kabisa sababu ikiwa ni kushindwa kushindana katika soko kutokana na changamoto zilizopo katika mazingira ya uzalishaji nchini ikiwepo ukubwa wa gharama za uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali kutekeleza kwa ufanisi mpango wa kuboresha mfumo wa uhibitaji wa biashara nchini (*Blue print for regulator reform to improve business environment*) hususani katika kipengele cha mapitio ya kodi na tozo mbalimbali za uzalishaji, kuhakikisha zinaendana na washindani wenzetu na kwa lengo la kuziwezesha bidhaa zetu zitakapoingia sokoni kuweza kushindana. (*Makoff*)

(ii) Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 28 na 29 ya Mkataba inatoa fursa ya kufanya mapitio ya Mkataba kila baada ya miaka mitano pamoja na kutoa fursa kwa Nchi Wanachama kuwasilisha mapendekezo yake, sisi Tanzania tumejiwekea mikakati mbalimbali itakayoweza utekelezaji wa Mkataba huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali kutekeleza mikakati hii kikamilifu na kutumia kipindi hiki kabla ya awamu ya pili ya majadiliano ya Mkataba, kujifunza na kubainisha changamoto tutakazokumbana nazo kama nchi ili tuweze kushiriki vizuri katika majadiliano na kuhakikisha changamoto husika zinatatuliwa.

(iii) Mheshimiwa Naibu Spika, tunaingia kwenye soko ambalo ni gumu yaani *tricky* kidogo na wajasiriamali wetu wa kati na wadogo bado hawajapewa elimu juu ya fursa na changamoto zilizopo katika soko hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali kuweka nguvu katika kutoa elimu ya kuchangamkia fursa za masoko chapa (*branding*) na vifungashio (*packaging*) chapa ili bidhaa zao ziweze kutambulika na wasiweze kudhulumiwa bidhaa au hati miliki zao, lakini kuwa na vifungashio ili waweze kushindana na viwango vya soko.

(iv) Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Mkataba unatoa fursa kwa mwanachama kuangalia bidhaa ambazo anaweza kuzilinda asilimia saba ya bidhaa zinazoweza kulindwa kwa miaka 13, tangu kuridhia Mkataba na asilimia tatu zinaweza kuzuiliwa kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali kutumia fursa hii adhimu vizuri kuhakikisha inachagua bidhaa na huduma ambazo zinaweza kuathirika kama zisipolindwa. (*Makofi*)

(v) Mheshimiwa Naibu Spika, Mkataba una mpango kazi wa kukuza biashara *Boosting Intra-African Trade* miongoni mwa nchi za Afrika. Mpango kazi una maeneo saba ya kipaumbele ambayo ni sera ya biashara, uwezesaji biashara, uwezo wa uzalishaji, miundombinu inayosaidia biashara, mitaji ya biashara, taarifa za biashara pamoja na mtangamano wa masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali kujipanga vizuri kutekeleza mpango kazi huo kwa lengo la kujiweka katika nafasi ya kunufaika na matunda ya Mkataba. (*Makofi*)

(vi) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ifanye juhudi za kutosha katika kutoa elimu na msukumo kwa wafanyabiashara wa Tanzania ili waweze kuchangamkia fursa hususani katika eneo la biashara za kimataifa.

(vii) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ifanye tathmini ya utekelezaji wa Mikataba ya aina hii ambayo Tanzania tumekwisha ingia, kwa mfano, Jumuiya ya Afrika Mashariki na *SADC* ili kubaini changamoto zilizojitokeza wakati wa

utekelezaji wake na hivyo kujipanga vyema kabla ya kuanza kutekeleza Mkataba huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho; naomba nimshukuru Mheshimiwa Spika, nikushukuru wewe mwenyewe kwa uongozi wako mahiri na kunipa fursa ya kuwasilisha maoni haya ya Kamati. Niwashukuru pia Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuratibu na kusimamia shughuli za Bunge kwa umakini na umahiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inapenda kumshukuru Waziri wa Viwanda na Biashara Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo; Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Kigahe Exaud Silaoneka; Makatibu Wakuu pamoja na wataalam wote wa Wizara hii kwa ushirikiano walioutoa wakati wa kujadili Azimio hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa ushirikiano waliutoa wakati wa kupitia na kuchambua na hatimaye kuwasilisha maoni kuhusu Azimio hili mbele ya Bunge lako Tukufu. Orodha yao ni kama inavyosomeka hapa chini na kwa ruhusa yako naomba majina yao yaingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge (*Hansard*).

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Nenelewa Mwihambi *ndc* na Mkurugenzi wa Idara ya Kamati Bwana Athuman Hussien *ndc*, kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

Kwa namna ya kipekee, naomba niwashukuru Makatibu wa Kamati Bi. Zainabu Mkamba, Bi. Amina Salum; Mshauri wa Bunge wa Mambo ya Sheria, Prudence Rweyongeza; pamoja na msaidizi wa Kamati Bi. Mwimbe John kwa kuratibu vema shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kukamilisha taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono Azimio hili. (*Makofi*)

**DHANA KUHUSU AZIMIO LA KURIDHIA MKATABA WA  
UANZISHWAJI WA ENEO HURU LA BIASHARA LA AFRIKA  
(*Agreement Establishing African Continental Free Trade  
Area - AfCFTA*) KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 108 (1) ikisomwa pamoja na Kifungu cha 7(1) (b), cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za kudumu za Bunge toleo la Juni, 2021, hoja ya Serikali kuhusu Azimio la Bunge Kuridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa Eneo Huru la Biashara la Afrika (*Agreement establishing African Continental Free Trade Area - AfCFTA*), ililetwa mbele ya Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa ajili ya kulipitia, kulichambua na hatimaye kulishauri Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni 60(6)(b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda Biashara na Mazingira kuhusu Mkataba wa Uanzishwaji wa Eneo Huru la Biashara la Afrika.

**Mheshimiwa Spika**, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi Mwanachama wa Umoja wa Afrika (African Union-AU) tangu tarehe 25 Mei 1963. Umoja huu kupitia Mkutano wa Abuja ulizaliwa Mkataba wa Abuja (Abuja Treaty) Mkataba huu unaelekeza kuanzishwa kwa Eneo Huru la Biashara la Afrika (African Continental Free Trade Area- AfCFTA). Lengo la Mkataba huu ni kuweka ushirikiano wa kiuchumi baina ya nchi za Afrika. Malengo mengine mahsusi ni pamoja na kuondoa au kulegeza masharti/vikwazo vya kikodi na visivyokuwa vya kikodi katika biashara ya bidhaa na huduma.

**2.0 MAMBO YA MSINGI YALIYOZINGATIWA NA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika**, ili kuliwezesha Bunge kutekeleza madaraka yake ipasavyo kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, toleo la 1977 pamoja na marekebisho yake, Kamati ilizingatia mambo mbalimbali yaliyo muhimu katika kuifanyia kazi hoja ya Serikali

iliyo mezani leo. Mambo yaliyozingatiwa na Kamati ni pamoja Chimbuko la Mkataba, dhumuni na maudhui ya Mkataba, faida na hasara za kuridhia Mkataba pamoja na changamoto katika utekelezaji wa Mkataba.

**Mheshimiwa Spika**, chimbuko la Mkataba huu ni katika kutekeleza Ajenda ya 2063 ya Afrika tunayoitaka (Agenda 2063 The Africa we Want) ambapo miongoni mwa Mikakati ya Ajenda hiyo ni kuanzisha eneo Huru la Biashara kwa lengo la kuongeza mauzo ya bidhaa na huduma baina ya nchi wanachama hadi kufikia asilimia 52 ambapo kwa sasa mauzo hayo yapo chini ya asilimia 20.

**Mheshimiwa Spika**, dhumuni la kuanzishwa Mkataba huu ni kuweka utaratibu wa pamoja wa nchi wanachama wa Umoja wa Afrika (African Union-AU) unaolenga kuchochea uchumi na biashara miongoni mwa nchi wanachama kwa kufunguliana masoko ya biashara ya bidhaa na huduma, kuondoleana ushuru wa forodha (tariffs) na kulegezeana masharti na taratibu nyingine zisizokuwa za kiushuru.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilijiridhisha kuwa, utekelezaji wa Mkataba huu haukinzani na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Sheria za nchi zinazohusiana na usimamizi wa Biashara.

**Aidha**, Kamati ilijiridhisha juu ya faida zitakazopatikana kutokana na kuridhia Mkataba huu ambazo ni:-

i) Kupatikana kwa masoko mapya ya mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi na hivyo kuchochea ongezeko la ajira kupitia Sekta hizi;

ii) Kupatikana kwa soko kubwa la bidhaa na huduma lenye idadi ya watu takribani bilioni 1.2 waliopo Barani Afrika;

iii) Kuongezeka kwa tija na ubora kwa bidhaa na huduma za Tanzania kutokana na kuongezeka kwa ushindani utakaowalazimu wazalishaji kwenda na kasi kulingana na viwango vya soko;

iv) Upatikanaji wa bidhaa za aina mbalimbali (varieties) nchini; na

v) Uhawilishaji wa teknolojia kutoka nje ya nchi (technology transfer) kutokana na uwekezaji utakaofanyika nchini.

**Mheshimiwa Spika**, hasara zinazoweza kupatikana kutokana na kuridhia mkataba huu ni:-

i) Kupungua kwa mapato na kodi yatokanayo na ushuru wa forodha kwa bidhaa ambazo tutaziondolea ushuru;

ii) Uwezekano wa kupoteza ajira kwa baadhi ya sekta hususani sekta ya uzalishaji (Viwanda); na

iii) Uwezekano wa Tanzania kuwa mwagizaji zaidi wa bidhaa (unfavourable balance of trade) utakaosababishwa na ushindani wa biashara miongoni mwa nchi wanachama.

**Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa Mkataba wa Eneo Huru la Biashara la Afrika unaweza kuwa na changamoto zifuatazo:-

i) Ugumu wa kuzioanisha au kuzipatanisha chumi zilizotawanyika au tofauti za nchi za Afrika;

ii) Tofauti za ukubwa na viwango vya maendeleo ya kiuchumi inafanya ugumu katika kuhakiki mapato ya Nchi Wanachama;

iii) Nchi maskini zina changamoto ya kutengeneza ajira, kukuza sekta ya viwanda jambo ambalo linaleta tofauti za viwango vya mapato;

iv) Baadhi ya nchi zina miundombinu dhaifu, teknolojia duni itakayosababisha utekelezaji wa Mkataba kuwa mgumu;

v) Kuna uoga miongoni mwa Nchi Wanachama wa kupoteza utambulisho (identity) kutokana na mwingiliano wa watu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilijiridhisha pia kuhusu maudhui ya Mkataba wa AfCFTA kwa kupitia vifungu vya mkataba huo. Baadhi ya vifungu muhimu katika Mkataba huu ni pamoja na **Ibara ya 3 kipengele cha 1-10** na **Ibara ya 4 Kipengele cha 1-7** ambavyo vinaelezea Malengo ya jumla pamoja na Malengo Mahususi ya Mkataba ambayo kimsingi yanalenga kuwa na soko moja la bidhaa na huduma kwa kuoanisha taratibu za kufanya biashara, kufunguliana masoko ya biashara pamoja na kuondoa vikwazo vya kikodi na visivyokuwa vya kikodi miongoni mwa nchi wanachama.

**Mheshimiwa Spika**, kuna fursa ya kujitoa katika Mkataba endapo Nchi mwanachama itakutana na changamoto baada ya kuridhia na kuanza utetekelezaji wa mkataba, **Ibara ya 27** ya Mkataba inatoa fursa hiyo isipokuwa jambo hilo linaweza kufanyika miaka mitano baada ya utekelezaji wa Mkataba kuanza.

**Mheshimiwa Spika**, Utekelezaji wa Mkataba huu umekwisha anza na kwa nchi zitakazo jiunga zitalazimika kuingia na kuendelea pale walipofikia wengine, Kamati imejiridhisha kuwa bado tuna fursa ya kwenda sambamba na wenzetu kwa kuwa **Ibara ya 28 na 29** ya Mkataba inatoa fursa ya kurejea mkataba na kufanya maboresho pamoja na fursa kwa Nchi Wanachama kuwasilisha mapendekezo ya marekebisho ya Mkataba.

**Ibara ya 16- Machapisho (Publication)**, Ibara hiyo inaitaka nchi kutoa machapisho ya sheria, kanuni na taratibu, masuala yote ya utawala na kuyaweka wazi kwa umma ikiwa ni pamoja na makubaliano ya kimataifa ambayo yanahusu masuala ya kibiashara yaliyomo ndani ya mkataba wa AfCFTA. Ibara hii itatoa fursa kwa Umma kujua kinachoendelea katika soko hilo.

### 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi Mwanachama wa Umoja wa Afrika (African



Union-AU) tangu tarehe 25 Mei 1963 pamoja na baadhi ya Itifaki zake, na

**kwa kuwa**, Eneo huru la Biashara la Afrika ni fursa muhimu sana kwa Afrika kukuza ushirikiano wa pamoja kwa Waafrika kufanya biashara miongoni mwao na kuimarisha mikakati ya kuinua uchumi; na

**kwa kuwa**, Tanzania kwa sasa inajielekeza katika kuhamasisha ujenzi wa Viwanda hivyo Eneo huru la Biashara la Afrika ni fursa ya masoko ya bidhaa zetu.

**Hivyo basi**, Kamati inalishauri Bunge lako Tukufu kuridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa Eneo Huru la Biashara la Afrika (Agreement establishing African Continental Free Trade Area - AfCFTA), kwa lengo la kujiweka katika nafasi ya kunufaika na Mkataba huu.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kuridhia Mkataba huu, naomba nitoe maoni na mapendekezo ambayo Kamati imeona ni muhimu Serikali ikayazingatia kwa lengo la kuboresha utekelezaji wa Mkataba huu kama ifuatavyo:-

i) Katika utekelezaji wa Mkataba kuna uwezekano mkubwa wa kupoteza ajira ya watu wetu hususani katika Sekta ya uzalishaji Viwandani, pia kuna uwezekana wa viwanda vinavyokua kupotea kabisa sababu ikiwa ni kushindwa kushindana katika soko kutokana na changamoto zilizopo katika mazingira ya uzalishaji nchini ikiwepo ukubwa wa gharama za uzalishaji. Kamati inaishauri Serikali kutekeleza kwa ufanisi Mpango wa kuboresha mfumo wa udhibiti wa biashara nchini (*Blueprint for Regulatory Reform to Improve Business Environment*) hususani kipengele cha kufanya mapitio ya kodi na tozo mbalimbali za uzalishaji kuhakikisha zinaendana na washindani wenzetu na kwa lengo la kuziwezesha bidhaa zetu zitakapoingia sokoni kuweza kushindana;

ii) **Ibara ya 28 na 29** ya Mkataba inatoa fursa ya kufanya mapitio ya Mkataba kila baada ya Miaka Mitano (5) pamoja

na kutoa fursa kwa nchi mwanachama kuwasilisha mapendekezo yake. Sisi Tanzania tumejiwekea mikakati mbalimbali itakakayo wezesha utekelezaji wa Mkataba huu. Kamati inaishauri Serikali kutekeleza mikakati hii kiukamilifu na kutumia kipindi hiki kabla ya Awamu ya Pili ya Majadiliano ya Mkataba kujifunza na kubainisha changamoto tutakazo kumbana nazo kama nchi ili tuweze kushiriki vizuri katika majadiliano na kuhakikisha changamoto husika zinatatuliwa;

iii) Tunaingia kwenye soko ambalo ni gumu (*tricky*) kidogo na wajasiriamali wetu wa kati na wadogo bado hawajapewa elimu juu ya fursa na changamoto zilizopo katika soko hili. Kamati inaishauri Serikali kuweka nguvu katika kutoa elimu hususani ya kuchangamkia fursa za masoko, chapa (*branding*) na Vifungashio (*packaging*), Chapa ili bidhaa zao ziweze kutambulika na wasiweze kudhulumiwa bidhaa/hatimiliki zao lakini Vifungashio ili waweze kushindana na viwango vya Soko.

iv) Utekelezaji wa Mkataba unatoa fursa kwa mwanachama kuangalia bidhaa ambazo inaweza kuzilinda, asilimia 7 bidhaa zinaweza kulindwa kwa miaka 13 tangu kuridhia mkataba na asilimia 3 inaweza kuzuiwa kabisa. Kamati inaishauri Serikali kutumia fursa hii adhimu vizuri kuhakikisha inachagua bidhaa na huduma ambazo zinaweza kuathirika kama zisipolindwa;

v) Mkataba una Mpango Kazi wa Kukuza Biashara (Boosting Intra-Africa Trade) miongoni mwa nchi za Afrika, Mpango kazi una maeneo saba ya kipaumbele ambayo ni Sera ya Biashara, Uwezeshaji Biashara, Uwezo wa Uzalishaji, Miundombinu inayosaidia Biashara, Mitaji ya Biashara, Taarifa za Biashara, pamoja na Mtangamano wa Masoko. Kamati inaishauri Serikali kujipanga vizuri kuutekeleza Mpangokazi huo kwa lengo la kujiweka katika nafasi ya kunufaika na Matunda ya Mkataba.

vi) Serikali ifanye juhudi za kutosha zifanyike katika kutoa elimu na msukumo kwa wafanyabiashara wa Tanzania ili waweze

kuchangamkia fursa hususani katika eneo la biashara za kimataifa;

vii) Serikali ifanye tathmini ya utekelezaji wa mikataba ya aina hii ambayo Tanzania tumekwisha ingia mfano EAC na SADC ili kubaini changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wake na hivyo kujipanga vyema kabla ya kuanza kutekelza mkataba huu.

#### 4.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, naomba nikushukuru sana wewe binafsi kwa uongozi wako mahiri na kwa kunipa ruhusa ya kuwasilisha maoni haya ya Kamati. Nimshukuru pia Mheshimiwa Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuratibu na kusimamia shughuli za Bunge kwa umakini na umahiri.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapenda kumshukuru Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe. Prof. Kitila Mkumbo(Mb), Naibu Waziri wake Mhe. Kigahe Exaud Silaoneka (Mb), Makatibu Wakuu, pamoja na wataalamu wote wa Wizara hii kwa ushirikiano walioutoa wakati wa kujadili Azimio hili.

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee kabisa, napenda kuwashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa ushirikiano walioutoa wakati wa kupitia, kuchambua na hatimaye kuwasilisha maoni kuhusu Azimio hili mbele ya Bunge lako tukufu. Orodha yao ni kama inavyosomeka hapa chini na kwa ruhusa yako naomba majina yao yaingie kwenye kumbukumbu Rasmi za Bunge (*Hansard*).

- |                                       |                |
|---------------------------------------|----------------|
| 1. Mhe. David Mwakiposa Kihenzile, Mb | - Mwenyekiti   |
| 2. Mhe. Eric James Shigongo, Mb       | - M/Mwenyekiti |
| 3. Mhe. Usonge Hamad Juma, Mb         | - Mjumbe       |
| 4. Mhe. Martha Nehemia Gwau, Mb       | - Mjumbe       |
| 5. Mhe. Cecil David Mwambe, Mb        | - Mjumbe       |
| 6. Mhe. Eng. Ezra John Chiwelesa, Mb  | - Mjumbe       |
| 7. Mhe. Lucy John Sabu, Mb            | - Mjumbe       |
| 8. Mhe. Hawa Chakoma Mchafu, Mb       | - Mjumbe       |

9. Mhe. Daimu Iddi Mpakate, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Haji Makame Mlenge, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Issa Ally Mchungahela, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Daudi Silanga Njalu, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Askofu Josephat Mathias Gwajima, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Boniphace Mwita Getere, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Maryam Omar Said, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Deodatus Philip Mwanyika, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Zulfa Mmaka Omary, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Jumanne Kibera Kishimba, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Nancy Hassan Nyarusi, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Salim Hassan Turkey Toufiq, Mb - Mjumbe
21. Mhe. Shamsia Azizi Mtamba, Mb - Mjumbe
22. Mhe. Antipas Zeno Mgungusi, Mb - Mjumbe
23. Mhe. Dkt. Charles Stephen Kimei, Mb - Mjumbe
24. Mhe. Dkt. James Kimea Alfred, Mb - Mjumbe
25. Mhe. Kavejuru Eliadory Felix, Mb - Mjumbe
26. Mhe. Irene Alex Ndyamkama, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, napenda pia kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Nanelwa Mwiambwe, (*ndc*) na Mkurugenzi wa Idara ya Kamati Bw. Athumani Hussein, (*ndc*) kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikukamilifu. Kwa namna ya pekee naomba kuwashukuru Makatibu wa Kamati Bi. Zainabu Mkamba na Bi. Amina Salum, Mshauri wa Bunge wa Mambo ya Sheria Ndg. Prudence Rweyongeza pamoja na Msaidizi wa Kamati Bi Mwimbe John kwa kuratibu vema shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kukamilisha taarifa hii kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono Azimio hili.

David Mwakiposa Kihenzile, (Mb)

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA**

9 Septemba, 2021

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira. Waheshimiwa Wabunge sasa kwa sababu tumeshapata maelezo yake kutoka kwa Mheshimiwa Waziri na sasa mapendekezo ya Kamati ninayo majina hapa ya Wabunge mbalimbali ambao wanahitaji kuchangia kwenye hoja hii, tutaanza na Mheshimiwa Ezra John Chiwelesa, atafuatiwa na Mheshimiwa Cecil David Mwambe na Mheshimiwa Deodatus Phillip Mwanyika ajiandae.

**MHE. ENG. EZRA J. CHWELESA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji katika Azimio la Uanzishwaji wa Eneo Huru la Biashara la Afrika. Pia naomba ku-*declare interest*, mimi ni Mbunge wa Kamati hii ya Viwanda, Biashara na Mazingira, kwa hiyo nitachangia maoni yangu binafsi nikijaribu kukazia kwenye yale ambayo yamewasilishwa na Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba vile vile niimpongeze Waziri na niimpongeze Serikali kwa kuchukua hatua hii muhimu ya kuungana na nchi nyingine 41 za Afrika ambazo tayari zilisharidhia Azimio hili na tayari zenyewe zinaendelea. Hii ni *decision* ya kishujaa kwa sababu nchi hii ni kubwa, sasa wenzetu wanapokuwa wamefanya jambo la kuendelea, halafu sisi tukabaki nyuma, kwangu niliona ni kama kitu kilikuwa kinaturudisha nyuma kidogo. Kwa hiyo, niimpongeze Serikali kwa hatua hii muhimu, lakini niseme yapo maeneo ambayo nimeyaona na nilipenda zaidi kuyaongelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani tumemaliza *discussion* ya mambo ya mahindi hapa, ni kitu ambacho nimejiandaa kuongea hasa masuala ya kilimo, maana tunayo fursa ya kufanya biashara hasa kwenye mazao ya kilimo, lakini nadhani yameongelewa mengi sana hapa, kwa hiyo nisingependa niingie sana huko. Hata hivyo, kwenye *research* zangu ambazo nilikuwa nimezifanya kwa siku mbili hizi wakati najiandaa, nilijaribu kuona eneo la tija, kwa sababu kilimo chetu tunapokwenda kuingia sasa katika ushindani

mkubwa wa takribani nchi 42 au 41 za Afrika zile ambazo zimeshaingia, ni lazima tujaribu kuangalia sisi tumejipangaje hasa kwenye *issue* ya tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa tunalima sawa, tunafanya shughuli zetu sawa, lakini ile *yield* tunachokipata labda kutoka kwenye heka moja unachokipata *comparing* na wenzetu ambacho wanapata tumekuwa tuko nyuma sana. Sasa ukija ukaangalia *cost of production*, kwetu inapokuwa kubwa zaidi na tunaingia kwenye ushindani huu mkubwa, wenzetu watatulazimisha tushushe bei ya mazao ili waweze kuza hapa au na sisi tutakapojaribu kwenda kuuza nje itakuja kuwa shida kidogo. Kwa hiyo, naomba tujikite zaidi kwenye suala hili kwa sababu nilikuwa naangalia *average production* katika tani moja ya mahindi, kwa mfano, kwa Tanzania, heka moja ya mahindi tumekuwa tunapata karibu gunia sita za kilo mia moja, mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ukija ukaangalia kwa wenzetu kwa mfano Zambia, kwa sababu tunaongelea ukanda huu wa kusini ndio unaolima mahindi sana, kwa Zambia ni *double*, tunaongea kwamba kwa hekta sio heka, kwa hekta moja kwa Tanzania ni 1.5 *tons* wakati kwa Zambia ni *three tons* kwa *same hector*. Ukija ukaangalia kwa South Africa inaenda karibu *six*. Sasa hawa ni wenzetu ambao ndio tunaoenda kushindana nao kwenye hili soko hasa uzalishaji wa mahindi. Sasa tukijaribu kuangalia *competition* yetu hasa kwenye bei itakuja kuwa ndogo zaidi, kwa sababu wenzetu watalima kidogo watawuna mengi. Wakishamaliza kuvuna mengi tunaingia kwenye soko moja la kushindana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo unakuja kukuta mbolea aliyoiweka kila kitu alichokiweka kwenye kuandaa shamba ni gharama zile zile sawa na wewe, lakini yeye amevuna magunia mengi zaidi, kwa hiyo atakuwa na uhuru zaidi wa kuuza kwa bei ya chini zaidi. Kwa hiyo hili jambo ningepomba tuliangalie ili tunavyokwenda kwenye ushindani kesho na kesho kutwa soko letu lisipotee, tuhakikishe kwamba hata na Wizara ya Kilimo inatusaidia tuweze kupata mazao mazuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine kikubwa liko suala la haya mazao ya *GMO*, hatuwezi kwenda mbali na dunia inapoelekea. Leo tunaingia kwenye ushindani, wenzetu wanalima pamba, tumekuwa tunasikia hapa Kanda ya Ziwa, watu wapo wanalima pamba, lakini pamba ambayo wenzetu leo wanalima ambapo wameshakwenda kwenye *GMO technology* ni tofauti. Yeye atalima heka moja, hapo unaongelea labda kwenye heka moja utavuna labda tani tano au tani 10, mwenzako labda yuko zaidi ya mara mbili kwa sababu wako kwenye *GMO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nilikuwa naomba kipindi tunaingia kwenye ushindani, kwa sababu nchi nyingine zimesha-*advance* kwenye teknolojia hii, Serikali ijaribu kuangalia kwamba teknolojia ya *GMO* bado tuna wasiwasi, tunajua labda ni *genetic modified*, tuna wasiwasi bado, lakini kwenye mazao ambayo siyo *consumables* kama vyakula, mazao yale ambayo tunaenda kushindana na wenzetu kama pamba na vitu vingine hivi vya kuuza kule, hebu tujaribu kuona kama tunaweza tuka-*adapt* hiyo teknolojia, tuanze kuruhusu baadhi ya vitu tukatumia teknolojia ya *GMO*. Kesi kubwa hapa ni kuwafanya Watanzania wanaofanya kilimo, kilimo chao kiwe cha tija, kiweze kuwaletea majawabu ambayo watawafanya wapate pesa kwenye *rotation* yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwenye suala la masoko, tuna hakika kwamba sisi tuna mifugo hapa, tuna maziwa na uvuvi. Kwa hiyo, kwa sehemu kubwa mkataba huu utaenda kusaidia zaidi vijana wa Kitanzania na hasa Watanzania kuweza ku-*embark* sasa kwenda kuuza katika nchi za jirani na hatimaye tuweze kujipatia kipato kizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo habari ya viwanda. Nadhani sasa hili ni soko ambalo tumekuwa tuna-*trade* labda sisi wenyewe na watu wa *East Africa*, hatuzidi watu milioni 200. Leo hii tunaingia kwenye soko la zaidi ya watu bilioni 1.2 iko fursa kubwa zaidi ya kuweza ku-*trade* na wenzetu, lakini ni lazima Serikali tuweke mguu chini; maana siku hizi vijana wanasema tuweke mguu chini. Maana ya kuweka mguu

chini ni nini? Lazima ifikie hatua tujue tunaingia kwenye biashara. Kama tunaingia kwenye biashara, tufanye *politics* lakini huku tukijua kwamba tunaenda kwenye biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, biashara ni ushindani. *The moment* umefungua, watamwagika Wanaigeria hapa, watamwagika Wakenya hapa; sasa siyo kesho umefungulia, halafu keshokutwa unanza kulalamika. Tutakuwa na miaka mitano ya kufanya *changes*, lakini hamtawafukuza kwa sababu watakuwa wamesha-*invest*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachoomba, kesi kubwa ambayo tumekuwa tunaipata upande wa Serikali, ni lazima tuhakikishe tunawa-*fever* hawa watu wanaofanyabiashara hapa. Tusione mfanyabiashara kama adui. Hiki ndicho kitu ambacho naomba zaidi upande wa Serikali ituangalie. Kodi na tozo zimekuwa nyingi mno kwenye biashara. Hatutaweza kushindana na wenzetu kama kodi na tozo zinaenda kuwa nyingi kiasi hicho. Kwa hiyo, hivi ni vitu ambavyo lazima tujaribu kuangalia. Tunapoingia kwenye uhuru wa soko hili la Afrika, kwa sababu ni *market* tunayoifungua, una wateja wengi, ukubali kushusha bei, kuondoa baadhi ya tozo, kuzalisha kwa wingi zaidi, kuuza kwa wingi zaidi, ndiyo tutakapopata faida, kuliko kuzalisha kidogo, ukataka kuuza kwa bei kubwa kwa sababu mna tozo nyingi zaidi, hatimaye ukajikuta kwamba umekwama na wenzetu ndiyo wakaanza kuingiza hapo, kwa sababu wao watakuwa wako *free*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilichokuwa naomba kwa upande wa Serikali, tuliangalie sana hili. Wafanyabiashara tusiwaone kama maadui, tuwaone kama *partners*. Ni lazima kwa upande wetu, hasa Serikali yetu ya Tanzania, Wizara ya Viwanda na Biashara muwe tayari kuwa-*support* wafanyabiashara wa Kitanzania, pale watakapotaka kwenda nje, watakapotaka kubaki hapa, waone kwamba Serikali iko nyuma yao. Kwa sababu tunavyoingia kwenye hili soko, wenzetu lazima Serikali zao zitakuwa zinawa-*support*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninao mfano hapa nilikuwa najaribu kupitia, kuna tangazo la *NEMC* walilitoa tarehe 7,



*this one here*, nimelitoa kwenye *Citizen* leo, linasema, “ *NEMC hits Lake Oil with 3.3 billion Fine*” ya vituo 66 vya mafuta. Sasa Waziri wa Viwanda na Biashara uko hapa, *Lake Oil* wana vituo 66 nchi hii. Leo *NEMC* anawatangazia kwamba anawapiga faini ya shilingi bilioni 3.3; huyu ni mfanyabiashara ambaye yuko hapa ame-*invest* kwenye vituo vyote hivyo, anampiga faini ya shilingi bilioni 3.3, *over sudden* tu anamwambia ndani ya siku 14 alipe. Kesi ni nini? Ni kwamba amefanya vituo vyake hivyo bila kufanya *Environmental Impact Assessment*. Unajuliza, mpaka mtu anafungua vituo 66, Serikali ilikuwa wapi? *NEMC* walikuwa wapi? Au kuna kitu gani ambacho walielewana na *NEMC*, sasa leo kimeshindikana hapo katikati, wanawageuzia kibao? *This is the very big shame!* (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ukiongelea vituo 66, Serikali itapoteza fedha kiasi gani? Yule mtu akisema leo hana, ikaamuliwa vifungwe, Serikali itapoteza pesa kiasi gani? Ajira ngapi za Watanzania zitapotea na vilevile ni *scandal*. Kwa hiyo, nilikuwa naomba, vitu kama hivi, kama kunakuwa na *cases* kama hizi; sasa leo unavyotumbia *Lake Oil* hawana hiyo *Environmental Impact Assessment* mnawafungia, vituo vingine waliokuwa wanalipa ambao wamefuata taratibu kihalali, wenyewe mliwafunguliaje? Yaani huyu mtu mpaka anajenga vituo 66 alikuwa anajificha wapi mpaka vikamilike 66 ugundue leo? Hivi ni vitu vidogo tu ambavyo baadaye vinam-*discourage* mtu.

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ezra Chiwelesa kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Ngassa.

## T A A R I F A

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpa taarifa mzungumzaji; ili uweze kipata kibali cha kujenga Kituo cha Mafuta, lazima uwe na *certificate* kutoka *NEMC*, ipelekwe Ewura, Ewura ndiyo

wakupe kibali. Ili upate kibali cha *NEMC*, ni lazima uwe umesajili kile Kituo cha Mafuta uweze kufanya hiyo *Environment Impact Assessment*. Maana yake, anachokiongea Mheshimiwa pale, kutakuwa kuna shida kule ambayo ndiyo imeleta hili tatizo kubwa. Kwa hiyo, hata Serikali waweze kuliangalia. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ezra Chiwelesa, unapokea taarifa hiyo?

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea. Hili ni jambo moja tu ambalo nimesema kwamba ni *discouragement* upande wa biashara. Ndiyo maana nikasema, Wizara ya Viwanda na Biashara na hasa upande wa Serikali, tuangalie; tunapoingia kwenye ushindani mkubwa namna hii tunakuja kuleta *giants* hapa, tutaleta *giants* kwa sababu sisi *advantage* tuliyonayo hapa, lazima wenzetu watakuja ku-*invest* tu hapa kwa sababu tuna ardhi nzuri, tuna vitu vingi, tuko kwenye ukanda huu wa bahari, lazima tutapata watu wa kuja ku-*invest* hapa. Ila kipindi wale *investors* tunajaribu kuwavuta, ni lazima tujaribu kuangalia kwamba vitu vidogo na vya kukwaza kama hivi visiweze kutuharibia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono azimio. Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Sasa Waheshimiwa Wabunge kwa sababu muda wetu mwingine tulitumia kwenye hoja nzito kabisa ya mahindi, na wachangiaji hapa ni wengi, wachangiaji wanaofuata watachangia kwa dakika tano. Mheshimiwa Cecil David Mwambe, atafatiwa na Mheshimiwa Deodatus Phillip Mwanyika na Mheshimiwa Judith Salvio Kapinga, ajiandae.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia. Kama ambavyo mtangulizi wangu amesema Mheshimiwa Eng. Ezra, nami pia ni Mjumbe wa Kamati ya Viwanda na Biashara. Tumetumia muda hasa kupitia huu Mkataba na

mapendekezo yaliyoletwa mbele yetu na Serikali na pia tulipata nafasi ya kuwaona wadau mbalimbali wakiwemo *TCCIA* na *CTI* tumesikia pia maoni yao na baadaye tulikutana na maoni ya mwavuli wa watu fulani walioungana, inaitwa *Trade Investment Coalition (TIC)* juu ya Azimio la Bunge la kuridhia Mkataba na Uanzishwaji wa Eneo Huru la Biashara Afrika ndiyo ambao tunajadli hapa sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mchango wao waliouleta kwenye Kamati ungeingia kwenye *Hansard* kama pia sehemu ya mchango wangu ili kuweza kuboresha zaidi na watu waweze kujifunza baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba Waheshimiwa Wabunge waridhie huu mkataba lakini lazima tuuridhie kwa tahadhari. Kwa sababu Tanzania tumekuwa na *tendency* kidogo wakati fulani ya kujilizaliza au kulalamika kwenye mambo ambayo sisi wenyewe labda hatuna nia nzuri ya kuyafanyia utafiti ili tuweze kuona tunakwenda wapi? Naomba radhi sana Waheshimiwa Wabunge waliochangia hapa kwenye hili swali linalohusiana na suala la mahindi na ndugu yangu pale ametumia mfano huo huo, na mimi naomba nitumie mfano huu ili kuweza kujenga hoja yangu vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunasema *NFRA* wanatakiwa wakanunue mahindi, halafu wayahifadhi na yaende kutumika labda wakati wa majanga. Pia tunatamani wafanyabiashara wa nje nao waje wanunue mahindi yetu Tanzania. Sasa swali ambalo sisi kama Watanzania tuna haja ya kujiuliza, mahindi yetu yana ubora sawa na mahindi yanayolimwa Kenya? Kwa nini Wakenya wasi-*saturate* kwanza *market* yao halafu wakaja kuchukua kwetu kiasi kidogo kwenda kujazilizia kwa sababu ya tofauti ya ubora?

Mheshimiwa Naibu Spika, hili liko wazi, tulifanya semina na ndugu yangu Mheshimiwa *Engineer* Ezra hapa alisema kidogo suala la *GMOs*; mpaka sasa watu wanaotumia kilimo cha kisasa au kutumia *GMO* ili kuweza kupata mazao bora, ni wachache sana Tanzania, kitu ambacho kinatusababisha

tushindwe kuingia vizuri kwenye soko bora kwa sababu ya ubora wa mbegu hata tunazozalisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku moja jaribu kufanya utafiti, chukua mahindi ya Tanzania halafu chukua mahindi ya Zambia, yaweke yote Mezani. Kuna kipimo wanachotumia, ni kama kanyundo fulani kadogo ili kuweza kuangalia ubora wa ile *grain*. Hindi la Tanzania ukiligonga linatawanyika, lakini ukichukua hindi la Zambia ukiligonga, litakatika vipande vine, vitano au sita. Ndiyo kipimo wanachokitumia, kwa hiyo, mwisho wa siku wanasema mahindi yetu hayana ubora kwa sababu watapata takataka nyingi zaidi kuliko ambavyo unaweza ukapata unga ulio bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninachotaka kusema ni kwamba tunaingia kwenye ushindani wa soko; na katika ushindani huu, pale ndani kuna sheria nyingi. Kwa mfano, Kifungu Na. 39 kinasema kinataka kulinda viwanda vidogo vidogo vya ndani. Sasa unavilinda viwanda vya ndani ambavyo vinatumia malighafi ambazo siyo bora sana ukilinganisha na nje ambako tunategemea ndiyo sehemu utakakokwenda kuuza kama wao wanavyokuja kuuza kwetu, kama ambavyo sasa hivi tumekuwa tukilalamika labda tumevamiwa na soko la China au tunavamiwa labda na soko la jirani hapo Kenya. Kwa hiyo, lazima tuangalie.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa namwomba sana Mheshimiwa Waziri kwamba pamoja na kutaka kuridhia Mkataba huu, lakini lazima tukatoe elimu ya kutosha kwa Watanzania kwamba sasa hivi tunakwenda kwenye mashindano ya kibiashara na tunaongezewa mkataba mwingine mpya. Kwa hiyo, kama hatujaweza kwenda vizuri, kwa mfano, kwenye Mkataba wa Afrika Mashariki, tumekuwa hapa kila mara tunasema tunaona *labor mobility*, tunaona na masuala ya *movement of labor*; Wakenya wanapokuja Tanzania kwenye *hospitality businesses* unafurahia zaidi huduma kuliko ambavyo sisi tunaokwenda kutoa kule kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, pamoja na maboresho yote, nakushukuru kwa kunipa nafasi, lakini

tuwatake Watanzania tuendeleo kujifunza ili tuweze kutoa kilicho bora. Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Sasa una karatasi hapo ambayo uliomba iingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge kama mchango wako, lakini umesema mchango huo ulipelekwa kwenye Kamati. Kwa hiyo, utakuwa umeingizwa kule kwenye Kamati badala ya hapa, kwa sababu hapa hatujausia. Kwa hiyo, sitakuwa najua ni kitu gani kilichoingia kwenye Taarifa Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Deodatus Phillip Mwanyika, atafuatiwa na Mheshimiwa Judith Salvio Kapinga na Mheshimiwa Eric James Shigongo ajiandae.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwenye hoja iliyo mbele yetu ya Kuridhia Mkataba wa Eneo Huru la Afrika. Napenda kuanza kwa kusema kwamba Mkataba huu tunaelewa kabisa umeridhiwa na baadhi ya nchi na nchi hizo ziko katika eneo letu la Afrika Mashariki. Hata hivyo kuchelewa kwa Tanzania kuridhia mkataba huu kumeleta hisia kwamba pengine wafanyabiashara wa Tanzania wanaogopa au wana uoga. Napenda kukudhihirishia, wafanyabiashara wa Tanzania hawana uoga wa kuingia kwenye ushindani, wafanyabiashara wa Tanzania wanaamini ushindani ndiyo utakaoboresha biashara zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa na nafasi ya kuwa Mjumbe wa Baraza la Biashara la Tanzania nikiwakilisha sekta binafsi katika nafasi yangu ya huko nyuma. Tatizo kubwa la wafanyabiashara wa Tanzania ni kuhakikishiwa kwamba kutakuwa na ushindani ambao upo *level* au uko sawa au una usawa, Waingereza wanaita *level playing ground*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hilo naomba niwashauri Wabunge kwamba wafanyabiashara wetu wanaiona hii ni fursa, nao ndio watakaokwenda kwenye soko hili. Wafanyabiashara/sekta binafsi ndio watakaokwenda kwenye soko hili na tuna kila sababu ya kuwasaidia na kuwa-

*support.* Nao wanachotaka siyo Serikali iwape fedha, Serikali iendelee kuboresha mazingira ya biashara. Tumeisema kwenye Kamati kwamba Serikali iendelee kuboresha mazingira ya biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami napenda kusema kwenye hili, Serikali ina *forum* ya kuongea na wafanyabiashara *on almost quarterly basis*. Tunaomba sana *forum* hii itumike vizuri ili kuweza kujua matatizo ya wafanyabiashara wa Tanzania kila wakati ambapo yanajitokeza, isiwe inangojewa mpaka malalamiko yanafika mbali au yanakuwa makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan hapa kwa juhudi zake kubwa sana za kuliweka hili jambo wazi na kuwaambia Watendaji ndani ya Serikali na kuonyesha mwelekeo wa nchi yetu kwenye masuala yote ya uwekezaji pamoja na kutoa kauli ambazo sasa zinatabirika katika Jumuiya ya Wafanyabiashara. Jambo hili ni zuri kwa nchi yetu, jambo hili ni zuri kwa wafanyabiashara wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ni la muhimu sana ili tuweze kufanikiwa kwenye suala hili ni kuhakikisha tunakwenda kwenye ushindani. Ushindani ni suala la bei na ubora. Sasa kwenye ubora, kwa kiasi kikubwa ni suala la mwekezaji mwenyewe au mfanyabiashara. Serikali kazi yake ni kuhakikisha kwamba *standards* zinakuwa *met*. Kuna suala la bei. Kwenye bei wafanyabiashara wetu lazima tuwasaidie. Nasi msaada wetu kama nchi au kama Serikali ni kuhakikisha kwamba tunawapunguzia gharama ambazo siyo za lazima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzangu wameliongea, kuna gharama nyingi ambazo siyo za lazima; nyingi tunasema ni kama tozo, lakini kuna gharama nyingine. Kwa mfano, ukichukua mkataba unaohusiana na masuala ya *electronic stamp*, tumeliongea sana hili hapa Bungeni. Gharama ya mkataba ule ni kubwa mno. Wenzetu watakaokuwa

wanazalisha vitu hivyo na kuvileta katika soko letu, pengine hawana hiyo gharama au kama wanayo ni ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nasi tuliangalie. Kwa mfano, *TBL* wanatumia dola milioni tisa kwa mwaka kwa kuweka hizo *stamp* tu. Hiyo gharama ni kubwa sana, nayo inakwenda kwenye masuala mengine vilevile. Tuangalie pia utaratibu mzima wa wafanyabiashara kuhakikisha kwamba tunaweza kuwarudishia kile ambacho wanadai kama *VAT*. Ni jambo la muhimu sana. Wengi tunashindwa kuelewa kwamba mtaji wa mfanyabiashara siku zote unahesabiwa kwa shilingi. Anapokuwa anadai Serikali marejesho na yanachukua muda mrefu, inampunguzia mtaji wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo napenda niliseme, naomba sana Serikali ifanye uchambuzi vizuri. Najua ndani ya mkataba huu unatoa nafasi ya kuhakikisha kuna maeneo ambayo tunadhani kwamba bado hatujafikia uwezo wa ku-*compete* au pengine tuna-*comparative advantage*. Serikali iyachambue vizuri. Nitatoa mfano, kuna maeneo ya nguo tumeambiwa kwamba haya yatabakia kuwa yetu, lakini kuna maeneo mengine uchambuzi ufanyike na hasa maeneo yale ambayo *SMEs* zetu zitashiriki. Iko haja ya kuona namna gani tutawasaidia ili waweze kuingia kwenye soko hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hii hoja na naomba sana Wabunge wenzangu tuiptishe kwa nguvu zote. Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Judith Salvio Kapinga, atafuatiwa na Mheshimiwa Eric James Shigongo na Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, ajiandae.

**MHE. JUDITH S. KAPINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwanza nianze kwa kuipongeza Wizara kwa kuja na mkataba huu, kwa kuwa naamini kwamba mkataba huu una manufaa makubwa sana kwa nchi yetu ya Tanzania na nchi nyingine za Bara la Afrika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kusema kwamba uanzishwaji wa maeneo huru ya biashara siyo jambo jipya duniani, ni jambo ambalo limeanza miaka mingi nyuma tangu miaka ya 1950; na mfano mzuri ni *European Economic Community* ambayo ilianza mwaka 1957 na baadaye kubadilishwa jina pale ambapo *European Union* iliundwa mwaka 1993. Kwa hiyo, inawezekana kwa sisi kama Bara la Afrika tumechelewa kutokana na changamoto mbalimbali na kuja na mkataba huu 2019 kwa sababu ni wazi kabisa sisi kama Afrika tumekuwa wahanga wa masuala ya ukoloni. Kwa hiyo, inawezekana tulichelewa kama Bara. hata hivyo, changamoto tulizonazo na ambazo tulikuwa nazo kama bara haziwezi kutunyima fursa ya sisi kama waafrika kuja na mbinu mbalimbali za kutuina kiuchumi ikiwemo kuwa na soko huru la biashara kuelekea kutimiza malengo yetu ya ajenda 2063. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuchangia kwamba mojawapo ya hasara au changamoto ambazo tunaweza kuzipata kutokana na kuridhia mkataba huu ambao tumeelezwa na Serikali, moja ni kupungua kwa mapato ya kodi yanayotokana na ushuru wa forodha kwa bidhaa ambazo zitaondolewa kodi kwa takriban shilingi bilioni 41 ndani ya miaka 10, yaani wastani wa shilingi bilioni 4.1 kwa mwaka. Pia mojawapo ya changamoto nyingine ambazo tumeambiwa ni uwezekano wa kupoteza ajira kwa baadhi ya sekta hususan sekta za uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachelea kusema kwamba changamoto hizi zinafikirisha ukilinganisha kwamba sisi kama Taifa bado tuna changamoto ya ajira, lakini niseme kwamba kuna baadhi ya masuala ambayo kama Taifa tukifanyia kazi, changamoto hizi ambazo tunaweza tukazipata kutokana na kuridhia mkataba huu, tunaweza tukazipunguza kwa kiasi kikubwa sana na njia mojawapo ni kuendelea kujenga uchumi shindani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uchumi shindani una *variables* mbalimbali, lakini sisi kama taifa tukiendelea kujijenga tunaweza tukapunguza changamoto hizi kwa



sababu tayari tuliishaanza. Mojawapo ya masuala ambayo tunaweza tukayajenga ili kuweza kuongeza uchumi shindani mojawapo ni kuendelea kuwa na miundombinu imara na wezeshi lakini vilevile kuendelea kuwa na taasisi imara, kuendelea kuwa na elimu ya juu inayotoa vijana ama watu ambao wanaweza kupambana kwenye soko la ajira la biashara, kuenzi mabadiliko ya teknolojia, kuenzi mabadiliko ya ubunifu na kuwa na masoko yenye tija. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naamini iwapo kama Taifa tutafanyia kazi masuala haya na kuwa na uchumi shindani, tunaweza tuka-*penetrate* kwenye masoko na vilevile athari ambazo tumeambiwa tunaweza tukawa nazo kama Taifa, tunaweza tukazipunguza ikiwemo suala la ajira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano ukiangalia ripoti ya takwimu za biashara za benki yetu kuu kwenye kanda za kiuchumi kati ya Tanzania na nchi nyingine za jirani kwa mfano tukianza biashara za bidhaa kati ya Tanzania na nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, Tanzania tumekuwa tukifanya vizuri. Kwa mfano ukiangalia takwimu za miaka saba nyuma yaani kuanzia 2013 mpaka 2020 kwenye kuuza bidhaa tumekuwa tukifanya vizuri kwa sababu tumekuwa tukipanda, tulianza mwaka 2013 na US dola milioni 419, lakini mwaka jana 2020 tumeweza kupanda mpaka US dola milioni 812.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwenye kuuza bidhaa tumeweza ku- *contained* soko letu na kulinda soko letu kwa sababu tulianza na US dola milioni 394, lakini kwa mwaka jana tumeweza ku-*contained* na kushuka mpaka dola milioni 324. Kwa hiyo, inaonyesha kabisa sisi kama Watanzania tunafursa kwenye soko hili kwa sababu bidhaa zetu kwa uuzaji wa nje tumekuwa tukifanya vizuri sana na tumeweza kulinda soko letu la ndani kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwenye masuala ya ajira, ukweli ni kwamba ukipunguza kodi kwenye bidhaa unafanya makampuni yaweze kuzalisha zaidi, lakini *generally* hii ina-*apply* kote, ina-*apply* tu kwenye nchi ambazo

gharama zao za maisha ni ndogo, ya kwamba kama gharama za maisha husika ni ndogo inamaana bidhaa zao zinaweza zika- *penetrate* kwenye masoko ya nchi nyingine kuliko nchi ambazo gharama za maisha ni kubwa mno.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaweza tukachukulia mfano, wamarekani wakati wamejiunga na mkataba wa *North America* na *free trade area*, wamarekani viwanda vyao vingi sana vilikosa ajira kwa sababu Mexico ilikuwa na gharama za chini ndogo kuliko Marekani, lakini sisi kama Tanzania *cost of living* inakuwa *approximated* kwa dola 0.32. ina maana tunafanya vizuri kuliko nchi nyingine za Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaweza tukauza zaidi ni kuimarisha tu baadhi ya masuala ya kiuchumi ili tuweze kushindana zaidi na kufanya vizuri katika soko. Na hapa sasa inabidi tufanyie masuala ambayo ni ya msingi sana ikiwemo kujiongeza kiji-*digital*, yaani huduma ambazo zinatolewa kiji-*digital* sasa tunafanya kazi kwa uharaka na ziweze kuwa *reliable*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilizungumzia suala la taasisi imara liweze kutuvusha lazima taasisi zetu ziweze kubadilika.

**NAIBU SPIKA:** Dakika moja Mheshimiwa kengele imeshangongwa imeshagongwa.

**MHE. JUDITH S. KAPINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia kwa mfano taasisi za kiserikali kama *AFTC* lazima zitoke kwenye kufanya kazi kwa mazoea ya *finically* na ziende kwenye biashara za mitandao kwenda kulinda walaji kwenye mitandao. Sasa hivi ukiwauliza hawana hata mkakati wa kulinda walaji kwenye mtandao ambapo biashara kubwa imeamia huko. kwa hiyo, mimi sina shaka kama Taifa tutafanya vizuri tukiendelea kufanya kazi tu kwa ajili ya *variable* sisi ambazo tukazifanyisha ukiwa na uchumi shindani basi tunaweza tukafanya kazi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Eric James Shigongo, atafuatiwa na Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, Mheshimiwa Felix Kavejuru ajiandae.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa mchango wangu katika kupitisha Azimio hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ni-*declare interest* kwamba ni makamu mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda na Biashara na nilikuwepo kwenye mjadala mrefu sana kuhusiana na mkataba huu. Cha kwanza niliposoma mkataba huu mambo mawili yalinikuta la kwanza nililingia hofu, hofu yangu ya kwanza kabisa ilikuwa ni kwamba mkataba huu utaua viwanda vyetu, mkataba huu utaondoa ajira zetu, huo ni upande mmoja, lakini kuna upande mwingine mzuri sana wa mkataba huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ambao ulikuwa ni kwamba Afrika sasa inakwenda kufanya *integration*, Afrika inaanza kuuziana Afrika kwa Afrika, Afrika inaanza kufanya biashara Afrika kwa Afrika jambo ambalo huko nyuma lilikuwa halifanyiki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipofika hapo nikaamua kuchagua upande wa uzuri wa mkataba, nikaamua kabisa kuachana na hofu ambayo ilikuwa imenikamata na hivi sasa nimesimama hapa kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wote kwa ujumla wetu tuweze kuridhia Azimio hili nchi yetu ikaweze kuingia katika mkataba huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wale waliowahi kusoma kitabu cha Walter Rodney *how Europe underdeveloped Africa*, alisema Walter Rodney ukitaka kuichezesha Afrika isababishie tu iwe na *disintegration* yaani tu tuwe hatuna ushirikiano na wakoloni walifanya jambo hili kwa umakini kabisa na wakatugawa wakaweka mipaka ardhini baadaye mipaka hiyo ikaamia kwenye vichwa vyetu. Kwa hiyo, tunatembea hapa Watanzania nikivuka tu pale Namanga kuingia upande wa Kenya hofu inaniingia. Na

wakati narudi nyumbani nikivuka Namanga nikiingia upande wa Arusha kiburi kinaanza. Kwa hiyo, kuna mipaka tunayo ndani ya vichwa vyetu hiyo ndiyo itakayotucheleweshwa kuweza kusonga mbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mkataba huu au Azimio hili linakwenda kuondosha *barrier* zote ambazo zilikuwepo ili sasa Afrika ifanye biashara Afrika kwa Afrika, ukijaribu kuangalia *data* ambazo zipo Afrika kwa Afrika kwenye *Intra business*, biashara ya ndani ya Afrika kwa Afrika ni asilimia 17, lakini ukiangalia Asia ni asilimia 69, ukiangalia *North America* ni asilimia 31. Kwa hiyo, ninachojifunza hapa ni kwamba tunafanya hii biashara sisi kwa sisi kidogo sana hatuwezi kukua mpaka tuweze kuondoa *barriers*, tuanze ku-*trade* kati ya Taifa na Taifa. Hapa tunazungumza tuna mahindi si ajabu kuna nchi haina mahindi, inahitaji mahindi lakini unaweza ukashangaa ikaagiza mahindi Brazil badala kuagiza mahindi Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naunga mkono Mkataba huu na ninaomba kabisa Waheshimiwa Wabunge wote turidhie kwa nia moja tuachane na hofu, tukubali kwenda kujifunza tukiwa tunafanya kuna *learning* unapokuwa unafanya na kuna kujifunza kwanza ndiyo ufanye. Ninawaomba tukubali nchi yetu iingie tukajifunze tukiwa tunatenda, tutarekebisha huko ndani kwa ndani, tutabadilisha mikakati tukiwa tunavyozidi kwenda tuta-*change strategies*, hatimaye tutaweza kuweza tutaweza kufanya vizuri hatutaweza kupata faidia kwenye mwaka wa kwanza au mwaka wa pili lakini nina uhakika kabisa baada ya muda si mrefu tutafanya vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la muhimu sana ni *capacity building* ni lazima nchi yetu iwawezeshe wafanyabiashara wetu. Ni lazima wapewe mikopo yenye riba ndogo, ni lazima tutambue ya kwamba Nigeria uchumi wake ni mkubwa sana kuliko uchumi wetu sisi. Ukinipambanisha mimi na Okwonko sasa hivi kuna uwezekano wa ku-*fail*, lakini kama nimewezeshwa na nchi yangu kama nchi yangu inadhamira ya kweli *political will* kwamba tunawapeleka

hawa watu vitani wakapambane tutahakikisha kwamba wanashinda lazima tutashinda vita hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *South Africa* ilifanya hivyo wakapatikana wakina Patrick Motsepe ni wakati wa nchi yetu tutengeneze mabilionea wengine wapya. Tumekuwa na mabilionea wale wale miaka hiyo tangu tukiwa watoto ni wakati sasa tuanze kusikia majina ya Aweso, tuanze kusikia majina ya kina Kigwangalla wakiwa mabilionea tumechoshwa na majina yale yale kila mwaka. Kwa mkataba huu nina uhakika wakiwezesha vijana wa kitanzania tutasikia majina mapya, kuna uwezekano kabisa wa kutengeneza wakina MO wengine, kutengeneza wanakina Bakharessa wengine kwa mkataba kama huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu niseme kwamba *tariff* za kodi; *tariff* za kodi tusipoziangalia vizuri zitatuumiza. Nitatoa mfano mmoja hai nilitembelea kiwanda kimoja cha mapipa pale Mbagala, Mhindi anatengeneza mapipa mazuri tu lakini anashindwa kuuza Kenya, kwa sababu gani anashindwa kuuza kenya Kodi, Wakenya wanapoagiza *sheet* za chuma pale kwao hawatozwi kodi kwa sababu wananunua kwenye COMESA, wananunua Egypt. kwa sababu wako ndani ya COMESA hawalipi kodi asilimia 10, lakini yeye anapoagiza hapa analipa *ten percent* na Wakenya wakitengeneza mapipa yao pale kwa sababu ni EAC wanauza soko la Tanzania. Kwa hiyo matokeo yake mapipa yale yanakuwa chini kwa asilimia 10 upande wa bei lakini mapipa ya Mbagala yanakuwa juu, hawezi kuuza Kenya, hawezi kuuza hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kodi zetu tuzitazame vizuri wenzetu tunapotoa *tariff* ya kodi wanaziangalia hivi Tanzania *import duty* wameweka shilingi ngapi, wao wanapunguza kidogo ili waweze kushinda kwenye soko/wawe *competitive* kwenye soko. Ombi langu *tariff* za kodi tuwe *smart* kwenye eneo hilo, tuzipitie tuziangalie na tuwe *smart* kuwashinda wenzetu. Kwa nini mtu anatoka hapa anaenda kununua masharti Kampala anakuja kuyauza Dar es Salaam anapata faida, hapo kuna tatizo kwenye *types* za kodi kama mnataka

bidhaa zetu ziweze kushinda kwenye soko tuziangalie *types* za kodi na ziweze kupunguzwa kushindana na wenzetu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono Azimio. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Shigongo nikawa natafakari hao uliowataja mbona kama ni tayari wapo kwenye hiyo orodha ya mabilionea lakini wazo nzuri. Waheshimiwa Wabunge Kanuni ya 68 inatukumbusha kutokuzungumzia jambo ambalo lina maslahi binafsi ya kifedha siyo ya ujumbe wa Kamati, siyo kuwa mjumbe wa kamati unasema nataka kusema ninamaslahi, huna maslahi binafsi ya kifedha kwa wewe kuwa mjumbe wa kamati, tuzingatia hilo maana tunapoteza muda wetu sisi wenyewe. (Makofi)

Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, atafutaiwa na Mheshimiwa Felix Kavejuru, Mheshimiwa Charles Mwijage ajiandae.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Awali ya yote kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema aliyeniweka hai na kuja kushiriki katika mjadala huu wa *African Continental Free Trade Area*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni *declare* kwamba mradi huu au itifaki hii ni itifaki nzuri ambayo itatuwezesha kufanikisha. Kwa hiyo, kwa mwanzo kabisa lazima niunge mkono hoja kwa sababu tunaenda kuliendea soko na takribani watu bilioni 1.2 ni watu wengi sana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini, baada ya kusema hivyo msimamo wangu mwingine wakutaka kuistua Serikali usichukulie kuwa kama nataka kuipinga Serikali au kutaka kuipinga hoja hii. Lakini ichukuliwe kwamba ni chachu ya kuisukuma Serikali kujielekeza katika kutatua changamoto muhimu hasa hizi za biashara ambazo zitatuwezesha sisi kunufaika sana na mkataba huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiniuliza kwamba, je? tumechelewa kwenye mkataba huu kama ambavyo watu wengine walivyojaribu kudai, ninaweza nikasema hapana hatujachelewa na hata wale waliokataa kusaini mwanzo mkataba huu walifanya jambo zuri kabisa kwa sababu gani? Kwa sababu Serikali iliweza kujiangalia kama Taifa na kuanza kutafakari njia bora za kuangalia changamoto ambazo zilitufanya tukaukataa mkakataba huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia sisi kama nchi tulijitutumua mbele za nchi nyingine duniani na kujionyesha kwamba sisi ni watu huru, lakini tunauwezo wa kujiamulia maamuzi yetu ambayo yenye maslahi na nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ukiniuliza kwamba, je, tuendeleo kukataa mkataba huu? Nitakuambia hapana, hatuwezi kufanya hivyo kwa sababu mazingira ya sasa hivi yamekuwa ni mazingira bora kuliko yale mazingira ya zamani. Lakini hali kadhalika pia mkataba huu una *content* nyingi sana ambazo ni *positive* ambazo kama Serikali itafanya jitihada kwa umakini kabisa kufuatilia maslahi gani ambayo tunayoyapata humu, tutanufaika na huu mkataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa utendaji wa Serikali nianze kusema kwamba sina shaka kwa sababu kuna mambo mengi sana ambayo nafikiri kwa kukataa ule mkataba mwanzo kusaini Serikali ilienda ikajielekeza katika mazingira mazuri yakuanza kutafuta changamoto kama vile nilivyosema zile zilizosababisha watu kuukataa ule mkataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano ukiangalia, Serikali ilienda ikaweka mazingira mazuri ya mtandao wa barabara, imeweka mtandao mkubwa kabisa wa barabara ambao ni chachu kubwa katika suala la kiuchumi hasa hasa katika uzalishaji kule kwa mfano vijijini kwenye mazao ya kilimo. Mtandao wa barabara umekuwa ni muhimu sana naweza nikaishukuru sana Serikali na kuipongeza na kwamba iongeze bidii, iongeze zaidi ya hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia ukiangalia Serikali iliifanya kazi kubwa pia ya kutengeneza mtandao wa nishati mpaka sasa hivi tunazungumzia kwamba nchi nzima tumekuwa na umeme takribani kila kijiji kasoro vijiji vichache. Hii pia ni sehemu kubwa sana Serikali ambayo iliifanya kazi hii kwa kuangalia changamoto zile ambazo zilipelekea sisi kuukataa ule mkataba kwa mara ya kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kwa namna moja au nyingine hatuna sababu ya sisi kujiona *inferior* kwa kukataa huu mkataba mwanzo haizidi haipungui ni kwamba tumepata nguvu sasa ya kuweza kupambana zaidi na wenzetu kwa sababu tayari tushapata vitu wezeshi vitakavyosaidia sisi kutusukuma kwenda mbele zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna kitu ambacho najaribu kutaka kusisitiza kwa Serikali pamoja na mazuri yote ambayo nimeyasema hapa na mengi ambayo nakusudia kuyafanya ukiangalia kuna mambo mengi sana kwa mfano, ujenzi wa *Stigler's gauge*, lakini kuna pia ujenzi wa *EPZ*, lakini kuna mambo mengi sana yaani kama vile vyanzo vya nishati nakadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado tunaona kabisa kwamba Serikali ina nia nzuri, lakini pia nataka kuisisitiza Serikali kwamba iongeze kasi katika utekelezaji wa hizi adhima zake au nia zake, kwa sababu gani? Zenyewe ndizo zitakazotufanya sisi tuweze kuonekana mbele za wenzetu kwamba ni watu tupo *superb* na tuweze kuchangamkia hizi fursa tunazokwenda kuziendea vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu ambacho nilichotaka kusisitiza hapo ni kuiomba Serikali ifanye jitihada ya makusudi kabisa kuweka *sub-seeds* kwenye mazao au biashara mkakati vitu ambavyo tunaona sisi tunafanya vizuri zaidi basi tujaribu kuweka *sub-seeds* kuwezesha sisi kupata bei nzuri au kuwa na gharama ndogo ya uzalishaji, lakini wakati huo huo tukiweza kuweka bei nzuri ukilinganisha na bei za wenzetu.



Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine pia ni kuweza kutumia kodi au *tariff* vizuri katika maeneo ambayo tunaona kwamba tupo tunakaribia kupoteza, sehemu ambapo tukiona kwamba hapa tunakaribia kupoteza tunatakiwa tuweke *tariff* kwa ajili ya ku-*protect*. Kwa mfano, hizi *product* zetu tunazozalisha, lakini pia ku-*protect* wazalishaji wetu wa ndani na wafanyabiashara wa ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo tukijaribu kufanya hivyo nafikiri sisi tutakuwa ni miongoni mwa watu wenye manufaa makubwa sana na huu mkataba kwa sababu hiyo inajieleza mpaka sasa hivi ukizingatia tupo katika ndani ya watu au nchi kumi ambazo ni bora sasa hivi Afrika katika masuala ya kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo naomba kuunga mkono hoja asilimia mia moja. Ahsante. (*Makoff*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Felix Kavejuru atafuatiwa na Mheshimiwa Charles John Mwijage, Mheshimiwa Aida Joseph Khenan, ajiandae.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikushukuru kwa upekee kabisa kwa kupata nafasi hii ili niweze kuchangia hoja kwenye Azimio la uanzishwaji wa Soko Huru katika Bara la Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, azimio hili ni azimio zuri sana, linafaida nyingi sana, ningepomba kila Mbunge aweze kuridhia mkataba huu, una faida nyingi sana. Kwanza ukiangalia nchi yetu kijiografia Tanzania mahali ilipo tumebahatika kuwa sehemu nzuri kijiografia, tuna maliasili, tuna ardhi nzuri. Kwa hiyo ni suala tu la kujipanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuridhia mkataba huu utafungua masoko mapya kwa mazao yetu ya kilimo. Tunachangamoto ya mazao kama tulivyoona kwenye mahindi, lakini litafungua masoko mapya kwa mazao mengine madogo madogo kama alizeti na choroko.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia mkataba huu utaimarisha mnyororo wa thamani utakuwepo na nini na ushindani, ushindani wa uzalishaji ambao tunaenda kushindana katika soko hilo huru utaboresha ubora wa mazao yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo mimi ninashauri sana, ninashauri Serikali ijipange kwa kuelimisha kwa kutoa elimu kwa mapana na kwa marefu kwa wazalishaji wetu. Kama ni kilimo sasa twende kwenye kilimo cha biashara, tulime kilimo cha kibiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile taasisi za kifedha zijipange kupunguza riba na ziwe tayari kusaidia wazalishaji kwa maana ya wakulima na wajasiriamali wapate mitaji ili tuweze kusogea kwenda kwenye masoko ya mbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa takwimu ambazo zipo sasa hivi nchi ambayo ina uchumi mzuri kwenye hili soko ambalo tunaenda kwenye wale wanachama ambao wamekwisha saini ambao ni 42. Nchi ambayo ina uchumi mzuri sasa hivi ni Nigeria ikifuatiwa na Egypt, ikifuatiwa na Afrika Kusini, sisi hatupo mbali sana tupo kama namba 10.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo sisi tuna nafasi nzuri kama Serikali ikijipanga ikahakikisha, ikaboresha miundo mbinu ili wakulima wetu huko wanako zalisha barabara zikafika, kukawepo na gharama ndogo za usafirishaji wa mazao yetu tutafaidika zaidi, zaidi na zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo azimio hili ni zuri, litatusogeza mbele, litaenda kuzalisha mabilionea wengi katika Tanzania yetu na litaenda kuleta mabadiliko makubwa sana katika sekta mbalimbali; sekta ya kilimo na biashara pia kutokana na ushindani utakaotokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuunga hoja Azimio hili la Mkataba wa Uundwaji wa Soko Huru la Afrika. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Charles John Mwijage, atafuatiwa na Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana ajiandae.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia fursa ya kuchangia hoja iliyopo Mezani. Awali ya yote na mimi naunga mkono Azimio la Kuridhia huu Mkataba, kazi ambayo na mimi nimeshiriki sana katika kufikisha maamuzi ya Wakuu wa nchi za Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianzie kwa madhumuni (*objectives*) ya makubaliano haya. Lengo kubwa ni kutengeneza soko kubwa la Afrika. Wataalam wanasema kufika mwaka 2050 nchi zitakazokuwa na watu wengi ni China, India na *African Continent*. Kwa hiyo soko ni wingi wa watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunao watu bilioni moja na milioni mia mbili, kama walivyosema Waheshimiwa Wabunge, lakini kwa takwimu za mwaka 2017 Afrika inaagiza nje chakula chenye thamani ya dola bilioni thelathini na tano. Lakini kufika mwaka 2025 keshokutwa tu, Afrika itakuwa inaagiza nje ya Afrika chakula chenye thamani ya dola bilioni 110, yaani pesa zenye thamani kuliko *GDP* ya nchi hii leo na itakapofika mwaka 2025. Kwa hiyo, kwa vigezo hivyo sisi hatuna kisingizo chochote, lazima tujiunge na soko kubwa na soko la Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia misingi (*principles*) katika *Article No. 5* ya hii *Africa Continental Free Trade* kuna suala la nipe nikupe (*reciprocity*). Kipengele namba 9, watu watakaokuwa wameelewana watauziana wao. Ni kama leo tunahangaika na mahindi lakini ukienda upande wa Nakonde, upande wa Malawi, malori yamejazana Malawi yanasafirisha mahindi kwenda *Southern Sudan*, sisi hapa tunatafuta soko tunakosa. Kumbe sasa tutakapokuwa sisi hatukujunga – na ninawaomba tujiunge, hakuna sababu ya kuogopa nitaiielezea, tujiunge ili wale watakaokubaliana wasije wakatengeneza kundi la waliokubaliana na sisi Tanzania tukabaki tunalia. Kama

nilivyoeleze *population* inakuja Afrika, sasa unajitoa Afrika uwe mgeni wa nani? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka kulizungumza ni kwamba hatuna sababu ya kuogopa. Tumejipanga kwa kipindi kirefu na hususan kwa kipindi cha miaka 15. Mpango wa kwanza wa miaka mitano tuliondoa vikwazo na ndiyo ikaja kuzaa *blueprint* katika mpango wa pili wa miaka mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, imeelezwa wazi mambo ya vikwazo, sasa vikwazo tunavijua, viondoke. Ninataka nirudie tena, Tanzania haina ukosevu wa wajasiriamali. Tanzania haina shida ya sekta binafsi, sekta binafsi ya Tanzania imefungwa minyororo, ina vikwazo vya kutosha. Kwa hiyo, ni suala la kuwaondolea vikwazo kama ilivyoandikwa kwenye *Blueprint Regulatory Reform*.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niseme *Blueprint Regulatory Reform* ni mkakati wa kujitokeza (*emergent strategy*), ni kwamba watu walibishana wakabishana vikwazo vipo au havipo, wataalam wakakaa chini wakaweza kuonesha vikwazo ambavyo wote tunavikiri kama alivyosema Mbunge wa Biharamulo, kwamba unaona vikwazo hivi. Yaani mtu anakupa faini kwamba nipe lita kumi za damu, nitazitoa wapi lita kumi za damu halafu niendeleo kuishi? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisikiliza maelekezo ya Wabunge katika Bunge Bajeti la liliopita, Wabunge msiwe na wasiwasi kwamba tutashindwa kushindana. Kama maelezo ya Mheshimiwa Spika ya kufanya mageuzi makubwa katika sekta za kiuzalishaji yatazingatiwa tutakwenda kwenye soko la Afrika tukiwa kifua mbele. *Transformation ya productive sectors* tunaiweza, hakuna jambo geni. Hatutaki kurudia, hatutaki kubaki kwenye idadi ya ng'ombe wengi, hapana, tunataka kuwa na ng'ombe wengi watakaoweza kutoa maziwa mengi na nyama nyingi na ngozi ya kutengeneza viatu vizuri vya *moccasins*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo Watanzania msiwe na wasiwasi. Lakini mjadala wa sekta ya elimu wa kutengeneza elimu inayotufaa, siyo tuitakayo, ni mjadala unaopaswa kwenda haraka sana kama alivyozungumza Mbunge wa Viti Maalum kutoka huko Mbinga, lazima tuwe na watu wabunifu na wanaoweza kuchezea teknolojia. Lazima watoto wetu, siyo kwamba waende darasani, waende darasani wapate maarifa na weledi kwa sababu sasa wanakwenda kushindana katika nchi inayoitwa Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatutengenezi watu wa kushindana Mbeya, Songea na Kagera, tunaandaa vijana wetu tutakuwa tukipigiwa simu sisi tukiwa wazee nyumbani, mtoto anakupigia simu akiwa *Ivory Coast*, anatoka hapo anakwenda Cairo.

Mheshimiwa Naibu Spika, na hili la *Continental Africa* linakuja. Juzi Misri wameamua wata-*pioneer* wao kujenga reli kutoka Cairo kwenda mpaka Durban, itapita Dodoma na Mbeya. Hiyo ndiyo Afrika inayokuja, ukiwa na wasiwasi utaachwa unazubaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, naunga mkono Azimio hili. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana, Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga ajiandae.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi. Na mimi naunga mkono hoja ya kuridhia Mkataba huu wa Uanzishwaji wa Eneo Huru la Biashara la Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania siyo kisiwa na sisi tuko ndani ya Afrika, na mimi pia najivunia kuzaliwa Afrika. Pamoja na maamuzi ambayo Serikali imefanya kupitia Wizara, tunawapongeza sana kwa maamuzi haya, lakini mimi nitakuwa na mambo machache.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuridhia ni jambo moja lakini lazima tujipe muda wa kufanya tafiti za kina, faida ambazo tutakwenda kunufaika kama nchi lakini Watanzania ni namna gani tumewaandaa ambapo wanaweza kunufaika na maazimio haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ni kwamba kama tunatambua tunaingia kwenye ushindani lazima tujue mshindani wetu ana nini na sisi tuna nini. Lazima kuandaa bidhaa ambazo tunaamini ndiyo hitaji kwenye biashara hiyo. Kwa mazingira hayo hayo tumekuwa na kasumba fulani tukiamini kwamba watu fulani ndio wanastahili kuwa wafanyabiashara. Kupitia hii nafasi lazima tuanze kuwandaa Watanzania ambao wanaweza wakawa ma-supplier kwenda kwenye nchi nyingine za Afrika, hiyo itakuwa ni faida mojawapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumzia ushindani lazima kuna vitu vinavyoitwa vikwazo. Lazima tutengeneze mazingira rafiki kwa uwekezaji pamoja na wafanyabiashara ambao tunaamini kwetu tutakuwa tumeitumia hiyo fursa kama nchi. Pamoja na kuangalia ni kipi ambacho tunaweza tukatumia kama fursa baada ya kuridhia, lazima pia tujenge uaminifu. Tusipojenga uaminifu pia ni changamoto. Uaminifu wetu utatengeneza mazingira rafiki ya watu waliopo nje kuja kwetu na sisi kujijengea mazingira ambayo hata mtu ambaye alikuwa hajawahi kufikiri kupitia tu ile sifa ya mtu mwingine ambaye aliona uaminifu wetu tunaendelea kutangaza Taifa letu na kunufaika na hayo maazimio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la teknolojia lazima tuone kama hilo jambo ni kipaumbele. Lazima tuachane na biashara za mazoea tuanze kuwandaa Watanzania kutumia teknolojia kuweza kunufaika kwa kuangalia huu mkataba ambao tunaamini utalisaidia Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri pia tuangalie sera zetu ni rafiki kiasi gani. Mara nyingi tumekuwa na mabadiliko sana ya hizi sera, lazima tuwe na sera ambazo hazitawapa

shida hizo nchi wanachama ambazo tumeamua kuingia nazo kwenye Bara la Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuzungumza yote ambayo Wabunge wenzangu wamezungumza hatuwezi kukwepa biashara mtandao, lazima tujijenge kwa kuanza kuwaandaa vijana wetu, kabla ya kufikia hayo malengo ambayo tumejiwekea, lazima tuanze kuwaandaa leo. Wafanyabiashara waliopo ni wajibu wa Serikali kuona namna bora ya kuwatengenezea *network* lakini kuna wale ambao lazima tuwaandae sisi, tutengeneze mabilionea wengine, tusifikiri walewale ambao walikuwepo kuanzia mwaka 2010, leo tuanze kutengeneza wengine ili na sisi tuweze kunufaika kwenye huu mkataba ambao tumekwenda kuridhia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mazingira yote ni lazima tujue sisi kwa upande wa kilimo ni mazao gani ambayo yana *pick* kwa Bara la Afrika kutoka Tanzania, lazima tuwe tunatumia hiyo nafasi. Tusisubiri baadaye tukiwa tumechelewa, ni nini kinahitajika tunaanza sisi kwanza kuitumia hiyo fursa. Leo tunahangaika na mahindi, kama mahindi hayalipi lazima muwe mmeshaangalia mapema, kama siyo mahindi ni kipi mbadala? Tunakiandaa mapema kwa ajili ya kutumia hiyo nafasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwa leo ni kupongeza na kuendelea kuwasisitiza kwamba lazima tuendeleo kufanya tafiti za kina, faida ni zipi, hasara ni zipi. Lakini kuna mengine yanaweza yakawa kama *challenge* kwetu ikawa kama fursa lazima tuitumie kwa sababu tunaamini itasaidia Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana, atafuatiwa na Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Mheshimiwa Godwin Kunambi ajiandae.

**MHE. BALOZI DKT. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nimesimama kwa heshima zote na taadhima kuunga mkono hoja iliyopo mbele yetu ya Kuridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa Eneo Huru la Biashara la Afrika. Naunga mkono na ninaomba nianze na historia. Naipongeza sana Serikali, Waziri, Naibu Waziri kwa kutuletea mkataba huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika historia nakumbuka Mwalimu Nyerere ilikuwa ni ndoto yake kuona Afrika ni moja, masuala ya *Pan-Africanism*. Hivi sasa chini ya *AU* tumefanikiwa kufanya masuala mengi, kwa mfano tayari tunalo Bunge la *Pan-African*, pamoja na Bunge hili Mwalimu alitamani sana Afrika iwe moja. Alikuwa anashirikiana na Mzee Mandela na akina Mzee Mugabe na wengine wote. Kwa kweli eneo hili liligawanyishwa na wakoloni. Wakoloni ndiyo walikuja wakafanya kutugawanyisha ili kututawala, lakini sasa wakati umefika wa kuwa na eneo huru la biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu *Europe* wamefanikiwa, *European Union*, mpaka wamekuwa na fedha inayofanana inaitwa *Euro* kutumia ndani ya *Europe*, hawatunii tena pesa za nchi nyingine. Sasa sisi tumefanikiwa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kama ni eneo la kujifunza, wengi wamesema, tulikubaliana kuwa na *Common Market*, *Custom Union*, *Monetary Union*, *ultimately* tulisema tunakwenda kwenye kitu kinaitwa *Political Federation*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo *common market* hii ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ni eneo zuri la sisi kulielewa vizuri kwa sababu tunapokwenda sasa kwenye eneo huru hapa tunazungumzia masuala ya mahindi, huku ndiko maeneo hasa ya kupeleka mahindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ziko nchi ndani ya Afrika wao kutwa ni kupigana, mara wamefanya mageuzi, mara wanapigana, sisi ni kisiwa cha amani. Kwa hiyo hiyo kwetu sisi tayari ni *strength*. Na upande ule sasa wana hizo *weaknesses* ni eneo sasa la kujikita na kuelewa ni namna gani sasa tunatchukua hizo fursa.



Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania tuna watu takribani milioni 60 na sasa tunakwenda kwenye soko la takribani bilioni 1.2, mazao tunazalisha ya kutosha, mambo kama mahindi. Sasa lazima tuone kuwalinda wakulima wetu, wazalishaji wetu. Kwa mfano, tunataka tuagize labda mafuta ya alizetu, lazima tujulize haya yaliyopo mafuta ya kula tumenunua kiasi cha kutosha? Tunaweka *threshold* kwamba kabla ya kuagiza ngano au mafuta, lazima ya kwetu tuwe tumechukua *a hundred percent* ndipo sasa tunaweza tukaagiza vitu vya nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia, na kwa kweli imekuja wakati muafaka, tuchape kazi. Soko hili la pamoja ni letu na bidhaa za kupeleka kwa kweli tunazo. Sisi ni wazalishaji wazuri sana wa mazao (*raw materials*), sasa tuone namna gani ya kuongeza thamani ili mwananchi anapoenda hata dukani akiona chai ya Tanzania na chai ya nje, akiona bidhaa nyingine aseme hapana sasa nachukua hii ya Tanzania. Wakati mwafaka sasa wa kulinda, kuangalia kodi zote ambazo siyo za lazima tuziondoshe (*non-tariff barriers*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nimesimama kwa heshima zote kuunga mkono, ilikuwa ni ndoto ya Mwalimu Nyerere, wacha Afrika tufanye kazi kwa pamoja ndipo sasa tutaweza hata kujadiliana na Mabara mengine. Afrika tukiwa pamoja tutaweza kujadiliana na Marekani, tutaweza kujadiliana na Ulaya na nchi zingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli Waziri nakupongeza sana, Kamati imefanya kazi nzuri sana, ninaunga mkono hoja. Tuombe tu *TIC* wajitahidi kusaidia kuungana na *TIC* za maeneo mengine tuone namna ya kuboresha. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, atafuatiwa na Mheshimiwa Godwin Kunambi, Mheshimiwa Abdullah Mwinyi ajiandae.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nianze kwa kuunga mkono hoja ya Uanzishwaji wa Eneo Huru la Biashara la Nchi za Afrika. Kwa kweli nafikiri hili Azimio limekuja kwa wakati wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kulileta Azimio hili ambalo ni muhimu sana, lakini pia naipongeze sana Kamati ya Viwanda na Biashara kwa kuchambua kwa undani sana Azimio hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ina historia ndefu. Nchi yetu imekuwa ni nchi ambayo iliongoza mapambano ya ukombozi wa Afrika wa kisiasa na nchi zetu zote zimepata sasa uhuru, lakini tunabaki nyuma katika kuongoza mapambano ya ukombozi wa kiuchumi, Sasa hili Azimio lengo ni kuleta ukombozi wa kiuchumi. Ndiyo maana lengo la Azimio hili ni kuchochea uchumi na biashara katika nchi za Afrika. Kwa hiyo, mimi nafikiri ni wazo ambalo ni zuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu tusibaki nyuma, kila wakati tunatakiwa tuwe mbele, kama tulivyoongoza mapambano ya kupata uhuru tuongoze na mapambano ya kuleta uhuru wa kiuchumi. Kwa hiyo, hili mimi nafikiri lazima tuwe mbele. Pili, nchi yetu imekaa kijiografia mahali pazuri *(strategically located)*. Sasa lazima tutumie fursa hii ya nchi yetu kuwa *strategically located* ili tuweze kunufaika na biashara ya nchi hizi ambazo tumezisaidia sana katika kuleta ukombozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukichukua hali ya biashara Bara la Afrika linatisha. Sisi tunafanya biashara katika nchi za Afrika kwa asilimia 17, nchi za Ulaya asilimia 69, nchi za Asia asilimia 60, Mabara mengine yote ni zaidi ya asilimia 60. Kwa hiyo, umefika wakati lazima tufanye biashara na sisi, tufufue tuweze kufanya vizuri. Na mimi ninaamini hili litatusaidia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninao mfano hai. Nimeona kwa mfano wananchi wa kule Songwe wanavyopata shida hasa inapokuja katika kufanya biashara na nchi za jirani. Tuko

pale karibu tunapakana na Malawi na Zambia, tuko ni lango la SADC lakini tunapata shida kwa sababu ya kutokuwa na misingi na mambo mazuri ya kufanya biashara katika hizi nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano pale Tunduma unakuta kwamba wananchi wanaagiza mbolea Zambia, ina bei ya chini sana, iko bei ya chini kabisa, lakini ukichukua mbegu ziko bei ya chini sana na ziko mbegu nzuri kabisa zinazofaa kwenye kilimo. Wananchi wale wakienda kununua kule wanapozilingiza Tanzania wanavyofukuzwa, wanavyokamatwa utafikiri wamefanya uhaini. Kwa hiyo, hili suala mimi nafikiri kwamba tukianzisha haya maeneo yanatusaidia sana katika kuweza kutuachia biashara katika maeneo ya namna hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mambo ambayo lazima tuyazingatie na Mheshimiwa Waziri na Serikali lazima tufanye kazi kubwa ya kuhakikisha kwamba tunahamasisha ili nchi yetu iweze kupata manufaa ya hili Azimio.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ni tija. Tija katika bidhaa zetu kwenye kilimo iko chini, kama wenzangu walivyosema. Tija kwenye bidhaa zetu iko chini, bidhaa zetu haziwezi kushindana na bidhaa kutoka maeneo mengine. Kwa hiyo ni wajibu wetu sisi kuhakikisha kwamba tunaongeza tija ili bei iwe nzuri ili zi-*meet* ubora unaotakiwa wa kuweza kushindana katika hii biashara. Mimi naamini hiyo itatusaidia sana tukiweza kuifanya hivyo. Wameweka mifano ya bidhaa za kilimo, wameweka bidhaa mbalimbali mimi sitaki kurudia, lakini nataka kusema kwamba hilo ni suala la msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, tunapoenda kufanya biashara swali ambalo ni lazima tujjulize ni biashara ya namna gani tunakwenda kufanya. Tunasema kama ni biashara ya kuuza malighafi hiyo ni biashara mbaya. Biashara inatakiwa ukauze bidhaa zilizoongezwa thamani, hiyo ndiyo biashara ambayo inatakiwa tuingine nayo katika Bara la Afrika. Hapa tusijipe moyo kwamba tunakwenda kuuza malighafi au tunakwenda kufanya nini, hiyo haitatusaidia kwa sababu tunayo matatizo ya msingi katika nchi hii ambayo ni

kupunguza umaskini na kutengeneza ajira kwa watu wetu. Ili tuweze kufikia hayo yote lazima tujenge viwanda imara, tuongeze thamani ya bidhaa zetu, ndiyo tutaweza kutoa ajira na ndiyo tutaweza kupunguza umaskini wa watu wetu katika maeneo mbalimbali. Kwa hiyo, mimi nafikiri mkazo lazima uwe katika kuongeza thamani ya mazao yetu, ndiyo tutaweza kushindana vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo eneo lingine katika nchi za Afrika ambalo lazima tubadilike kifikra. Tuanze kujenga uaminifu, Waafrika walio wengi si waaminifu. Katika biashara sasa hivi tunazoenda kushindana tunaenda kushindana na baadhi ya nchi wapo watu ambao si waaminifu. Kwa hiyo na sisi lazima tujitahadhari na watu wetu wawe waaminifu. Ujue kabisa kwamba ukikopa unatakiwa ulipe, ukifanya biashara, ukiingia mkataba u-*deliver*. Kama inatakiwa upeleke bidhaa ndani ya wiki moja upeleke ndani ya wiki moja. Tukiendelea na uswahili wetu ambao tumeuzoea huu mimi nadhani kwamba hatutaweza kufanikiwa na kuona manufaa mapana ya azimio hili ambalo nafikiri ni muhimu sana katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi nataka kusema kwamba hili Azimio limekuja kwa wakati muafaka tuliunge mkono, tushikamane na Serikali tuhakikishe kwamba kweli tunaenda kunufaika na Azimio hili na wananchi wetu waandaliwe vizuri, wapewe elimu ya kutosha ili waende sasa, twende tukafanye biashara katika hizi nchi za Afrika na sisi tufungue mipaka na masoko ya bidhaa zetu yapatikane.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuunga mkono hoja. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Godwin Kunambi atafuatiwa na Mheshimiwa Abdullah Mwinyi, Mheshimiwa Exaud Kigahe, ajiandae.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kimsingi mimi nianze kwa kuunga hoja mkono.

Naunga mkono hoja ili nisije nikasahau huko mbeleni. Nianze mchango wangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania sasa tunapaswa kubadilika. Tuanze sisi viongozi na Watanzania wote kwa ujumla, tunabadilikaje? Ninavyozungumzia kubadilika namaanisha kwamba tunapaswa kufikiri kimkakati, yaani kila mmoja wetu afikiri kimkakati. Kufikiri kimkakati kutatusaidia kwa sababu kwanza tunakaribisha ushindani na kwenye ushindani maana yake anayeweza kuwa na uwezo katika kushinda atashinda tu, na sisi kwa bahati mbaya sasa, kwasababu hii ni fursa kwetu inaweza ikawa bahati mbaya kwetu sisi tukawa walaji na si wauzaji. Sasa lazima tufikiri kimkakati wote kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Uwekezaji pamoja na Wizara yetu ya Mambo ya Nje. Nianze na Wizara ya Mambo ya Nje. Tuna Balozi mbalimbali kwenye nchi mbalimbali hapa Afrika, Balozi zetu sasa nazo zifikiri kimkakati. Tunao Mabalozzi, lakini pia tuna maafisa ambao wapo Ubalozini. Je? tunaowapeleka kule; nimuombe pia Waziri wa Mambo ya Nje, tutazame wale maafisa wetu waliopo huko nje wapo kimkakati? Au tunawapeleka tu kwa sababu waende kutoa huduma kwenye balozi hizo. Nadhani nao tungepaswa kuwapeleka watu ambao wanakwenda kuwa Mabalozzi na maafisa ambao wapo kimkakati. Lakini pia na Balozi zetu pia zitumike kimkakati ili kuboresha biashara huko nje ya nchi ambako Balozi zetu zipo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niende eneo lingine. Nimezungumzia Wizara ya Viwanda na Biashara. Wizara ya Viwanda na Biashara sasa tubadilike na sisi tuwe walezi wa wafanyabiashara wa ndani ya nchi yetu. Kwa mfano; tunaona mtu kama Bakhresa, Azam ukienda takriban nchi zote za SADC anafanya biashara huko, tunaona mfano mzuri. Vilevile tunaona benki ya CRDB leo wapo Burundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu hawa wanapaswa kulelewa, na wakilelewa hawa wachache wengine

watavutiwa na wakivutiwa wengine maana yake pia itaongeza wigo mpana kwa wale wawekezaji nje ya nchi hizi ndani ya Bara letu la Afrika. Kwa hiyo Wizara ya Viwanda na Biashara sasa mnaweza kuwa walezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mzuri ni wenzetu China. Kampuni zote za ujenzi zinazokuja kujenga hapa Tanzania kutoka China zinakuwa *funded* na nchi zao, na China. Zenyewe zinapambana kutafuta *tender* zikipata *tender* zinakwenda kwao wanapewa fedha kwa ajili ya kuendelea na miradi ya ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, na sisi yamkini tukashindwa kuwapa fedha hawa wafanyabiashara ndani ya nchi yetu, lakini tuwa-*guarantee* tu, tunaweza kuwapa dhamana tu, kwamba Serikali ikawa dhamana ya Watanzania wanaokwenda kufanya biashara ndani ya Bara letu la Afrika. Hii itasaidia kwenda kwenye ushindani ambao na sisi utatupa manufaa makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini eneo lingine nizungumzie suala zima la taasisi za kifedha. Ukiitazama Kenya wana benki kadhaa hapa nchini ikiwemo *KCB*. Tujiulize Tanzania tuna benki gani kule Kenya? Sasa haya ni maswali ambayo kimsingi yanapaswa kutufikirisha ili na sisi tujipange kimkakati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia haitoshi, eneo lingine ni kuhusu suala zima la Sera na Sheria zetu, je, sera zetu na sheria zipo katika mtazamo ambao unaweza kutusaidia kama nchi kunufaika na mkataba huu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo haya ni mambo ambayo nadhani kimsingi tunakwenda kwenye ushindani ambao kimsingi lazima tujiandae. Kwa mfano; tunaweza kuanza na jambo la tunatazama tu kwenye *comparative advantage*. Kwamba sisi kama Watanzania ni eneo gani tumekuwa mabingwa kwenye uzalishaji na tukatumia eneo hilo kutusaidia ku-*compete* na wenzetu, mathalani kwenye mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, imezungumzwa hapa, na leo tumepata changamoto hapa, ni jambo ambalo wengine watatushangaa. Tukiwa tunajadili kununua mahindi leo hii, yaani dunia inatushangaa, dunia ingetutazama sisi tukiwa tunajadili kuuza unga, kwamba tayari tumeshafanya *processing* na si mahindi. Sasa tukiona tunafikiri kujadili mahindi tutoke kujadili mahindi tujadili bidhaa ambayo inakwenda kuuzwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, huko Kenya tunakopeleka mahindi tunapata hasara kubwa sisi, hilo lazima mjue. Tunapata hasara kubwa kwa sababu unauza mahindi, kuna pumba na yana vitu vingi ambavyo tunavipeleka Kenya. Kwa hiyo tusiendeleo kuuza *raw materials* tupeleke bidhaa ambazo tayari zimeandaliwa nchini. Na hili haliwezi kufanywa na Serikali, Serikali ibaki kuwa *regulator* na sekta binafsi sasa iende kwenye ku-*capture production*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninayasema haya lengo langu likiwa ni kuona kwamba kama nchi tunakwenda kunufaika na mkataba huu wa eneo huru la biashara ndani ya Bara letu la Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo katika haya narudia kusema kwamba inawezekana, inawezekana tukifikiri kimkakati, na kufikiri kimkakati kutatuwezesha sisi kwenda kuwa washindani kwenye eneo huru la biashara ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. naomba kuunga mkono hoja. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Abdullah Mwinyi atafuatiwa na Mheshimiwa Exaud Silaoneka Kigahe, Mheshimiwa Mtoa Hoja, Waziri wa Viwanda na Biashara, ajiandae.

**MHE. ABDULLAH ALI MWINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana nami kupata fursa hii na kuchangia katika hoja hii ya Uanzishwaji wa Eneo Huru la Biashara la Afrika

(Agreement Establishing the African Continental Free Trade Area).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hakika siku ya leo ni siku ya kihistoria ambayo, kama dada yangu Mheshimiwa Pindi Chana alivyosema, ni siku ambayo ndiyo chanzo cha ndoto za Baba wa Taifa mwanzilishi wetu kufika sehemu ya kuwa na Afrika moja. Siku zote nchi kuungana zinatakiwa ziwe na chachu na chachu kuu ya muunganiko ulimwengu mzima ni biashara na uchumi. Kuanza kufanya biashara kwa pamoja mkawa na soko moja ndiyo chachu kuu ya kuunganisha nchi au mabara kote ulimwenguni. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ndoto ya Baba wa Taifa ilikuwa Afrika iwe moja, na ndoto yakeni tofauti na Kwame Nkrumah, fikra zake ilikuwa Afrika iwe moja kwa kupitia *building blocks*. Kwame Nkrumah yeye alisema tuwe wamoja kuanzia siku ya kwanza, kama Muammar Gaddafi alivyokuwa anafikiria.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Baba wa Taifa alisema *through building blocks* ya Afrika Mashariki, ya SADC, COMESA na *Building blocks* nyingine. Na huu mkataba chanzo chake ndiyo hivyo, mazungumzo ya mkataba huu yalikuwa mazungumzo ya viongozi wa *Secretary General* wa *East African Community*, kipindi kile alikuwa Balozi Mwapachu, SADC na ECOWAS ndio chanzo, inakwenda sambamba na ile ndoto ya Baba wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wasiwasi mwingi mkumbwa niliuisikia leo ni kama Tanzania tupo tayari au la; na kama tumejipanga na kama tuna kasoro zozote. Kasoro hazikosekani kila nchi ina mapungufu yake. Lakini Tanzania na mfumo huu wa soko tayari sisi tumeshajifunza na tupo daraja la juu kabisa kulinganisha na nchi nyingi hizi za ndani ya Afrika, tofauti na tunavyojifikiria. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Jumuiya ya Afrika Mashariki ni jumuiya ya mambo mazito kabisa. Kwanza, Umoja wa Forodha, pili, Soko Huria ndani ya nchi hizi tano, tatu, Umoja



wa Kifedha. Kwa sehemu kubwa Umoja wa Forodha tayari umeshakamilika, na kwa kipindi ambacho sisi tupo toka mwaka 1999 mpaka leo; wakati tunaanza hofu kubwa ya Tanzania ilikuwa kuwa soko la Kenya kwa sababu kulikuwa kuna dhana ya kwamba Kenya ina uchumi mkubwa, ambao ni sahihi, na sisi kwa sababu uchumi wetu ni mdogo tutakuwa tu na watu wengi, tutakuwa tu soko la Kenya; lakini ukweli uliothabitika ni tofauti na hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipindi cha zaidi ya miaka sita mpaka saba leo Tanzania ina *positive balance of trade*. Maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba inauza zaidi katika masoko ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kushinda tunachokinunua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naona kuna kimya hivi kana kwamba hamuamini, angalieni takwimu. Tanzania inauza bidhaa yenye thamani kubwa Kenya kushinda inachonunua kutoka Kenya kuja Tanzania kwa zaidi ya miaka sita. Hali kadhalika Tanzania tunauza vitu vingi Uganda kushinda tunachonunua. *The same* Rwanda, na Burundi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ki ukweli kama Mheshimiwa hapa mmoja aliyezungumza hatuna tatizo lolote na wajasiliamali na wafanyabiashara wetu. Tatizo muda hadi muda tunawafunga minyororo wanashindwa kufanya kazi vizuri zaidi, lakini juu ya hivyo tuna mifano ya kampuni za kitanzania ambao wanafanya biashara nchi zaidi ya kumi na mbili na nyingine kumi na nane na zina-*compete* vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakupa mfano; Azam ipo ndani ya Afrika inafanya biashara nchi 15, MeTL nchi 18, *export trading* nchi 12, *MM Steel Intergrated* nchi 13, wamekwenda huko wanaendesha viwanda vikubwa na wanaweza ku-*compete*. Sasa huu umoja umuhimu wake ni soko, soko ni watu. Ukiangalia nchi ambazo zimeendelea kwa haraka sana kama vile China, India, Brazil, Marekani, nchi zote hizi zina kitu kimoja, zina watu wengi. Jumuiya Afrika Mashariki ina watu zaidi ya milioni 200, hili eneo lote hili

litakuwa na watu zaidi ya bilioni moja, hii ni fursa adhimu sana kwa Tanzania kujipambanua na kuuza nje ya soko. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nini tunachokuiza kikubwa Kenya na ndani ya Jumuiya Afrika Mashariki ni mazao, Tanzania inalisha Afrika Mashariki katika kuzalisha, na tunalisha mpunga, vitunguu, machungwa na mananasi. Kimsingi tunaweza ku-*compete*.

Mheshimiwa Naibu Spika, wiki iliyopita, nikimalizia, nilikuwa naangalia *You Tube* kupitia *Internet* kuangalia katika sekta ya muziki, kwa sababu nimekaa na kaka yangu hapa naona niugusie, sekta ya muziki. Nikaangalia katika *You Tube*, ni muziki gani inasikilizwa Nairobi kwenye ile *top ten* ya *You Tube*. Katika *top ten* wana muziki saba wa Tanzania wakiongozwa na *Diamond Platinums*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nazungumzia hilo, vijana wetu hawana hofu ya kupambana wakati sisi tunafunguka *Music Industry* Nairobi ilikuwa imefika daraja kubwa kushinda sisi, lakini wale vijana hawakuwa na hofu. Leo hii Afrika Mashariki yote vijana wetu wana *dominate*. Hii ni *message positive* kwamba Tanzania mapungufu tunayo, tunajua matatizo yetu yapo wapi, lakini tunauwezo mkubwa sana wa kupambana na kushindana na kupata manufaa makubwa katika hili eneo huria la biashara. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. ABDULLAH ALI MWINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. naomba kuunga mkono hoja. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Exaud Silaoneka Kigahe atafuatiwa na Mtoa Hoja.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia kwenye hoja hii muhimu ya kuridhia Azimio la Eneo Huru la Biashara Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nianze kwa kuunga mkono hoja, na kimsingi kama ambavyo wajumbe wengi wamesema labda na mimi niseme tu kidogo. Eneo Huru la Biashara Afrika ni utaratibu wa pamoja wa Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika unaolenga kuchochea uchumi na biashara miongoni mwa nchi wanachama.

Mheshimiwa Naibu Spika, na kama walivyochangia wachangiaji wengi na kukubaliana na Azimio hili, lengo hasa litakuwa ni kufunguliana masoko ya biashara ya bidhaa na huduma, kuondoleana ushuru wa forodha, pamoja na kulegeza vikwazo na masharti mbalimbali ili kuhakikisha Afrika tunafanya biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, wachangiaji wengi wamekubaliana, lakini wametoa baadhi ya maoni kwa upande wa Serikali. Na mimi kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba maoni haya tunayachukua na moja ya mikakati ambayo tunaenda kuitekeleza ni kuhakikisha tunaendeleza kuimarisha mazingira bora au wezeshi ya kufanya biashara katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia katika hilo kweli kulikuwa kuna changamoto kidogo, kama walivyosema Waheshimiwa Wabunge, na tuliona baadhi ya hata wafanyabiashara wakubwa wakiondoka, wakiondoa mitaji yao na kuwekeza katika nchi zingine, lakini sasa baada ya maboresho yanayoendelea hasa kupitia *blue print* kama mlivyosema Waheshimiwa Wabunge tunaona tayari wawekezaji wengi wanaanza kurudi kuwekeza hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, maana yake hili ni *move* nzuri ambayo na sisi tuitumie nafasi hii sasa kuvutia mitaji mingi kwa kuweka mazingira wezeshi ili tuanze kuzalisha nchini na kuuza katika eneo hili la biashara la Afrika kwa faida zaidi kulingana na utaratibu tunaondana nao sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia, wameongelea kuhusiana na kuhakikisha sekta binafsi inawezeshwa au

inashirikishwa. Hili tunalichukua na kuhakikisha kweli sasa tunaenda ku-engage; na kama ulivyosema wengine tayari sekta binafsi imeshasema faida kubwa ambayo wataenda kuipata au manufaa makubwa ya Tanzania kuridhia mkataba huu wa eneo huru la biashara Afrika, kwamba wao wataenda kufaidika Zaidi, na ni wengi wamesema.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia tutaendelea kuimarisha uwezo wa uzalishaji wa ndani na hasa kwenye kukidhi viwango, kwa maana ya kuhakikisha unahamasisha uzalishaji wa tija kwenye bidhaa zetu lakini na mazao. Kama walivyosema wengine, kwamba angalau sasa bidhaa zetu na mazao yetu yawe shindani kulingana na soko la sasa, lakini hasa kwenye hili soko la Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia, wameongelea kuhusiana na sekta ya biashara ndogo, kwamba lazima hawa nao pia tuendeleo kuwawezesha. Ni kweli, tuhakikishe sasa sekta ndogo kwa maana wajasiliamali waweze kuzalisha kibiashara kwa kuhakikisha kwamba vifungashio vyao vinakuwa vya viwango, lakini pia hata ubora; na hii tunaenda kuhakikisha tunafanya hivyo kwa sababu sasa hivi tunaenda kuandaa sera ya ubora. Tuwahakikishe Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote kwamba tutaenda kutekeleza au tutaingia tukiwa na nguvu katika soko hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kwa ujumla wake Waheshimiwa Wabunge wameongelea sana kuhusiana na umuhimu wa sisi kama Bara la Afrika kuanza sasa kuishi pamoja, kwa maana ya kufanya biashara pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli changamoto mojawapo kubwa sana katika kufanya biashara katika bara letu ni miundombinu. Kwa mfano; utakuta mtu anataka kwenda labda hata Kongo tu hapo, kama kwa njia ya ndege maana yake lazima uende Ethiopia au hata nchi za nje ili kesho yake ulale, uje Kongo, DRC. Sasa unakuta miundombinu hii ndiyo imekuwa na changamoto kubwa sana ya sisi kwenye kufanya biashara katika Bara la Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo moja wapo ya vitu ambavyo vitaenda kutupelekea kuhakikisha sasa tunaimarisha miundombinu yetu hii ni moja ya fursa ambayo naamini, kama alivyosema Mheshimiwa Mwijage na mwingine, kwamba sasa miundombinu hii itajengwa kwa sababu tunajua tunakwenda kufanya biashara kati ya nchi na nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili pia, naona kwa mfano; hata kwenye njia tu za barabara watu wanaouza mazao mbalimbali ikiwemo hata mbao kupeleka Kongo badala ya kukatisha hapa tunaenda mpaka Zambia halafu uanze kurudi hivi. Maana yake kwa miundombinu hii inapelekea bidhaa zetu kuwa *uncompetitive*, kwamba zitakuwa sasa haziwezi kushindana na bidhaa hata za kutoka ulaya kwa sababu ya miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niwaombe, kama ambavyo wote wamekubali, kwamba tuunge mkono Azimio hili kwa sababu lina manufaa mengi kwa nchi yetu, lakini pia kwa Bara zima la Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.  
(*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Sasa nimkaribishe mtoa hoja ili ahitimishe hoja yake, Mheshimiwa Prof. Kitila Alexander Mkumbo, karibu.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kukushukuru sana kwa jinsi ambavyo umeendesha mjadala huu na kutupa nafasi ya kuweza kuwasilisha Azimio hili. Nimshukuru sana Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuruhusu Mkataba huu uwasilishwe hapa Bungeni kupitia Baraza lake la Mawaziri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka nichukue nafasi hii pia kumshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, Mheshimiwa David Kihenzile na Makamu wake Mheshimiwa Eric Shigongo na Wajumbe

wote kwa nafasi ambayo walipata ya kuchambua kwa kina sana Mkataba huu. Nikutaarifu tu kwamba siku tunajadili Mkataba huu, tulikuwa na Wenyeviti wa Kamati wengine walikuja kushiriki zaidi ya Wenyeviti watano. Kwa hivyo, siku ile ilikuwa ni mjadala mzuri sana na Waheshimiwa walipata nafasi ya kuchambua na kuuliza maswali na sisi ni wataalamu tuliweza kuwajibu ipasavyo. Pia nichukue nafasi hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamepata nafasi ya kuchangia, kwa hoja zao lakini pia kwa uwingi wao na ujumla wao kwa kuunga mkono hoja hii. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu kwa kiasi kikubwa karibu Wajumbe wote wameunga mkono hoja hii, sitaki kutumia nafasi hii kuchukua muda wako mwingi katika kujibu. Naomba nitoe ufafanuzi kwa maeneo machache sana katika kuhitimisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kutoka kwa Kamati walitoa maoni na mapendekezo kwamba ni muhimu sana tukachagua bidhaa za kulindwa kwa umakini mkubwa. Nataka tu nilitaarifu Bunge lako kwamba katika Mkataba huu na katika majadiliano ambayo tumeyafanya kwa sasa tumekamilisha majadiliano kwenye Itifaki tatu; Itifaki ya Biashara ya Bidhaa; na Itifaki ya Biashara ya Huduma na Utatuzi wa Migogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukubaliana huku tumegawa bidhaa katika makundi makubwa matatu. Kuna kundi la kwanza ambapo tunajadiliana tufikie asilimia 90 na Wakuu wa Nchi na Serikali waliagiza kwamba ili biashara ianze kufanyika tukubaliane kufanya biashara katika angalau asilimia 90 ya bidhaa. Sisi tuna-*negotiate* kama Afrika Mashariki na tumeshakubaliana asilimia 86, majadiliano yanaendelea ili tupate bidhaa tufike asilimia 90.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kundi la pili ni asilimia 7 ambazo hizi hatutaingia kwa sasa, tutaingia katika kipindi cha miaka 13 ijayo. Hizi ni bidhaa ambazo zitaingia katika soko hili baadaye katika miaka 13.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna kundi la tatu ambalo ni asilimia 3, hizi ni bidhaa ambazo hatutaingia kabisa. Hizi ni bidhaa ambazo nchi zimekubaliana zipo kwenye kitu kinaitwa *exclusion list* kwamba zenyewe hazitakuwa sehemu ya bidhaa ambazo zitafunguliwa masoko haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo, wataalamu na Serikali tumekaa tayari tunaendelea na majadiliano kuona kwamba ni bidhaa gani ziingie kwenye asilimia 3, zipi ziingie kwenye asilimia 7 na zipi ambazo ziingie kwenye asilimia 90. Kwa hivyo, Serikali ipo makini kwenye jambo hili lakini pia Mkataba umetoa mawanda mapana kuhakikisha kwamba nchi zinalindwa katika hatua zake za viwanda na biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya pili, nataka tu niseme kwamba tayari sisi kama Tanzania tuna-*advantage* ukilinganisha na wenzetu kwa sababu sisi tayari tupo katika nchi 19, kwa maana ya kwamba sisi ni Wajumbe wa *EAC* na Wajumbe wa *SADC*, kwa hiyo, tayari tulishafunguliana masoko yetu. Kwa hivyo, sisi ni wazoefu wa kutosha, katika nchi zote 54 tayari sisi tunafanya biashara na nchi 19, kwa hivyo, hili jambo siyo jipya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama walivyosema wengine, tathmini imefanyika kwa kina sana na Wizara ya Fedha na Mipango kuona matokeo chanya na hasi ya kujiunga na Mkataba huu. Hitimisho ni kwamba matokeo chanya ni mengi zaidi na kwamba ni lazima twende kwenye Mkataba huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama walivyosema wengine, nikitoa mfano tu takwimu za mwaka jana tumeuza *EAC* dola milioni 812 ukilinganisha na zile ambazo tumeingiza Tanzania dola za Kimarekani milioni 324. Kwa hivyo, tunauza zaidi kuliko vile ambavyo tunavyonunua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *SADC* tumeuza dola za Kimarekani milioni 999 wakati ambazo tumenunua sisi ni dola za Kimarekani milioni 604. Kwa hivyo, hakuna kipya ni kwamba

uzoefu tunao na kama walivyosema Waheshimiwa Wabunge tunafanya vizuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja nyingine niitolee ufafanuzi kuhusu hizi tozo, Mheshimiwa Rais alishatoa maelekezo kwamba lazima tufanye *review* na kuna *review* kubwa inaendelea kuhusu tozo mbalimbali jinsi ambavyo tunakamilisha biashara. Tunaamini kwamba mwaka huu tutapata suluhu kwa baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nieleze hili la *ETS* na *VAT refund* ambalo Mheshimiwa Mwanyika aliliongelea, kama ambavyo mnafahamu, tayari Serikali imeshaanza kulipa *VAT refund*. Sisi tumeshapokea pongezi nyingi kutoka kwa wafanyabiashara wakishukuru sana kitendo ambacho Serikali imefanya cha kuanza kuwalipa *VAT refund*. Pia *ETS* tunafanya majadiliano na Wizara ya Fedha na wafanyabiashara ili kuona kwamba gharama za huduma hii zinapungua, tumeshakubaliana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja nyingine ambayo ni ya msingi pia imetolewa na Waheshimiwa Wabunge kuhusu utafiti za kina na hili aliliongelea Mheshimiwa Aida juu ya faida na hasara. Kama nilivyosema Serikali imefanya utafiti wa kutosha sana lakini pia watafiti huru wameshiriki kwenye suala hili. Tunao utafiti wa *REPOA* na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na wame-*publish study* mbili hapa muhimu kabisa na zote ni mpya za mwaka jana. Moja, inaitwa: "*Cost and Benefits of Regional Integration in Tanzania: Case Study of African Continental Free Trade Area*". Hitimisho lao ni kwamba Tanzania ijiunge na eneo hili mapema sana kwa sababu kuna faida kubwa kuliko hasara.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini *study* ya pili ambayo wameifanya inasema: "*Regional Integration and Tanzania's Export Performance*" wakiifanyia *EAC* na *SADC*. Katika *study* yao wameonyesha wazi kwamba Tanzania katika miaka 10 iliyopita imekuwa ikifaidika sana kuwa Mjumbe wa *EAC* na Mwanachama wa *SADC* katika suala zima la biashara.



Hitimisho lao ni kwamba hatuna sababu ya kuogopa, tujiunge haraka kwa sababu kwa kweli nchi inakwenda kufaidika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama walivyosema Waheshimiwa Wabunge hatuna sababu ya kuogopa. Tupo tayari na Serikali imefanya maandalizi ya kutosha sana kwa ajili ya kujiunga na eneo hili. Pia wafanyabiashara tumefanya nao kazi sambamba na kwa kweli wao wangetaka tujiunge juzi sio leo. Kwa mfano, hata leo asubuhi wameniidikia *email* kunitakia kila la kheri katika kuwasilisha Azimio hili na kuwaomba sana Waheshimiwa Wabunge waridhie. Kwa hiyo, napenda kusema kwamba Serikali imejiandaa, wafanyabiashara wamejiandaa na tupo tayari kufanya kazi na wenzetu katika eneo hili la biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nihitimishe kwa kusema kwamba nchi yetu iliongoza mapambano ya ukombozi wa kisiasa katika Bara la Afrika. Sisi ndio tulikuwa viranja, tunapoanza mapambano ya ukombozi wa kiuchumi hatuwezi kubaki nyuma. Mkataba huu unatupa fursa ya Tanzania kuchukua nafasi yake katika Bara la Afrika katika kuongoza mapambano ya kujikomboa kiuchumi. Niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge waridhie Azimio hili ili tuanze safari hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri mtoa hoja.

Waheshimiwa Wabunge, sasa kwa utaratibu wetu nitawahoji kuhusu hoja ya Waziri wa Viwanda na Biashara ya Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa Eneo Huru la Biashara la Afrika (*The Agreement Establishing African Continental Free Trade Area - AFCFTA*).

*(Hoja Ilitolewa lamuliwe)  
(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa Eneo Huru la Biashara la Afrika (The Agreement Establishing African Continental Free Trade Area - AFCFTA) lilipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji katika Wizara hii kwa kufanya haraka kuleta Mkataba huu lakini pia, kwa kufanya utafiti uliowezesha ninyi ndani ya Serikali kuona umuhimu wa kuleta Mkataba huu uweze kuridhiwa na Bunge, ninawapongeza sana. *(Makofi)*

Pia kwa namna Wabunge walivyounga mkono Azimio hili ni dhahiri kwamba Kamati yetu mliiridhisha na majibu kwa maswali mbalimbali waliyokuwa nayo. Hata Wabunge waliopata fursa ya kuchangia humu ambao sio Wajumbe wa Kamati hii, wameonyesha namna ambavyo Mkataba huu una manufaa mengi kwa nchi yetu na sisi nchi yetu kama sehemu ya nchi zingine lazima tuwe tayari kwa ajili ya ushindani. Naamini Wizara hii kwa sababu ndiyo iliyoleta Mkataba huu basi itaweka mazingira mazuri kuwezesha wafanyabiashara wa nje kuja hapa ndani kirahisi ili na sisi pia tunapoenda huko nchini kwao kufanya biashara basi mazingira yetu yawe mazuri pia. Kwa hiyo, tunawatakia kila la kheri katika utekelezaji wa Mkataba huu ambao Bunge limeridhia siku ya leo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nichukue pia fursa hii kuipongeza sana Kamati yetu kwa kazi nzuri waliyoifanya. Ninyi wote ni mashahidi kwamba wameuchambua Mkataba huu na wametueleza faida na hasara. Zile hasara walizosisema Serikali itaanza kuzifanyia kazi ili wananchi wetu waweze kufaidika katika kuungana na nchi zingine za Afrika kwenye kufanya biashara. Kwa hiyo, kwa nafasi hii niwashukuru Wabunge wote pia mliopata fursa ya kuchangia Mkataba huu na tuwatakie kila la kheri, Wizara kwenye

utekelezaji wa yanayojiri baada ya Bunge kuridhia Mkataba huu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, wakati wa kipindi cha maswali na majibu, Mheshimiwa Dkt. Pallangyo alisema Wizara haijajibu swali alilokuwa ameluliza na Kanuni yetu ya 53 inaeleza kwamba maswali yanatakiwa kujibiwa kikamilifu na fasili ya (1) inatoa maelezo hayo sina haja ya kurejea lakini fasili ya (4) inasema hivi: "Iwapo Spika ataridhika kuwa, swali la msingi au la nyongeza halijapata majibu ya kuridhisha, ataagiza lijibiwe kwa ufasaha zaidi katika kikao kingine cha Bunge". Maana yake Mbunge anaposema hajaridhika na majibu au anaposema Serikali haijajibu swali lake kikamilifu, mimi nikisoma swali lililoulizwa na Mbunge lakini majibu yaliyotolewa na Serikali kama nitajiridhisha kwamba Serikali haikujibu kikamilifu nitaagiza swali hilo liweze kujibiwa tena.

Sasa kwa muktadha huo swali namba 96 lilikuwa limeuliza kwa ujumla na Serikali imekuja pia na majibu ya jumla kama ambavyo Mbunge alikuwa ameuliza. Kwa ajili ya faida ya Waheshimiwa Wabunge kwa sababu swali hili lipo kwenye Vishikwambi vyetu kwa hiyo, mnaweza kulipitia baadaye lakini swali ni fupi kwa hivyo nitalisoma, linasema: "Je, ni lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami barabara zinazopanda milimani Arumeru Mashariki ili kuwafikishia wananchi huduma pamoja na kupunguza gharama za matengenezo ya mara kwa mara kwa barabara hizo ambapo gharama zake ni kubwa kutokana na ugumu wa kijiografia?" Swali hili halikuwa limetaja ni barabara zipi anazozitungumzia Mbunge, kwa hivyo, alikuwa anaongelea barabara zote ambazo zinaelekea milimani.

Serikali hapa sehemu ya kwanza kwenye majibu wameeleza barabara ambazo zimefanyiwa kazi kwa kiwango cha changarawe. Wamezitaja hapa kwa kilomita na idadi ya barabara hizo na kwa majina yake. Sehemu ya pili ya majibu ya Serikali wameeleza kwamba katika mwaka wa fedha 2020/2021, Serikali ilifanya matengenezo, wameeleza hapo ni barabara gani ambazo zilifanyiwa

matengenezo ambazo zinaelekea huko milimani, zimetajwa hapo.

Sehemu ya mwisho ya hiyo sehemu ya pili kwa maana ya sentensi ya mwisho inasema: "Pamoja na ujenzi wa barabara ya Sangis-Nambala kilomita 1.9 kwa kiwango cha lami kwa jumla ya gharama ya shilingi bilioni 1.38". Halafu Serikali itaendelea kutenga fedha na Serikali itaendelea na ujenzi, hayo yote yameelezwa hapo. Kwa namna swali lilivyoulizwa na kwa namna majibu yalivyotolewa, kwa sababu swali halikuuliza barabara ipi mahsusi, Serikali imetaja barabara ambayo inaelekea milimani ambayo imetengenezwa kwa kiwango cha lami na imeeleza ambazo imetengeneza kwa kiwango cha changarawe.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Pallangyo ulivyosema Serikali ilikuwa haijajibu swali lako kikamilifu swali lako umeuliza kwa jumla, Serikali imejibu kwa jumla kwa hivyo, kama kuna barabara mahsusi ambazo unataka sasa Serikali izisemee utazipeleka kama swali lingine. Kwa hivyo, mwongozo kwa mujibu wa hiyo Kanuni ya 53 kuhusu maswali kujibiwa kikamilifu Swali Na. 96 la Mheshimiwa Dkt. John Daniel Pallangyo limejibiwa kikamilifu na Serikali. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa nane mchana.

*(Saa 12:37 Jioni Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 10 Septemba,, 2021 Saa Nane Mchana)*